# Nipashe

Alhamisi Novemba 21, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580081

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Ashambuliwa na fisi usiku wa manane akiwa kitandani

UKURASA 3




UKURASA 13



# MAGUFULI AWEKA MSIMAMO MAHINDI

•**ASEMA** hakuna kupanga bei elekezi, asisitiza wakati wa mkulima kufaidi, amwamuru kigogo Nida kutoa vitambulisho...

UKURASA 2

Distributed via ippmedia

## WABUNGE CHADEMA WAPEWA ONYO KALI

UKURASA 3

Scan Hapa



Pakua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

# Serikali yashtushwa kasi kuvunjika ndoa

UKURASA 2

**MICHEZO** POCHETTINO ANASTAHILI SANAMU SPURS- CROUCH UK. 29

MAONI, KATUNI UK.6

# JPM aweka msimamo bei ya mahindi

**Na Mary Geofrey**

HUKU kukiwa na kilio cha kupaa kwa bei ya mahindi na unga utokanao na nafaka hiyo nchini, Rais John Magufuli amesema hataingilia suala la kupanda kwa bidhaa hizo.

Juzi, serikali kupitia Wizara ya Kilimo, ilieleza kuwa bei ya mahindi imepaa hadi Sh. 107,000 kwa gunia, kulinganishwa na Sh. 65,000 katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Akiwa safarini jana kuelekea Dodoma kwa ajili ya ziara ya kikazi, Rais Magufuli alitoa msimamo huo aliposimama eneo la Dumila mkoani Morogoro.

Alisema malalamiko ya watu kuhusu bei ya mahindi ndiyo furaha ya wakulima ambao wamelima mazao hayo kwa shida.

Alisema serikali yake haitapanga bei elekezi katika zao hilo pamoja na uwapo wa malalamiko kuwa bei ya zao hilo imepanda na kusababisha unga kuuzwa kwa bei ghali.

Alisema watu wanapaswa kufahamu kuwa muda wa kuwapangia bei za mazao wakulima umeshakwisha kwa kuwa katika kipindi chake hatapanga bei ya mazao kwa wakulima.

"Kwa hiyo, hili nataka niwaeleze ndugu zangu, wakati wa kuwapangia bei wakulima na mazao yao umeshakwisha, katika kipindi changu, sitapanga bei ya mkulima na mimi ni mtoto wa mkulima, ninafahamu maana ya kulima.

"Sasa, wale wanaotaka bei nzuri ya mahindi, mpunga au tikiti maji, huu ndo wakati wa kutengeneza bei nzuri, mvua inanyesha, ndiyo niwambie ndugu zangu wa Morogoro, mkoa huu ni miongoni mwa mikoa muhimu katika uzalishaji wa chakula, limeni.

"Narudia tena, ukiona mahindi yapo bei ya juu, nenda kalime

INAENDELEA UK. 8


Distributed via ippmedia

Rais mstaafu, Ali Hassan Mwinyi, akijiandaa kutia saini maazimio ya watoto wanayotaka yatekelezwe katika maadhimisho ya 30 tangu kupitishwa azimio la kimataifa la haki ya mtoto yaliyoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), kwa kushirikiana na serikali, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yashtushwa kasi ndoa kuvunjika

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imeshtushwa na ongezeko la kuvunjika ndoa kwa muda mfupi baada ya kufungwa na kuwaomba viongozi wa dini kuingilia kati suala la malezi na maadili ya familia.

Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndungulile, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto (Unicef) kwenye maadhimisho ya miaka 30 ya Azimio la Kimataifa la Haki za Watoto.

Tanzania ilitia saini mkataba huo Juni 1, 1990 na kuuridhia Juni 10, 1991 na maadhimisho hayo ni kuikumbusha dunia kuwa, watoto wana haki ambazo hazistahili kupuuzwa.

Akieleza tatizo la kuvunjika kwa ndoa, Dk. Ndungulile alisema masuala ya malezi na maadili kwa watoto kwa sasa ni changamoto na yamesababisha ongezeko la ndoa kuvunjika na ukatili wa watoto.

"Ndoa kuvunjika ndani ya mwaka mmoja baada ya kufungwa zimeongezeka zaidi, niwaombe viongozi wa dini masuala ya makuzi na malezi na msingi ya familia muyasemee," alisema.

Alisema viongozi wa dini wanafungisha ndoa, lakini ndani ya siku tatu, sita au mwaka zinavunjika.

**TALAKA 1 KILA BAADA YA SIKU 2**

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, katika wasilisho lake bungeni Aprili 17, mwaka huu, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka huu wa fedha, alibainisha kutolewa kwa talaka moja nchini kila baada ya siku mbili.

Balozi Mahiga alibainisha Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita) ulifanikiwa kusajili ndoa 26,953 na talaka 122 katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha uliopita (yaani kuanzia Julai 2018 hadi Machi mwaka huu).

Kwa takwimu hizo za wizara, ina maana kwamba, kila mwezi kuna talaka 14 zinazosajiliwa nchini, sawa na talaka moja kila baada ya siku mbili.

Akitaja changamoto ya ndoa kuvunjika, Dk. Ndungulile, alisema watoto wa sasa wanalelewa na mzazi mmoja hivyo kuleta tatizo kwenye malezi yao.

Imeelezwa kuwapo kwa idadi kubwa ya watoto duniani wanaokabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo ukiukwaji wa haki za mtoto na ukatili wa aina mbalimbali kama vipigo, kubakwa, mimba na ndoa za utotoni, ukeketaji, ulawiti, vitisho, umasikini unaowanyima mahitaji ya msingi, utumikishwaji, kuhusishwa na vita vinavyosababisha ulemavu na hata kupoteza maisha. "Lengo la kuadhimisha siku hiyo ni kuelimishana na kuikumbusha jamii hasa wazazi na walezi wajibu wao katika kuhakikisha watoto wanapata haki zao za msingi," alisema Dk. Ndungulile.

Vile vile, katika kuimarisha usimamizi na utoaji wa haki na ulinzi wa mtoto, serikali imezindua mpango kazi wa taifa wa miaka mitano (2017/18-2021/2022) wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Kupitia mpango huo kamati za ulinzi wa wanawake na watoto ambao ndiyo wasimamizi wakuu wa usalama wa wanawake na watoto zimeanzishwa katika ngazi mbalimbali na jukumu lake ni kuratibu vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kuanzia ngazi ya taifa, mikoa hadi mamlaka za Serikali za Mitaa.

## Bana matumizi Udom yaokoa milioni 400/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHUO Kikuu cha Dodoma (UDOM), kimepunguza idara zake kutoka 62 hadi 30 na kuokoa Sh. milioni 400 ambazo zilikuwa zikitumika kwa mwaka kulipa kodi ya pango kwenye nyumba za wafanyakazi na watalaamu kutoka nje ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Makamu Mkuu wa UDOM, Prof. Faustine Bee, alisema wamefanikiwa kupunguza gharama kwa kuwajengea nyumba watalaamu waliokuwa wakiishi nje ya chuo hicho awali.

"Gharama hizi ni kubwa sana kwa chuo, ndiyo maana tuliamua kukaa na kupunguza vitu hivi pia tunatarajia kujenga majengo mawili ya ghorofa yenye uwezo wa kuchukua familia 30 na kujenga nyumba tatu za viongozi, hivyo familia 33 zitapata mahali pa kuishi na ujenzi huu tutatumia fedha za ndani," alisema Prof. Bee.

Kuhusu kufutwa kwa machapisho, alisema UDOM kimeyafuta majarida hayo kufuatia uamuzi wa seneti ya chuo kutokana na kuonekana hayana ubora.

"Waliopanda madaraja kupitia majarida hayo hawataathirika na chochote," alisema Profesa Bee.

Pia, aliwataka wafanyakazi wake watafute ufadhili wa masomo ili kujiendeleza na kupunguza mzigo kwa chuo.

"Awali wakati chuo kichanga kilikuwa kikisomesha wafanyakazi wake kupitia mapato ya ndani, lakini hivi sasa hatufanyi hivyo," alisema Prof. Bee.

Alisema kinachotakiwa hivi sasa wafanye jitihada za kutafuta wafadhili hao ili kujiendeleza wao mwenyewe.

Kuhusu kupatiwa cheti cha ithibati kutoka TCU kwa kipindi cha miaka mitano na kujifanyia tathmini ili kupatiwa cheti kingine cha ithibati baada ya miaka mitano mingine, alisema wamefanya pia ukaguzi wa taaluma za wafanyakazi wake ili kuwa na watu wanaostahili na kufanya kazi katika idara kulingana na taaluma zao.

Katika hatua nyingine, Prof. Bee alisema suala la unyanyasaji wa kijinsia, chuo kimeunda Tume ya kudhibiti mienendo hiyo inayosikika katika chuo hicho na vyuo vingine.

"Wafanyakazi wamekuwa wakiomba rushwa ya ngono au fedha kwa wanafunzi suala hili halikubaliki hata kidogo," alisema Prof. Bee.

Aliomba ushirikiano kwa wanafunzi ili kuwabaini wafanyakazi wenye tabia hiyo isiyofaa.

HABARI KITAIFA

# Mahakama yatoa onyo kali wabunge Chadema

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imetoa onyo kali na kuwaachia huru wabunge wanne wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mbunge wa Iringa mjini, Peter Msigwa na wenzake watatu wanaokabiliwa na kesi ya uchochezi baada ya kulala mahabusu kwa kukiuka masharti ya dhamana.

Kadhalika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, imempa muda Msigwa wa kupeleka mahakamani taarifa kama mdhamini wake mmoja kati ya wawili aliyedaiwa kukihama Chadema kama bado ana mdhamini au la.

Mbali na Msigwa wengine ni, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, wa Kawe Halima Mdee na Bunda, Ester Bulaya wote kwa pamoja walifikishwa mahakamani hapo jana wakiwa chini ya ulinzi mkali wa Jeshi la Magereza wakitokea mahabusu ya Segerea, jijini Dar es Salaam baada ya kukiuka masharti ya dhamana kwa kushindwa kufika mahakamani.

Akisoma uamuzi huo, hakimu alisema pamoja na washtakiwa kutoa hoja za kushindwa kufika mahakamani, lakini hazikuwa na msingi.

"Mahakama hii inaona kuwafutia dhamana itakuwa adhabu kubwa, inatoa onyo kali tabia yenu washtakiwa isijirudie kesi inapopangwa lazima mfike kwa wakati msipoteze muda wa mahakama," alisema hakimu.

Alisema siku ya kesi watuhumiwa wanne na wadhamini wao waliwahi kwa wakati mahakamani na kuhoji kwa sababu gani wao wanne na wadhamini wao walishindwa kufika kusikiliza kesi yao na kwamba ina maana walikusudia jambo hilo.

"Nachukulia wamefanya makusudi kwa nini washtakiwa wote wanne washindwe kuwahi na wadhamini wao, kitendo chao cha kujisalimisha Polisi Oysterbay kimetokana na kuogopa, kuhusu Msigwa mdhamini wako kuhama chama hakikisha unaleta taarifa kama amejitoa au la, na wewe Heche walete wadhamini wako kabla ya Novemba 29, mwaka huu," alisema Hakimu Simba wakati akisoma uamuzi huo. Kesi hiyo imepangwa kuendelea kusikilizwa ushahidi wa utetezi Novemba 26, mwaka huu na dhamana zenu washtakiwa zinaendelea.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakurugenzi wa Mashtaka Wasaidizi, Faraja Nchimbi, Joseph Pande, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, Mawakili wa Serikali, Jaqline Nyantori na Salim Msemo.

Mapema Ijumaa ya wiki iliyopita mahakama hiyo ilitoa hati ya kukamata washtakiwa wanne hao kwa kukiuka masharti ya dhamana pamoja na wadhamini wao kwenda kujieleza kwanini hawakutimiza wajibu wao kuwapeleka washtakiwa mahakamani.

Washtakiwa hao walikiuka masharti hayo kwa kushindwa kufika mahakamani hapo bila kutoa taarifa.



Muuguzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, Nyanjura Mjuberi akimhudumia Deus Charles (37) aliyelazwa hospitalini hapo juzi, baada ya kuvamiwa na kupigwa na watu watatu katika Kata ya Busoka wilayani humo, mkoani Shinyanga Novemba 13 mwaka huu, na kumvunja mguu na mkono, kwa kilichodaiwa kuwashinda katika michezo ya kubahatisha. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Ashambuliwa na fisi usiku akiwa amelala

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa kijiji na kata ya Chela, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, Buluba Jilasa (70), amevamiwa na kushambuliwa na fisi kisha kung'atwa sehemu mbalimbali za mwili wake.

Uvamizi huo pia umesababisha kukatwa kwa kiganja cha mkono wa kushoto kilichokuwa kimeshambuliwa vibaya.

Akieleza kwa uchungu akiwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama, Jilasa alisema tukio hilo lilitokea majira ya saa nane usiku wa kuamkia jana akiwa amelala.

Jilasa alisema alishituka mlango ukivunjwa na kukutana uso kwa uso na mnyama huyo.

Alisema alianza kupambana na fisi huyo ili asimdhulu lakini baadaye fisi alibugia kiganja cha mkono wa kushoto na kumjeruhi sehemu ya mguu wa kulia na kusababisha kiganja kukatwa.

Baada ya purukushani hizo, alisema fisi alianza kushambulia kuku na ndipo alipotoka na kwenda kumgongea mjukuu wake aliyemtaja kwa jina la Charles Bushemeli na kumpeleka katika Kituo cha Afya cha Ngaya kwa ajili ya matibabu.

Alisema kutokana na kuwa na majeraha makubwa mwilini, walimpatia huduma ya awali na kumruhusu kwenda katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa ajili ya matibabu zaidi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Chela, Zephrine Samuel, alisema tukio la fisi kuvamia kwenye mkazi wa wananchi si la kwanza kwa kuwa wamekuwa wakivamia nyakati za usiku na kushambulia mifugo kama vile ng'ombe, mbuzi na punda.

Pia alisema kijiji cha Chela kimezungukwa na milima yenye mapango ambayo ndiko fisi hao wanakojificha na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari na kutoa taarifa kwa maliasili pindi watakapowaona fisi hao.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Kahama, Dk. George Masasi, alithibitisha kupokewa kwa majeruhi huyo na kusema alimpokea majira ya saa moja asubuhi jana akiwa na majeraha sehemu mbalimbali za mwili wake.

Dk. Masasi alisema baada ya kumpokea, walimchoma sindano ya kuzuia kichaa kinachotakana na kung'atwa na fisi na kuongeza kuwa kutokana na mkono wa kushoto kushambuliwa vibaya, wamelazimika kumkata kiganja.

Distributed via ippmedia


**BANI INVESTMENT LIMITED**
**DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS**

**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KWA WADAIWA WA NBC BANK MAKAO MAKUU DAR ES SALAAM**

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA NBC MAKAO MAKUU** tunatoa notisi ya siku 14 na tangazo la mnada wa hadhara wa mali zilizoorodheshwa hapo chini ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo. Hivyo basi utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili,Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada.Mnada utafanyika mahali zilipo mali hizi, siku na saa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

| JINA LA AKAUNTI | MMILIKI | MALI ZILIZOWEKWA DHAMANA | MAHALI | TAREHE | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| Zamaka Gen Supplies | Ernest Iganyega | Nyumba yenye CT No.11249, L.O. No.354298, Plot no.66 Block "25" | Ilala Municipality | 4.12.2019 | 4:00 asubuhi |
| Joseph Kilimbe | Joseph Issaya Kilimbe | Nyumba yenye CT No.15995-DLR, L.O. No.96253/10416, Plot No.10, Block 'M' | Chang'ombe-Dodoma | 4.12.2019 | 4:00 asubuhi |
| Isack E. Mwalongo | Goodlike Isaack Mwalongo | Nyumba yenye CT No.9538-MBYLR L.O.No. 143000 Plot No 109 Block 'Y' | Mfaranyaki - Songea | 4.12.2019 | 4:00 asubuhi |
| Brown J. Simsokwe | Brown John Simsokwe | Nyumba yenye CT No.9694-MBYLR L.O. No.176177, Plot No.185 Block "X" | Mfaranyaki-Songea | 4.12.2019 | 6:00 mchana |
| Victor L Mgani | Victor Ludandila Mgani | Nyumba yenye CT No.10295-MBYLR, L.O. No.149010,Plot No.61 Block "L" | Njombe urban area | 7.12.2019 | 4:00 asubuhi |
| Twahiru H Semtindi | Shauri Athumani Semtindi | Nyumba yenye C.T.No.23363-LR MOSHI, L.O. No. 171445, Plot .No. 1116 | Lukozi area Moshi | 7.12.2019 | 4:00 asubuhi |
| Zedeck Joseph | Zedeki Joseph Mgaya | Nyumba yenye CT No.10179-MBYLR, L.O. No.185601, Plot No.134, Block 'F' | Makambako urban | 10.12.2019 | 3:30 asubuhi |
| Justin S Kapanga | Justine Kapanga | Nyumba yenye CT No 11979 MBYLR Plot No 135 Block F | Makambako area | 10.12.2019 | 6:00 mchana |
| Oscar L Mwinuka | Oscar Lwemeko Mwinuka | Nyumba yenye CT No.9658-MBYLR, L.O No.185530, Plot No.39, Block 'K' | Makambako urban area | 10.12.2019 | 8:00 mchana |
| Dgs Agency Ltd | Christopher Adam Ritte | Nyumba yenye CT No.5737-MBYLR, L.O. No.155252, Plot No.486b Block "M" | Forest area ,Mbeya municipality | 14.12.2019 | 4:00 asubuhi |
| Aloyce W Lupondo | Aloyce Lupondo | Nyumba yenye CT No 8107MBYLR Plot No 252 Block EE land office No 174015 | Kalumbulu area, Kyela | 17.12.2019 | 4:00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa "kama zilivyo" as is where is basis"
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:

Kwa maelezo zaidi wasiliana Na ofisi ya BANI INVESTMENT LTD
Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340
Dar es Salaam au kwa simu na. 0713 224578, 0713, 295747, 0653 640999.

# Wakili akwamisha kesi vigogo Simba

**Na Hellen Mwango**

KESI inayomkabili Rais wa zamani wa Klabu ya Simba, Evans Aveva na wenzake akiwamo Makamu wake, Godfrey Nyange, maarufu kama Kaburu, imeshindwa kuanza kusikiliza ushahidi wa utetezi kwa madai kuwa Wakili wa Serikali anayeendesha kesi hiyo amepata udhuru wa kikazi.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa ushahidi wa utetezi lakini akadai kuwa wakili anayeendesha kesi hiyo amepata udhuru, hivyo aliomba tarehe nyingine ya kusikilizwa.

Kutokana na maombi hayo, Hakimu Simba alisema kesi hiyo itasikilizwa ushahidi wa utetezi Desemba 5, mwaka huu.

Mapema, mahakama hiyo iliwaona washtakiwa hao hawana kesi ya kujibu dhidi ya makosa ya kutakatisha fedha.

Aidha, washitakiwa hao waliachiwa kwa dhamani baada ya kufutiwa mashtaka mawili ya kutakatisha fedha Dola za Marekani 300,000 kutokana na upande wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha.

Katika kesi ya msingi, shtaka la kwanza, Aveva na Kaburu wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya madaraka.

Katika shtaka la pili, wanadaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha Dola za Kimarekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko benki ya CRDB Azikiwe kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva iliyoko benki ya Barclays.

Katika shtaka la tatu, Aveva na Kaburu wanadaiwa kwa pamoja kughushi nyaraka iliyokuwa ikionyesha Simba inalipa mkopo wa Dola 300,000 kwa Aveva kitu ambacho si kweli.

Aidha, Katika shtaka la nne, Aveva anadaiwa katika benki ya CRDB kutoa nyaraka ya uongo ikionesha Simba wanalipa mkopo wa kiasi hicho cha fedha.

Aveva anadaiwa kuwa katika Benki ya Baclays Mikocheni alijipatia Dola 187,817 wakati akijua zimetokana na kughushi.

Katika shtaka la sita, Kaburu anadaiwa kumsaidia Aveva kujipatia Dola 187,817 kutoka kwenye akaunti ya Simba wakiwa wanajua fedha hizo zimetokana na zao la kughushi.

Aveva, Kaburu na Zacharia Hans Poppe wanadaiwa kughushi hati ya malipo ya kibiashara wakionesha kwamba nyasi bandia zilizonunuliwa na Simba zina thamani ya Dola 40,577 huku wakijua kwamba si kweli

Katika shtaka la nane, Aveva anadaiwa kuwasilisha hati ya malipo ya kibiashara ya uongo kwa Levison Kasulwa kwa madhumuni ya kuonesha kwamba Simba wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola 40,577

Shtaka la tisa, Aveva, Kaburu na Hanspope wanadaiwa kuwasilisha nyaraka za uongo kuonesha kuwa Simba imenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola 40,577.

Distributed via ippmedia



Vijana wakiishusha mihogo kwenye gari ili wajipatie ujira wa siku katika soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**






# Waziri asikitishwa kasi makusanyo kodi ya ardhi

**Na Munir Shemweta, GAIRO**

KASI ndogo ya ukusanyaji mapato ya kodi ya pango la ardhi katika wilaya ya Gairo mkoani Morogoro, imemsononesha Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula na kuagiza halmashauri hiyo kuongeza kasi ili kufikia lengo.

Akiwa katika ziara yake ya siku moja wilayani hapa juzi, Dk. Mabula alielezwa na Ofisa Ardhi wa Halmashauri hiyo, Nicolaus Matsuva, kuwa halmashauri hiyo katika kipindi cha mwaka 2018/19 ilikusanya Sh. milioni 12.3 na mwaka huu kufikia Novemba, imekusanya Sh. milioni 10 wakati lengo ni Sh. Milioni 55.

Kutokana na taarifa hiyo, Mabula alisema kiwango hicho ni kidogo na hakijafikia hata nusu ya makadirio, hivyo kuitaka halmashauri hiyo kupitia idara ya ardhi, kuongeza kasi ya makusanyo ya maduhuli.

"Msipokusanya kodi ya ardhi mjue mnamkwamisha Rais kutekeza miradi mikubwa kama vile mradi wa kufufua umeme wa Mwalimu Nyerere maarufu kama Stieglers Gorge, hivyo ni lazima tuongeze kasi ya makusanyao," alisema.

Dk. Mabula pia aliitaka halmashauri kuhakikisha kufikia Desemba, mwaka huu, inarejesha Sh. milioni 31 ilizopatiwa kama mkopo kwa ajili ya upimaji viwanja.

Hatua hiyo ilitokana na Mabula kuhoji kuhusiana na marejesho ya fedha za mkopo huo na kuelezwa na ofisa ardhi kuwa halmashauri hajarejesha kiasi chochote cha fedha za mkopo iliopatiwa kwa ajili ya upimaji viwanja na kuomba kuongezewa muda hadi Machi, mwakani.

"Toka Juni hadi leo (juzi) hamjarejesha wakati ulitakiwa kurejeshwa ndani ya miezi mitatu. Mkopo huu unazunguka kwa nini hamjarejesha hadi leo? Kazi mliyopewa hamjamaliza, naagiza hadi Desemba fedha hiyo iwe imerejeshwa," alisema Dk. Mabula.

Pia alishangazwa na idara ya ardhi katika halmashauri ya Gairo kuingiza viwanja 155 kati ya 1,198 kwenye mfumo wa makusanyo ya kodi ya ardhi kwa njia ya kielektroniki jambo alilolieleza linaikosesha serikali mapato yatokanayo na kodi ya pango la ardhi sambamba na kushindwa kutoa ilani kwa wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi ingawa ilani hizo ziliandaliwa tangu mwezi Machi 2019.

Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Sirieli Mchembe, alisema wilaya yake inakabiliwa na changamoto ya ujenzi holela na kubainisha kuwa hata urasimishaji katika wilaya hiyo ni tatizo ikiwamo sebule za baadhi ya nyumba kuelekezwa kwenye vyoo vya nyumba nyingine.

Hata hivyo, alimwahidi Naibu Waziri kuwa ofisi yake itayafanyia kazi maagizo yote aliyoyatoa ikiwamo uandaaji wa mpango kabambe katika wilaya hiyo kupangika kimji sambamba na kuwa na mji wa serikali utakaojumuisha taasisi zote za serikali zilizoko katika wilaya hiyo.

# Watalii mil. 1.5 watembelea Tanzania kwa mwaka

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Profesa Adolf Mkenda, amesema juhudi za serikali za kukuza utalii nchini zimezaa matunda kutokana na ongezeko la watalii wanaoingia nchini kupanda hadi kufikia milioni 1.5 kwa mwaka. Prof. Mkenda aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake, jijini Dodoma.

Alisema, idadi hiyo ya watalii haijawahi kufikiwa nchini. “Mwaka 2018 idadi ya watalii waliokuwa wakitembelea Tanzania ilikua kwa wastani wa asilimia 13 kwa mwaka ikiwa ni mara mbili ya wastani wa ukuaji wa idadi ya watalii wanaotembelea nchi za kigeni duniani. Katibu Mkuu huyo alisema takwimu zinaonyesha kwamba mwaka 2018 idadi ya watalii duniani iliongezeka kwa wastani wa asilimia sita pekee ikilinganishwa na asilimia 13 kwa Tanzania.

Alipotakiwa kueleza kama ongezeko hilo la watalii lina mchango kiasi gani katika nchi alisema utalii unachangia jumla dola za Kimarekani bilioni 2.4 sawa na robo ya fedha zote za kigeni zinazopatikana nchini.

Prof. Mkenda alisema, “Takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania inaongoza kwa kupata fedha nyingi za kigeni katika utalii. Pamoja na kwamba Kenya ilipata watalii zaidi milioni mbili mwaka 2018, idadi hii iliingizia Kenya Dola za Kimarekani bilioni 1.6 tu.”

Hata hivyo, alisema, Tanzania imeendelea kufanya vizuri Afrika ambapo takwimu zinaonyesha kwamba hadi sasa inashika nafasi ya nne barani Afrika kwa kuingiza fedha za kigeni nyingi kutokana na utalii. Katibu Mkuu huyo alifafanua kuwa mafanikio hayo yametokana na juhudi kubwa za serikali za kutangaza utalii na kuimarisha miundombinu katika maeneo ya utalii. Kwa upande mwingine alisema kuwa sekta binafsi pia imechangia kutokana na uzalendo wao wa kushirikiana na serikali kuutangaza utalii kwa kuwekeza katika hoteli na vyombo vya usafiri.

Hata hivyo, Prof. Mkenda alisema, pamoja na mafanikio mazuri yaliyopatikana, serikali inaweza kufanya vizuri zaidi. “Ilani ya CCM inataka idadi ya watalii wanaokuja Tanzania kwa mwaka ifikie milioni mbili ifikapo mwaka 2020. Kwa mwenendo uliopo, lengo la Ilani ya Chama Cha Mapinduzi litafikiwa,” alisema na kuongeza, “Hata hivyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli aliagiza juhudi zifanywe ili mchango wa utalii katika uchumi wa nchi uongezeke maradufu. Kwa hiyo bado juhudi zaidi zinahitajika,” alisema.

Alipoulizwa ni mbinu zizotatumika kuhakikisha wizara inatekeleza agizo la Rais Magufuli la kuongeza mchango wa uchumi katika alisema, “Ili tuweze kuongeza zaidi idadi ya watalii wa kigeni ni lazima tufanye mambo manne. Kwanza, ni lazima tuhakikishe utalii unaenea maeneo yote nchini. Sasa hivi utalii umejikita zaidi upande wa Kaskazini Mashariki mwa nchi yetu.”

Pili, ni lazima tuongeze vivutio vya utalii, ili tuwe na watalii wanaokuja kuvinjari kwenye fukwe, kutembelea malikale, kutazama tamaduni, kuja kwaajili ya michezo, mikutano na kadhalika. Sasa hivi takribani asilimia 80 ya watalii wanaoingia nchini kwa mapumziko huelekea kwenye mbuga za wanyama. Tatu ni lazima kuimarisha huduma mbalimbali kwa ajili ya utalii. Na nne ni kuendelea kutangaza utalii wa Tanzania duniani, kwenye masoko yaliyozoeleka na mapya kama Urusi na China.

Alisemna serikali ya awamu ya tano imedhamiria kuimarisha zaidi utalii nchini ili unufaishe wananchi wote na uongeze mapato ya serikali na kukuza uchumi.

Distributed via ippmedia



Mwandishi wa habari, Erick Kabendera (kulia), akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusikiliza kesi inayomkabili ya uhujumu uchumi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kesi ya Kabendera kupigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana imepiga kalenda kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili mwandishi wa habari za uchunhuzi, Erick Kabendera, baada ya upande wa Jamhuri kudai kuwa upelelezi wake bado haujakamiliwa.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upepelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na upande wa Jamhuri unaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Wakili wa utetezi, Jebra Kambole, aliieleza mahakama kuhusu maombi aliyowasilisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) kuwa bado wako katika mazungumzo na hawajafika muafaka, na kwamba yakikamilika watawataarifu mahakama.

Akijibu hoja ya utetezi, Wankyo alikiri kuwapo kwa maombi hayo yaliyowasilishwa na upande utetezi ambayo wanayafanyia kazi na yatakapokamilika watawataarifu.

Hakimu Mtega aliahirisha kesi hiyo mpaka Desemba 4, mwaka huu, itakapotajwa tena.

Kabendera anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi yenye mashtaka matatu likiwamo la utakatishaji wa Sh. milioni 173.

Katika mashtaka ya kwanza ilidaiwa kuwa katika kipindi hicho, Kabendera alijihusisha na mtandao wa kihalifu kwa kutoa msaada kwa genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Inadaiwa kuwa katika kipindi hicho, bila ya sababu, alikwepa kodi ya Sh. 173,247,047.02 ambayo ilitakiwa ilipwe Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Pia inadaiwa Kabendera alitakatisha Sh. 173,247047.02 huku akijua fedha hizo ni mazalia ya kosa la kujihusisha na genge la uhalifu na ukwepaji kodi.

# Ndugai aiahidi THBUB ushirikiano

**Na Mbaraka Kambona**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameihakikishia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) kuwa itaipatia kila aina ya ushirikiano itakayohitaji kutoka kwa taasisi ya Bunge.

Ndugai alieleza hayo alipokutana na Mwenyekiti wa Tume, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, aliyemtembelea katika ofisi yake ya jimbo iliyopo wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

Ndugai alimueleza Mwenyekiti kuwa tume ni taasisi muhimu katika kusimamia na kuhamasisha masuala ya haki za binadamu nchini.

“Tume ni taasisi muhimu ambayo imepewa dhamana ya kusimamia haki za binadamu nchini, nawapongeza kwa kazi nzuri mnazozifanya japo mna changamoto nyingi katika kutekeleza kazi zenu,” alisema Ndugai.

Ndugai aliendelea kueleza kuwa anatambua eneo ambalo tume inalifanyia kazi ni gumu kwa kuwa linahusiana na masuala ya usimamizi wa haki za watu, na kuwataka changamoto hizo zisiwakatishe tamaa pale watakapokuwa na jambo lolote wasisite kuwasiliana na ofisi ya Bunge ili kushirikiana kuzitatua.

“Najua katika utekelezaji wa majukumu yenu mtakutana na changamoto nyingi hususani migogoro ya ardhi, migogoro ya wakulima na wafugaji, naamini mtaisaidia serikali katika kuipunguza kama sio kuimaliza kabisa,”aliongeza Ndugai.

“Naamini mtaenda kushughulikia pia migogoro ya wafugaji wanaokaa karibu na maeneo ya hifadhi, haiwezekani na haiingii akilini mifugo ikiingia katika hifadhi adhabu yake ni kunyang’anya mifugo yote ya mwananchi, nadhani hii sio sawa wala sio haki, nendeni mkayashughulikie haya,” alisisitiza.

Aidha, Ndugai alimueleza Mwenyekiti wa tume kuwa wasisite kupeleka mapendekezo yoyote pale watakapoona kuna sheria ambazo wataona ni kandamizi waziwasilishe na kushirikiana na Bunge katika kuzirekebisha.

Naye Jaji Mwaimu alimueleza Spika Ndugai kuwa dhamana waliyopewa ni kubwa, hivyo wanaahidi kuitendea haki kwa kufanya kazi kwa bidii ili kusaidia kutimiza ndoto ya nchi ya kufikia uchumi wa kati.

“Sisi kama viongozi wa tume, tunaunga mkono jitihada za serikali katika kukomboa wananchi kiuchumi, tunachokiomba kutoka kwenu na wadau ni ushirikiano kwani tukishirikiana kwa pamoja tutaweza kufanikisha jitihada hizo” alisema Jaji Mwaimu.


KUMBUKUMBU



ROSE SIMON IVAMBI

LEO TAREHE 21/11/2019 UMETIMIZA MIAKA 10 TANGU UITWE NA MWENYEZI MUNGU. INGAWA HAUPO NASI KIMWILI LAKINI KIROHO TUPO PAMOJA DAIMA. BADO TUNAKUMBUKA UPENDO, BUSARA, HEKIMA NA MCHANGO WAKO MKUBWA WA USHAURI KATIKA FAMILIA NA JAMII KWA UJUMLA.

PENGO ULILOLIACHA MAMA YETU MPENDWA KAMWE HAKUNA WA KUZIBA.

UNAKUMBUKWA SANA NA WANAO: VERONICA, SEBASTIAN, OLIVA, JANETH NA FRIDA. WAJUKUU ZAKO: HANS, LOUISE, MARTHIN, AGATHA, SIMON SENIOR, BENARD, MARCELLA, SIMON JUNIOR, STEVE, NANCY JUNIOR, NANCY SENIOR NA DIANA. DADA NA KAKA ZAKO, WAKWE ZAKO, WIFI ZAKO, SHEMEJI ZAKO, PAMOJA NA WANAFAMILIA WOTE NA WAUMINI WENZAKO.

DAIMA TUNAOMBA MAMA UPUMZIKE KWA AMANI.
“BWANA ALITOA NA BWANA AMETWAA JINA LA BWANA LIHIMIDIWE”.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Unahitajika utafiti wa kina kupaa bei mahindi

**SERIKALI** imekiri kupaa kwa bei ya mahindi kufikia Sh. 107,000 kwa gunia, huku ikiwataka watafiti kufanyia kazi suala hilo na kutoa mapendekezo ili kukabiliana na hali hiyo.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Siza Tumbo, alisema hayo juzi alipokuwa akifungua kikao cha uwasilishaji wa taarifa mbili za utafiti kuhusu kuimarisha usalama wa chakula na biashara ya mazao ndani na nje ya nchi uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa masuala ya Kiuchumi na Kijamii (ESRF) kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Afrika (AGRA) na Wizara ya Kilimo.

Alisema utafiti huo ulitokana na kilio kilichokuwapo mwaka jana cha kuzuia uuzaji wa mazao ya chakula hususan mahindi nje ya nchi na kwamba mahindi yanatumika zaidi kwenye nchi za Afrika Mashariki.

Aliwataka kuangalia sababu za bei ya mahindi kupanda sana, kutokana na wakazi wa mijini kuanza kuzungumzia hali hiyo ya kupaa hadi kufikia Sh. 107,000 kwa mujibu wa takwimu rasmi sasa kulinganisha na mwaka jana bei ilipokuwa Sh. 65,000.

Prof. Tumbo alisema kupanda kwa bei hiyo hakutokani na kukosekana kwa chakula, na kusisitiza kuwa chakula kipo.

Alisema anaamini watatoa ushauri mahsusi kwa Wizara ya Kilimo na kuwahakikishia kuwa wizara itaamua namna gani ya kwenda mbele, huku akisema serikali haiwezi kukwepa mahindi kwa kuwa ni zao linalopendwa sana na ni moja ya viashiria vya usalama wa chakula.

Bei ya mahindi imekuwa ikipaa mara kwa mara bila kuwapo sababu za kupaa kwake, hali ambayo imekuwa ikisababisha kupanda kwa kasi kwa bei ya unga kama inavyoshuhudiwa sasa katika maeneo mbalimbali nchini. Jijini Dar es Salaam kwa sasa kilo moja inauzwa kwa zaidi ya Sh. 1,500.

Bei hiyo inaweza kuendelea kupaa na kuwaathiri zaidi watu wengi wenye kipato kidogo ambao ni watumiaji wakubwa wa unga.

Jambo hili linapaswa kufanyiwa ufuatiliaji wa karibu na endelevu ili kuepukana na uwezekano wa nchi kukosa usalama na uhakika wa chakula.

Hii inapaswa kuwa changamoto kwa wataalamu na watafiti wetu; kwa maana ya kutakiwa kuendelea kutafuta sababu na kuja na majawabu ya kudumu kumaliza kabisa changamoto hiyo.

Kitu ambacho sisi Nipashe tunakiona kuwa kinaweza kuwa kisababishi cha kupaa kwa bei ya mahindi kila wakati ni serikali kutuhusu usafirishaji wa zao hilo nje, lakini bila umakini katika udhibiti.

Serikali kwa kuruhusu wakulima kuuza mazao ya chakula nje hususan mahindi ilikuwa na nia njema, baada ya kilio cha muda mrefu cha kutaka kujipatia kipato kutokana na mazao ya chakula huhitajika sana nje. Kwa mfamo, nchi nyingi jirani kama Kenya, DRC, Zambua na Malawi zinanunua kwa wingi mahindi kutoka Tanzania.

Kilichotakiwa kufanyika ni kuwaruhusu, lakini kuhakikisha kuwa wanabakia na ziada ya kutosha ili kuondoa uwezekano wa nchi kukumbwa na uhaba.

Ni kweli kuwa mipaka ya chakula kuuzwa nje imefunguliwa, lakini tunaishauri serikali isiache biashara hii kufanyika kienyeji na baadaye kusababisha athari.

Sisi kama taifa, tunaheshimu na kuzingatia mazingira ya soko huria, lakini pale inapoonekana kuwa mambo yanaharibika, serikali haina budi kuchukua hatua ikiwamo kuingilia kati kwa muda kuyaweka sawa.

Pamoja na hayo, msisitizo wetu ni kwamba wataalamu na watafiti waendelee kufanya ufuatiliaji ili tatizo hili lipatiwe ufumbuzi wa kudumu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ndugu zangu wauza mafuta Mwanza, mteja ni mfalme

**'MTEJA** ni mfalme' ni usemi unaobeba nafasi fulani yenye ukweli katika jamii. Ni kauli inayotumika sana katika masuala ya uhusiano kibiashara, hasa kati ya mnunuzi na muuzaji.

Kimazingira, mteja ana nafasi kubwa ya kusikilizwa, pia kuhudumiwa kwa mengi, ajione ana haki kubwa mahali hapo.

Pamoja na kufika katika biashara zao, kunatakiwa mteja aheshimiwe katika nafasi muhimu, kuzingatia uamuzi wa kuja kupata huduma mahali hapo.

Kunaelezwa, iwapo mtu hataona umuhimu wa wateja katika biashara zako, basi wajue wako mbioni kuporomoka kibiashara.

Inaelezwa, nafasi ya kushuka biashara mara nyingi inaanzia katika kukosekana kauli au matendo mazuri kutoka upande wa muuzaji, kwenda kwa mnunuzi.

Mhusika wa mauzo anapotakiwa kuboresha biashara na mapokezi ya ombi hilo kutoka kwa muuzaji ikawa ubabaishaji, kunachangia wateja kukimbia.

Nirejee tena, neno 'mteja ni mfalme' lina maana kubwa kwa matendo na utawala wa kifikra, katika kujenga uhusiano wa pande hizo mbili husika na jamii kwa jumla.

Kuwapo biashara, iwe kubwa au hata ndogo, wamiliki wanatakiwa kuwa na watumishi waliosomea au kunadaliwa, kuhusu dhana nzima ya mapokezi bora, kwa ajili ya kuwakaribisha wateja wao, ikiwamo na kumuelewesha mteja wake. Ina maana kubwa sana.

Pia, mfanyakazi asipokuwa na lugha nzuri kwa wateja, ajue anaweza kuisababishia hasara sehemu anayofanya kazi, akiponzwa na kauli zake.

Jiulize nini mvuto hata mteja akapiga hatua hadu penye biashara,akachukua pesa zake na kufanya ununuzi, Iko wazi kuna sababu inayoambatana na msukumo.

Kwanini namtaka hayo? Nimejaribu kueleza kidogo umuhimu huo, kutokana na ushuhuda wetu katika jamii; uhusiano wa muuzaji bidhaa na huduma, pia mnunuzi wake.

Mwanzo ni kwamba, wafanyabiashara wanaingia gharama kubwa katika kutangaza bidhaa zao, ili zitambulike kwa jamii wanakopatikana wateja.

Hilo hufanyika, huku katika baadhi ya biashara zinaumizwa na sehemu ya watendaji wake wasio na lugha nzuri kwa jamii kwa jumla. Hatima ni hasara, baadhi ya biashara zinatumbukia shimoni kwa bidhaa 'kudoda'

Katika hilo hapo nina ushuhuda hasa ulionifanya kuwasilisha hoja hii. Nakumbuka siku ya wiki moja iliyopita mwaka huu majira ya jioni, katika kituo kimojawapo cha mafuta, jirani na hospitali kubwa ya jijini Mwanza, nilishuhudia vijana wawili wanaotoa huduma ya biashara hiyo.

Cha kushangaza ni pale nilipowaona vijana hao wauza mafuta,walitoa kauli isiyofanana na ufanisi wa biashara.

Mteja alipofika, akitaka kuwekewa mafuta na ana pesa kubwa inayohitaji chenji, alikatizwa katika lugha fupi 'haiwezekani' na akatakiwa aende mjini ndiko kwenye chenji.

Hilo halikuwa kwa mteja mmoja, bali wengi. Ilinisikitisha sana, kwani nilishuhudia malalamiko mengi kutoka kwa wateja hata nao walishangaa hayo.

Mimi nikiwa mmoja wao, kinachoshangaza ni kituo hicho cha mafuta kinashindwa kutafuta mbadala wa kukabili hali hiyo, kwa mategemeo benki inashindwa kuchukua pesa benki zitakazowasaidia kurudisha chenji na wateja wao kunufaika kibiashara kwa ufasaha.

Vivyo hivyo, inapendeza dhana ya huduma kwa wateja kutawala, ili kuwapo kauli bora na yenye busara zaidi.

Mnapowaambia wateja waende mjini kuchukuwa mafuta, je, mnategemea kwa lugha hiyo, kesho wataendelea kushiriki biashara zenu?

Kwa mara mwisho niwatamkie tena tamathali 'Mteja ni Mfalme' ndugu zangu wa vituo vya mafuta.

# Kampeni 'Linda ardhi ya Mwanamke' kuzinduliwa

**Na Beatrice Moses**

OMBWE lililopo katika utekelezaji wa sheria za ardhi nchini, linatarajiwa kupunguzwa kupitia kampeni ya kimataifa ya 'Linda ardhi ya Mwanamke' inayozinduliwa leo jijini Dar es Salaam.

Tanzania imechaguliwa kuwa nchi ya mfano katika kampeni hiyo, ikitajwa kuwa na sheria nzuri za ardhi ambazo pamoja na mambo mengine inatoa fursa sawa katika umiliki wa ardhi wa jinsia zote mbili.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mwenyekiti wa kampeni hiyo, Tike Mwambipile, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (Tawla), alisema itazinduliwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ummy Mwalimu.

Alisema licha ya kuwapo kwa sheria za ardhi kumekuwa na uzito katika kuzitumia, wakati wanawake wengi wanazidi kuteseka kiuchumi na kijamii kwa kunyimwa haki hiyo kutokana na sababu za kimila na kitamaduni.

"Tanzania ni nchi ya kwanza iliyochaguliwa kuendesha kampeni hii kwa kuwa ina sheria nzuri za ardhi, kimataifa itawezesha na Shirika la Landesa Ulimwenguni, Habitat for Humanity, Huairou Commision na Benki ya Dunia," alisema Mwenyekiti huyo.

Alibainisha kuwa asasi za kiraia nchini zitafanya uraghibishi wa kina unaolenga kuleta mabadiliko ya umiliki wa ardhi baina ya wanawake na wanaume.

Pia, kampeni hiyo inatekelezwa na asasi za kiraia 26 zinazojihusisha na masuala ya ardhi, inaratibiwa na Landesa Tanzania zinazozuia wanawake kumiliki ardhi. Alisema lengo la kampeni ni kufungua ombwe lililopo kati ya sera au sheria na taratibu za maisha ya kila siku ya jamii ya Watanzania ikiwamo kubadili fikra za wanajamii kutoka katika mila kandamizi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Rose Reuben, alisema vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika kuondoa ombwe hilo kwa kuripoti habari zinazoelimisha umuhimu wa kumiliki ardhi kwa usawa badala ya kuwatenga wanawake.

Dk. Monika Mhoja, Mkurugenzi Mkazi wa Landesa, alisema mila potofu zimesababisha wanawake wengi kutojiamini katika kumiliki mali ikiwamo ardhi, hali inayosababisha wengi wao kuwa na maisha duni.



Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB Tanzania, Sabasaba Moshingi (katikati), akishirikiana kukata keki na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Fei Girls, Jackline Mgina (kushoto) na Mary Kyando, wakati wa mahafali ya kwanza ya kidato cha nne ya shule hiyo katika Halmashauri ya Madaba, Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma, juzi. Kulia ni mmiliki na meneja wa shule hiyo, Omari Msigwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Italia kuipa Tanzania bil. 5/- za tabianchi

Distributed via ippmedia

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya Sh. bilioni tano zinatarajiwa kutolewa na Serikali ya Italia kwa Tanzania ili kushughulikia changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene kwa wanahabari, na kuwa hatua hiyo inafuatia mazungumzo ya awali na Balozi wa Italia nchini, Roberto Mengoni.

"Kukamilika kwa mazungumzo haya ambayo kwa sasa yapo katika hatua za awali, kutasaidia sana katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo tayari matokeo yake yameshaanza kuonekana sehemu nyingi duniani," alisema Simbachawene.

Simbachawene amesema mazungumzo yatakapokamilika watahakikisha pesa yote inaenda kuwekezwa katika miradi itakayokuwa imepangwa.

"Mazungumzo yatakapokamilika tutakuwa tumepata zaidi ya Sh. bilioni tano, ambazo tutazielekeza katika kushughulikia mazingira hali ambayo itachochea kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi,"alisema.

Aliyataja baadhi ya maeneo ambayo yatanufaika na msaada wa fedha hizo ni ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa zinazohusiana na mabadiliko ya tabia nchi, kuendeleza vyanzo vya nishati mbadala na kukuza ufanisi wa nishati pamoja na maendeleo ya mipango ya upatikanaji wa umeme wa bei nafuu.

Balozi Mengoni alisema kufikiwa kwa makubaliano baina ya pande hizo mbili kutaimarisha na kuratibu jitihada za kupambana na mabadiliko ya tabia nchi duniani na kupunguza athari mbaya.

"Makubaliano haya ni mwendelezo wa ushikirikiano mzuri kati ya Tanzania na Italy ambapo kukamilika kwake kutasaidia katika kupunguza athari za mabadiliko ya tabia ya nchi duniani," alisema Balozi Mengoni.

Balozi Mengoni aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa juhudi zake inazochukua katika kukabiliana na utunzaji wa mazingira ikiwamo ya upigaji marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki.

# CCM kufanya kongamano Dar es Salaam

**Na Romana Mallya**

UMOJA wa Wazazi Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), umeandaa kongamano ambalo litajumuisha viongozi mbalimbali ambapo miongoni mwa mada zitakazotolewa ni pamoja na mikakati ya uchaguzi na maadili ya Taifa.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Dk. Edmund Mndolwa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari na kuwa mgeni rasmi atakuwa Mwenyekiti wa CCM, Rais, John Magufuli.

Dk. Mndolwa alisema kongamano hilo linatarajia kufanyika Novemba 29 jijini Dar es Salaam na litahudhuriwa na watu 1,500 kutoka mikoa 32 kwenye wilaya 168.

"Kongamano hili ni sawa na Mkutano Mkuu Maalum wa Taifa ambalo ajenda kubwa ni kumpongeza Rais John Magufuli kwa utekeleza wa Ilani ya CCM na kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)," alisema.

Dk. Mndolwa alitaja mada ambazo zitatolewa siku hiyo kuwa ni mikakati ya uchaguzi itakayowasilishwa na Makamu Mwenyekiti CCM Taifa, Philip Mangula.

"Mkurugenzi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogoda atawasilisha mada ya maendeleo ya sekta hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, atazungumzia kuhusu maadili ya Taifa na Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Dk. Alan Kijazi atazungumzia ulinzi wa maliasili na faida za utalii wa ndani," alisema.

Alisema Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano (TTCL), Waziri Kandamba, atazungumzia sekta ya mawasiliano na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Umeme Tanesco, Tito Mwinuka ataongelea maendeleo ya nishati ya umeme," alisema.

Dk. Mndolwa alisema wamechapisha jarida la pongezi kwa serikali kwa utekelezaji wa Ilani ambalo siku hiyo watalizindua.

Alisema watatengeneza majarida zaidi ya 10,000 na yatasambazwa nchini na kwenye balozi za Tanzania zilizopo nchi mbalimbali duniani.

Pia alisema jarida hilo litawekwa kwenye ndege za Tanzania na kuzitaka taasisi zitangaze biashara zao humo.



Wachuuzi wa samaki wakiwa wamekaa chini wakisuburi wateja katika eneo la Ruvu, mkoani Pwani, wikiendi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri ataka taarifa ya mlipuko wa gesi

**Na Mwandishi Wetu,**
MTWARA

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Musa Sima, ametoa wiki moja kwa kituo cha gesi cha Songas kilichopo Somanga wilayani Kilwa kutoa taarifa kamili kuhusiana na chanzo chamlipuko wa gesi uliotokea hivi karibuni.

Akizungumza katika ziara yake ya kutembelea miradi ya kimkakati Kanda ya Kusini katika mikoa ya Lindi na Mtwara kujionea namna shughuli za uhifadhi wa mazingira zinavyotekelezwa,

Sima alisema milipuko ya gesi husababisha moto ambao ni chanzo cha uharibifu wa mazingira kama kuteketeza uoto wa asili na kuhatarisha maisha ya binadamu.

"Natoa wiki moja kwa wamiliki wa mradi wa gesi kuhakikisha tunapata taarifa kuhusu chanzo cha mlipuko huu na hatua zilizochukuliwa," alisema na kuendelea:

"Baada ya wiki moja tutarudi ili tuone mikakati ipi tutumie ili kuwashirikisha wenzetu wa wizara nyingine wanaohusika katika eneo hili katika kutoa elimu kwa wananchi kutoka maeneo mbalimbali."

Waziri Sima alisema ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ( NEMC),

wameona wafike ili kujua kiundani chanzo cha mlipuko huo, ushiriki na ushirikishwaji wa wananchi kwa maana ya kutoa elimu juu ya

madhara yatokanayo na gesi na namna ya kujikinga ikiwa bomba hilo limepita takribani vijiji 64 mpaka kufika Dar es Salaam.

"Bomba hili limepita kwenye vijiji takribani 64, hivyo ni wajibu wetu kama serikali kwa kushirikiana na taasisi sizizo za kiserikali kuhakikisha elimu inawafikia wananchi juu ya madhara na faida zitokanazo na mradi huu." aisema Sima.

Aliongeza kama wananchi watapewa elimu ya kutosha kuhusiana na namna bora ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira, itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza athari zitokanazo na shughuli za binadamu na tija katika uzalishaji wa vitu mbalimbali.

Mwenyekiti wa Bodi ya MENC, Prof. Esnati Chaggu, alisema udhibiti madhubuti usipofanyika katika kutunza na kuhifadhi mazingira, athari yake itakuwa ni kubwa kuanzia kwenye mazingira yenyewe mpaka kwa wananchi, hivyo ni jukumu la Watanzania wote kuhakikisha wanatunza na kuhifadhi mazingira yanayowazunguka.

Aliongeza kuwa vifaa vinavyotumika kwenye marekebisho viwe kwenye ubora unaohitajika ili kupunguza matatizo ambayo yangechochea kwa namna moja uharibifu wa mazingira.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliipongeza kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kilwa kwa kuonyesha ush mkubwa kuanzia mwanzo wa tatizo la mlipuko wa gesi mpaka mwisho sambamba na juhudi madhubuti walizochukua kuhakikisha mazingira yanakuwa salama.

Alisema ni muhimu kusajili miradi ili ifanyiwe tathmini ya athari za mazingira kwa kufuata sheria na kanuni za mazingira pasipo kuleta athari katika mazingirakutokana na mradi wake.

# JPM aweka msimamo bei ya mahindi

**INATOKA UK. 2**

yako ya bei ya chini, biashara hii ni lazima iwe huru, mkulima anatafuta mbolea, anahangaika, anafukuzwa na nyoka, matope ni yake, wakati wakuvuna ni yeye, halafu avune umpangie bei.

"Bei inajipanga yenyewe, akikosa wanunuzi kwa sababu mahindi yake yapo juu, atakaa na mahindi yake. Na ninachoweza kuwaeleza, ninyi wakulima chapeni kazi, kwa walio maofisini tumeni watu wakawalimie, wakati wa kutajirika ni sasa," alisema.

**MAAGIZO NIDA**

Rais Magufuli pia alilazimika kumpigia simu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Dk. Arnold Kihaule, na kumtaka kwenda Morogoro jana kutatua tatizo la wananchi kushindwa kusajili laini zao za simu kwa alama za vidole kutokana na kukosa vitambulisho.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Desemba 31, mwaka huu ndio mwisho wa usajili wa laini za simu kwa alama za vidole na hadi Agosti, 2019 laini milioni 5.2 ndio zilikuwa zimesajiliwa kati ya laini milioni 44.2.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo jana eneo la Msamvu, mkoani Morogoro, akiwa ziarani kwenda mkoani Dodoma kwa ziara ya kikazi ya siku tano, baada ya kusimamishwa katika eneo hilo ambao walimweleza adha wanayopata wakati wa kujiandikisha kupata vitambulisho.

Mbali na kumwagiza Dk Kihaule kwenda Morogoro kutatua changamoto hiyo, alisema tatizo linalowakabili wakazi hao huenda likawa linawakumba wananchi wengine katika maeneo mbalimbali nchini.

Baada ya wananchi kumweleza changamoto wanazokumbana nazo, Magufuli alimpigia simu Dk. Kihaulealisema: "Nipo Morogoro hapa nimeelezwa tatizo la Nida, mna ofisi moja tu Mkoa wa Morogoro kwa nini? Mbona watu wa Kilosa wanakuja hapa wanapata shida.

"Sasa nisikilize Mkurugenzi uko wapi, uko Dar? Ondoka sasa hivi uje hapa Morogoro ushughulikie hili tatizo la Nida na ninataka watu walioko wilayani wasije hadi mkoani uje kutatua hili tatizo la Nida."

Aliendelea kumweleza kuwa: "Leo(jana) uje hapa Morogoro ukae na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ujipange ofisi yako izunguke katika wilaya zote ili wananchi wapate vitambulisho haraka."

Kiongozi mkuu huyo wa nchi alisema huenda tatizo linalowakabili wakazi wa Morogoro lipo katika maeneo mengine, kumtaka mkurugenzi huyo kufuatilia mikoa yote.

"Inawezekana matatizo yapo Tanzania nzima na si Morogoro pekee. Mzunguke katika wilaya zote ili wananchi wapate huduma haraka," alisema Rais Magufuli.

**KUMTUMBUA KEBWE**

Rais Magufuli alitaja sababu ya kutengua uteuzi wa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Steven Kebwe, ni kujihusisha na biashara na kujiingiza kwenye miradi ya halmashauri.

"Nataka niseme wazi, Mkuu wa Mkoa aliyekuwapo, alijisahau na baadhi ya miradi ya halmashauri ilikuwa yake na kuna halmashauri alisambaza mbao za ovyo, ninayajua yote," alisema.

Alimtaka Mkuu wa Mkoa aliyepo ahakikishe anashughulikia kero za wananchi ikiwamo migogoro ya wakulima na wafugaji iliyoshamiri katika mkoa huo.

## Maskini wajitosa ufugaji samaki

**Na Elizabeth Zaya,**
NJOMBE

WANUFAIKA wa mpango wa kunusuru kaya masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) katika kijiji cha Mkeha, Halmashauri ya Wanging'ombe mkoani Njombe, wameanzisha ufugaji wa Samaki.

Mwenyekiti wa Kamati ya usimamizi wa walengwa hao (CMC), Baton Kidzumbe alisema mradi huo uliibuliwa na walengwa wenyewe ambao wako 64 katika kijiji hicho kwa ajili ya chakula na kujiongezea kipato.

Alisema wameanza mradi huo kwa mabwawa manne na kwamba wanatarajia kuongeza kulingana na maendeleo ya mradi. Alisema katika kila bwawa waliweka vifaranga vya samaki 2,000 na kwamba matarajio yao ni kuhakikisha wanazalisha samaki wengi na kuuza kwa wateja wakubwa na wadogo.

"Mradi huu tuliibua wenyewe na tukasaidiwa na Tasaf vifaa vya kuchimbia mabwawa na pesa kwa ajili ya kununulia vifaranga, na mpaka sasa maendeleo ya mradi ni mazuri na tutaanza kufurahia matunda muda si mrefu," alisema Kidzumbe.

Afisa Uvuvi wa Halmashauri hiyo, Abdon Komba, alisema kufikia mwezi ujao watakuwa wameanza kuvuna samaki na kwamba matarajio ni kuvuna mara mbili kwa mwaka kila bwawa kwa kipindi cha miaka mitatu.

Komba alisema kitaalamu wanatarajia kwamba baada ya kuvuna kwa mabwawa yote, kiasi cha pesa kitakachopatikana ni zaizi ya Sh. milioni 20 kila mwaka.

Distributed via ipnmedia

HABARI KITAIFA

# Makandarasi watupa lawama kwa serikali

Na Romana Mallya

BARAZA la Vyama vya Makandarasi (CCA), linapinga vitendo vinavyofanywa na baadhi ya viongozi vya kuwakamata na kuwaweka ndani kijinai makandarasi bila kuzingatia mikataba ya miradi inayotekelezwa.

Kwa mujibu wa tangazo lao lililochapishwa katika gazeti la Nipashe, CCA limesikitishwa na vitendo vya kuingilia utekelezaji wa miradi ya umma na kuwekwa ndani kijinai makandarasi bila kuzingatia mikataba.

"Baraza linasikitishwa na ongezeko la matukio haya na tumesikia katika vyombo vya habari kuhusu uamrishaji wa mabadiliko ya muda wa utekelezaji na mengine bila kuzingatia mikataba iliyoko.

"Utumiaji wa madaraka kutoa maagizo au kuwakamata wakandarasi na kuwaweka ndani kijinai, badala ya kutumia vifungu vya mikataba ya ukandarasi kutatua matatizo yaliyojitokeza."

Pia CCA imeeleza kwenye tangazo hilo kuwa kumekuwa na utumiaji vitisho na kuwadhalilisha makandarasi. "Tunatambua shauku ya viongozi wa umma kuona miradi inatekelezwa kwa ufanisi na kwa muda mfupi iwezekanavyo.

"Tunatambua pia, kwamba kazi za ujenzi haziendeshwi kijinai bali hutekelezwa kwa kuzingatia mikataba ya kisheria ambayo ikivurugwa, huharibu utekelezaji wa miradi hiyo na huharibu mazingira ya kufanya biashara ya ujenzi na sekta ya umma kwa jumla."

Katika tangazo hilo CCA limeiomba serikali na taasisi zake kuwasihi viongozi wa umma kuwatumia wasimamizi wataalam kutekeleza mambo yote yanayohusu miradi kwa kuzingatia mikataba husika.

"Baraza na wakandarasi wote kwa ujumla wataendelea kushirikiana na Serikali kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa ufanisi na kwa muda muafaka na mara zote, kutumia vipengele vya mikataba ya miradi husika kushughulikia migogoro yake," ilieleza.



Wafanyabiashara wakiwa wamepanga bidhaa zao chini, kwenye mazingira yasiyo salama kwa afya za walaji, katika Soko la Buguruni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mradi umwagiliaji kunufaisha Kiteto

**Na Mwandishi Wetu,** KITETO

ZAIDI ya wakulima 1,000 wa Kata ya Matui, Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, wanatarajiwa kunufaika na mradi wa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia visima vinavyojengwa kwa lengo la kuongeza tija kwenye mazao ya mahindi na alizeti.

Mradi huo unaotekelezwa na kampuni ya wazawa inayojishughulika na kuhamasisha kujenga afya na kutokomeza umasikini (JATU Plc), unatarajiwa kuwawezesha wakulima kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Akizungumza wilayani Kiteto wakati wa uzinduzi wa mradi huo wa umwagiliaji, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Peter Isare, alisema kampuni imetenga Sh. bilioni 7.5 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

"Ipo fursa ya uwekezaji kwenye eneo hilo kwa kua ardhi yake ina rutuba lakini ukosefu wa mvua ndio tatizo," alisema.

"Hivyo tumeamua kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji ili kusaidia wakulima wa maeneo hayo na wanaotoka nje ya wilaya kunufaika na fursa ya kilimo, na kuchochea upatikanaji wa malighafi za viwandani," aliongeza.

"Tumeamua kuwawezesha wakulima kuachana na kilimo cha kutegemea mvua ambazo hazina matarajio ya moja kwa moja, hali inayoathiri uzalishaji bora wa mazao," alifafanua Isare.

Isare alisema mradi huo utawezesha wakulima kupata mavuno kwa wingi kwa kuwa watalima mara tatu ndani ya mwaka mmoja.

Kampuni imetenga hekari 500 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na matarajio ni kufika hekari 1,500 ili kutoa fursa ya uzalishaji wa mazao kwa wingi na ajira kwa vijana.

Kampuni imeanza kuchimba visima vikubwa na vya kisasa vitakavyowezesha kutoa huduma kwa wakulima zaidi ya 1,000 waliopo kwenye Wilaya ya Kiteto wanaolima mahindi na alizeti.

"Kiteto ni wilaya yenye ardhi yenye rutuba nyingi kwa ajili ya kilimo, ingawa inakabiliwa na tatizo la uhaba wa maji kutokana na asili ya eneo hilo kuwa nusu jangwa," alisema Isare.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Tamim Kambona, alisema mradi huo umekuja wakati mwafaka kwani utawasaidia wakulima wa wilaya husika Kata ya Matui kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua na kuhamia kwenye kilimo cha kisasa cha umwagiliaji.

Ameongeza kua Wilaya ya Kiteto inakabiliwa na ukame wa muda mrefu unaoathiri uzalishaji wa mazao kwa wingi na kusababisha wakulima kukosa kipato cha kuridhisha.

# Mshindi wa nishati mbadala afunguka

Na Mwandishi Wetu

JITIHADA za makusudi zinazofanywa na wadau wa mazingira katika kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala wa kupikia zimeanza kuzaa matunda baada ya washindi wa shindano la nishati mbadala kueleza mafanikio hayo.

Mshindi wa Shindano hilo lililoandaliwa na Shell Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Joyce Ndonde wa Kampuni ya Kuja na Kushoka, amesema limeleta mafanikio makubwa kwani washindi waliopatikana wametumia vyema fursa kwa kuzalisha nishati hiyo ya mkaa mbadala ambayo ni rafiki kwa mazingira na kuvutia watumiaji wengi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Ndonde ambaye ni Msimamizi wa Mradi wa Kampuni ya Kuja na Kushoka, alisema walikuwa washindi wa kwanza wa shindano na kwamba kumekuwa na mwitikio mkubwa kwa Watanzania katika kutumia nishati hiyo ambayo kampuni yake inazalisha.

"Kumekuwa na mwitikio mkubwa kwa wateja wanaotumia nishati hii ya mkaa mbadala jambo linalotulazimu kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya soko" alisema Ndonde.

Aidha, katika kuifanya bidhaa hiyo iwe na ubora unaohitajika, wameanza kufanya mazungumzo na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na TIRDO ili kuifanya bidhaa hiyo kuwa bora zaidi na rafiki kwa mazingira hapa nchini.

"TBS ndio watu wanaohusika na udhibiti wa viwango vya ubora, walishatutembelea ofisini kwetu na kutupa maelezo ya awali juu ya namna nzuri ya kuwa na bidhaa ambayo itakuwa bora na rafiki kwa mazingira, tunaamini tutafikia viwango vinavyohitajika ili kuyanusuru mazingira yetu," alisema.

Ndonde alieleza changamoto ambayo wanakutana nazo katika uzalishaji, ni pamoja na upungufu wa vifaa vya usambazaji wa bidhaa, ukosefu wa jua la kutosha hasa katika kipindi hiki cha mvua na mazingira ya ofisi ambayo yamekuwa sio rafiki. "Ukiondoa mafanikio tunayoyapata sokoni, tumekuwa na changamoto kubwa katika mazingira yetu ya ofisi kwa kuwa eneo tulilopo haliruhusiwi kuboreshwa chochote hali inayotupa mashaka makubwa katika usalama wa rasilimali tulizonazo hapa ofisini," alieleza Ndonde.

Alizishukuru taasisi za umma ikiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais, Wakala wa Misitu (TFS), TBS pamoja na TIRDO na taasisi binafsi ikiwamo Shell Tanzania kwa jitihada zao za kuhakikisha nishati hii ya mkaa mbadala inawafikia Tatanzania ili kuyalinda mzangira kwa faida ya kizazi cha leo na kesho.

"Tunazishukuru taasisi zote za umma na binafsi na hasa Shell Tanzania kwa namna wanavyosimamia jitihada hizi za kuwa na mkaa mbadala. Wito wangu kwa Watanzania kuona wakitumia bidhaa hii ambayo ni rafiki katika kuyatunza mazingira yetu na gharama zake ni nafuu zaidi," alisema.

Kampuni ya Kuja na Kushoka Tools Manufactures Group Company ambao ni watengenezaji na wauzaji wa mashine za kuzalisha mkaa mbadala, wamekuwa wakishirikiana na taasisi za umma na sekta binfsi katika kuhakikisha elimu ya matumizi ya mkaa mbadala inawafikia walengwa katika ngazi mbalimbali.

# Wakala wa kilimo maua, mboga, matunda mbioni

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MCHAKATO wa serikali kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Kilimo cha Maua, Mboga, Matunda na Viungo maarufu kama 'Horticulture' ili kuchochea mkakati mpya wa kufikia mapinduzi ya kijani, umeiva.

Jana, Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wakala huyo atajulikana kama 'Horticulture Development Agency' (HDA).

Kwa mujibu wa Bashe, mchakato huo utakuwa umekamilika rasmi ifikapo Februari mwaka 2020, ukilenga zaidi kuchochea ukuaji wa sekta ndogo ya kilimo hicho.

"Wakala wa Maendeleo ya Kilimo cha Maua, Mboga na Matunda atasaidia kuondoa vikwazo vyote vinavyokwaza sekta hii ndogo, lakini yenye manufaa makubwa na kuchochea ukuaji wake kwa kasi,"alisema Bashe.

Bashe, alidokeza kuhusu mchakato huo, baada ya kukutana na wadau wa sekta hiyo wakiongozwa na Taasisi Kilele ya Kilimo hicho yaani Tanzania Horticultural Association (TAHA).

Chombo hicho kinachotarajiwa kuibeba sekta hiyo, kinatajwa kwamba kinapaswa kuchangia kwenye uchumi wa taifa kiasi cha dola za Marekani bilioni 1.85 kwa mwaka ifikapo mwaka 2021.

Mchango huo wa sekta ya matunda na mboga utakuwa umepanda kutoka dola milioni 764 za Marekani inayochangia kwa sasa na kuajiri vijana na wanawake kwa wingi.

"Serikali imeamua kwa makusudi kabisa kuipa kipaumbele sekta ndogo ya horticulture ambayo inakua zaidi ikilinganishwa na kilimo cha mazao mengine ya biashara kama pamba, kahawa, korosho, tumbaku na mengine," alisema Bashe.

Takwimu za Wizara ya Kilimo zinaonyesha kuwa sekta ndogo ya horticulture inakua kwa asilimia 11, wakati sekta nzima ya kilimo inakua kwa takribani asilimia nne tu. Bashe alisema Wizara ya Kilimo inabadilisha sheria kwa lengo la kuunganisha mamlaka za udhibiti ili kupunguza urasimu, kurahisisha taratibu za kusafirisha mazao nje ya nchi na kuwapunguzia mzigo wa tozo wakulima wa horticulture.

"Tutahakikisha tunarahisisha uingizwaji wa teknolojia za kisasa ili kuinua kilimo cha horticulture, usafirishaji wa mazao, uboreshaji wa miundo mbinu na pia kutenga maabara tatu maalumu kwa ajili ya kupima mazao ya horticulture kwa ajili ya masoko ya nje," alisema Bashe. Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, aliitaka TAHA kuandaa orodha ya kodi sumbufu na kuziwasilisha kwenye kikosi kazi cha bajeti cha Wizara kwa ajili ya kutafutiwa ufumbuzi ikiwamo kufutwa.

Aliitaka TAHA kuangalia uwezekano wa kukodisha ndege kwa ajili ya kusafirisha mazao hayo nje ya nchi, na kwamba serikali itasaidia mpango huo wakati inaangalia uwezekano wa kununua ndege maalumu ya mizigo.

Naye, Mkuu wa Kitengo cha Utafiti wa Masoko wa Mamlaka ya Bandari nchini (TPA), Lydia Mallya, alisema wanafikiria kuanzisha kitengo maalumu cha kuhudumia mazao ya horticulture bandarini kwa ufanisi zaidi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Mifugo, Mahmoud Mgimwa, alisema kamati yake itafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kusaidia kukuza kilimo cha horticulture.

Awali, akiwasilisha matatizo na fursa za sekta ndogo ya horticulture, Mkurugenzi Mtendaji wa TAHA, Jacqueline Mkindi, alisema mkulima aliyerasimisha shughuli zake za kilimo analipa kodi na tozo mbalimbali zipatazo 47 kwa mwaka, jambo ambalo ni mzigo mzito kwa mkulima.

Mkindi alisema: "Ili kukuza horticulture kwa kasi, serikali inapaswa kuboresha mazingira ya kufanya biashara, kubadilisha sheria ya mazao, kurahisisha usajili wa viwatilifu vinavyohitajika kwenye mazao ya mboga, matunda na maua.

Mkindi aliiomba serikali kusaidia uanzishwaji wa vyuo binafsi vya mafunzo ya kilimo cha horticulture kwa vitendo, kuboresha mitaala ya kufundishia wataalamu wa kilimo hicho katika vyuo vya Horti-Tengeru na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na pia kurahisisha utoaji wa vibali vya kufanya kazi kwa wataalamu kutoka nje

Distributed via ippmedia




Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Ombeni Msuya (kushoto), akitoa taarifa kwa Wajumbe wa Tume ya Maadili na kupambana na Ufisadi Nchini Kenya, chuoni hapo, jijiji Dodoma jana, kuhusu mipango mikakati ya chuo kupambana na rushwa pamoja na utovu wa nidhamu wa watumishi na wanafunzi. Ujumbe huo, upo nchini kubadilishana uzoezi namna ya kupambana na rushwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wanufaika wa Tasaf wajikita mradi nyuki

**Na Elizabeth Zaya,** MAKETE

WANUFAIKA wa Mpango wa kunusuru kaya masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), katika Kijiji cha Kemilembe, Halmashauri ya Makete wameanzisha mradi wa ufugaji wa nyuki.

Katibu wa mradi huo wa kijiji hicho, Thomas Mbugai, alisema mradi huo uliibuliwa na walengwa wenyewe kwa ajili kujiongezea kipato.

"Tasaf wametuletea utaratibu wa kuwashauri walengwa kuibua miradi ambayo wanaamini kwamba inamanufaa kwao na wanapofanya hivyo huwa wanawasaidia kuhakikisha wanaitekeleza, ndivyo ilivyo na hapa kwetu tulipoona kwamba ufugaji wa nyuki utaleta tija, tuliwaambia, na ndiyo maana tumeanza,"alisema Mbugai.

Alisema kwa hatua za awali wameanza na mizinga 120 na wanatarajia kuongeza zaidi kulingana na namna watakavyoona maendeleo yake.

"Walengwa wa Tasaf katika kijiji hiki wapo 41, kwa hiyo tunaamini kwamba kwa mizinga hii 120 endapo uzalishaji utakuwa mzuri kama tulivyoshauriwa na mtaalam kila mlengwa atanufaika sana,"alisema Mbugai.

Kwa upande wake Ofisa Mifugo wa Makete, Saimon Mbilinga, alisema wamekuwa wakiwafundisha walengwa hao namna ya kufuga kitaalam ili kuwasaidia ufugaji wao uwe wenye tija na wavune asali nyingi ya kuwapatia faida.

"Tunatarajia kwamba ndani ya miezi sita, wataanza kulina asali, na endapo mambo yataenda vizuri kitaalam kutokana na mizinga waliyonayo watakuwa wanapata faida ya Sh.milioni 60 kwa mwaka, "alisema Malima.

Aliongeza: "Tunawapongeza Tasaf wamefanya kazi nzuri ya kuziinua kaya hizi hususani kwa kuwashika mkono katika miradi hii ambayo tunaamini huenda ikawa mkombozi kwao, kwa hiyo na sisi inabidi tuonyeshe mchango wetu pale wanapoishia kwa kuwasaidia kuendesha miradi yao kitaalam na iwe na tija, "alisema Malima.


# Jela miaka mitatu dawa za kulevya

**Na Mwandishi Wetu,** pemba

MOHAMED Salum Mohamed (37) mkaazi wa Mtuhaliwa Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba, amehukumiwa kwenda jela miaka mitano au kulipa faini ya Sh.milioni 40, baada ya kupatikana na kete 126 za madawa ya kulevya aina ya heroin yenye uzito wa gramu 2.28. Hukumu hiyo ilitolewa katika mahakama ya Mkoa 'A' Chake Chake na Hakimu Abdul-kadir Abdul-razak Ali. Hakimu wa alitoa hukumu kwa mtuhumiwa huyo na kumtaka kwenda kutumikia kifungo cha miaka mitano au kulipa faini ya Sh.milioni 40.

Awali ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Aprili 4, mwaka huu saa 11:20 jioni Mtuhaliwa Wilaya ya Mkoani kwa kupatikana na kete 126 za dawa za kulevya aina ya heroin yenye uzito wa gramu 2.28.

Kufanya hivyo ni kosa kinyume na kifungu cha 15 (1) (a) cha Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Sheria namba 9 ya mwaka 2009, Sheria ya Zanzibar kama ilivyorekebishwa na Sheria namba 12 ya mwaka 2011, Sheria ya Zanzibar.





# Mapya kupotea fedha za kikundi

**Na Allan Isack** ARUSHA

SAKATA la Kikundi cha Ujasiriamali cha Imani kilichopo Ngusero jijini Arusha, kuibiwa fedha za mgawo Sh. milioni 39, limechukua sura mpya, baada ya maofisa wa Takukuru mkoani hapa wakiambatana na wanakikundi hicho kuvamia nyumbani kwa mweka hazina na kufanya upekuzi kusaka fedha zinazodaiwa kupotea katika mazingira ya kutatanisha

Wanakikundi hao walifika nyumbani kwa mweka hazina, Halima Mwidadi, mapema jana wakiwa na viongozi wa serikali ya mtaa (balozi wa nyumba kumi) kisha kufungua kisanduku kilichokuwa kikihifadhi fedha hizo na vitabu vya kumbukumbu.

Hata hivyo, baada ya kisanduku hicho kufunguliwa wanakikundi hao ambao wengi wao ni wanawake, walipigwa na butwaa baada ya kukuta kiasi kidogo cha Sh. 145300.

Kiasi kingine cha Sh. 315,000 zilikutwa zikiwa kwenye bahasha, huku kiasi kikubwa cha Sh. milioni 39 bila kuwapo, jambo lililozua taharuki na baadhi yao kuangua kilio upya.

Mmoja wa wanakikundi hao, Grace Kened Magala, alisema walifika nyumbani kwa halima Mwidadi kwa lengo la kutafuta fedha zao zinazodaiwa kupotelea nyumbani kwa mweka hazina huyo, ambaye bado anashikiliwa na Takukuru kwa ajili ya uchunguzi.

Pia, alisema kwa mujibu wa nyaraka mbalimbali ikiwemo vitabu vya kumbukumbu vya mahesabu waliyokuwa wakizitumia wakati wa mawasilisho ya fedha zao, ilikuwa kila mwanakikundi ajiridhishe na fedha anayodai kwa mwekahazina .

Maofisa wa Takukuru hawakuwa tayari kuzungumzia jambo hilo, lakini walisema kwa kifupi wapewe muda wafanye kazi yao, na kuwa wakikamilisha watatoa taarifa.

Kabla ya Mwidadi kukamatwa na Takukuru, alikuwa akijitetea kwamba fedha hizo zimepotea kimazingara nyumbani kwake, huku akidai kuna 'chuma ulete' iliyotafuna fedha hizo, utetezi ambao hata hivyo umepuuzwa na wanakikundi wenzake na kuamua kwenda kwenye vyombo vya sheria.



Distributed via ...media

Mafundi wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) Mkoa wa Arusha, wakiendelea na operesheni ya kubomoa vibanda mbalimbali na nyumba zilizojengwa chini ya njia za umeme mkubwa wa 66 kv, unaopita katika Kata ya Ungalimited, pamoja na Daraja Mbili, jijini humo jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Dawa migogoro waajiri, waajiriwa hii

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAAJIRI na waajiriwa nchini, wametakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kazi, ili kuepukana na migogoro isiyokuwa na tija kazini.

Hayo yalisemwa na wakili wa Kampuni ya Uwakili ya Claritate Legal Consultant, Peter Kivuyo, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, wakati wa semina kwa waajiri na waajiriwa iliyofanyika jijini Arusha.

"Endapo waajiri na waajiriwa mtazingatia sheria, kanuni na taratibu za kazi mtaepuka migogoro isiyokuwa na tija sambamba na gharama ambazo mnazitumia kuwalipa mawakili kusikiliza kesi zenu," alisema Kivuyo.

Alisema lengo la semina hiyo ni kutoa elimu itakayosaidia kuondoa misunguano kati ya waajiri na waajiriwa kutokana na pande hizo kutokuwa na uelewa wa kutafsiri sheria za kazi.

Aliongeza wao kama mawakili si jambo jema kufurahia migogoro hiyo ili kujipatia ujira badala yake wameamua kutoa elimu hiyo kama njia pekee itakayosaidia kupunguza misuguano isiyokuwa ya lazima.

"Kasi ya kukimbilia mahakamani kwa waajiriwa imekuwa ikiongezeka kila mara, na hii inatokana na waajiri kutotaka kufuata sheria za kazi ambazo zipo wazi," alisema Kivuyo.

Alisema tatizo kubwa lililopo kwa waajiriwa ni kusimamishwa ovyo na waajiri wao bila kufuata utaratibu na kunyimwa au kupunjwa stahiki zao, na kuwa hatua hiyo husababisha pande hizo kufikishana mahakamani, hivyo kuwagharimu kwa kutumia rasilimali fedha na kuwapotezea muda.

Alisema waajiri na waajiriwa wakiielewa sheria za kazi, wana imani migogoro hiyo, itakwisha na hatimaye pande hizo kuwa na mahusiano mazuri .

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, alisema migogoro isiyokuwa tija kazini imekuwa ikichangia kurudisha nyuma maendeleo na mpango wa serikali ni kutatua migogoro iliyopo kati ya mwajiri na waajiriwa.

Alisema serikali itatatua migogoro hiyo mapema kabla ya kufikishwa mahakamani ili kulinda mahusiano kati yao na waajiriwa.

Kwitega alisema waajiri walipata mafunzo hayo kama watayatumia vizuri, yatawasaidia kuondoa migogoro na migongano katika taasisi za umma na watu binafsi.

## Ushauri wa kukamilisha elimu ya ufundi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZAZI na walezi wametakiwa kutoa hamasa kwa watoto kujifunza elimu ya ufundi ili kuendeleza vipaji vitakavyowasaidia kuajiriwa na kujiajiri watakapohitimu.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Chuo cha Ufundi cha Help to Self Help, kilichopo jijini Arusha, Amani Golugwa, katika mahafali ya 20, na wanafunzi 93 waliohitimu kozi mbalimbali za ufundi.

Alisema chuo hicho kinatoa kozi mbalimbali za ufundi kwa wanafunzi hao na wamewaandaa kitaaluma kukabiliana na soko la ajira kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo watakapohitimu mafunzo.

Golugwa aliwataka wazazi kuwahamasisha watoto kujiunga na elimu ya ufundi ambayo itawawezesha kujiajiri haraka, na kuondokana na changamoto ya kusaka ajira baada ya kuhitimu.

Alisema tangu kuanza kwa chuo hicho mwaka 1993, zaidi ya vijana 5,000, wamejiajiri na kufungua shughuli mbalimbali za kiufundi ndani na nje ya nchi .

"Pamoja na mafanikio tuliyonayo, bado chuo chetu kinakabiliwa na tatizo la wazazi kutowalipia ada wanafunzi kwa wakati, ingawa vijana wengi wamekuwa na shauku ya kujiendeleza , lakini tatizo limejitokeza kutokuona umuhimu wa kuwekeza kwenye elimu," alisema Golugwa.

Mgeni rasmi katika Mahafali hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Help to Self Help, Mchungaji Peter Golugwa, aliwataka wazazi kuongeza bidii ya kusomesha watoto wao hususan kuwapa elimu ya ufundi ili waweze kujitegemea na kuondokana na tatizo la kuwa tegemezi katika jamii.

Aliwataka kujiendeleza zaidi kwani elimu waliyoipata ni ya bado haitoshelezi mahitaji yao. Pia aliwasisitiza kuitumia elimu hiyo, kuwa chachu ya mabadiliko katika jamii pamoja na kuwasaidia vijana wengine.

Mkuu wa chuo hicho, Eliza Kiwia, alitoa wito kwa wazazi na walezi kupeleka watoto kupata elimu ili wajifunze zaidi kwa vitendo. Mmoja wa wahitimu wa kozi ya umeme, Diana Dickson, alisema chuo kimewaandaa katika fani ya ufundi kwa vitendo zaidi, ikiwamo katika kozi za ushonaji, upishi, uhudumu, mapokezi ya wageni, ufundi umeme wa majumbani na wa nishati ya jua.

## Fursa ya mikopo kwa wanawake

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANAWAKE wametakiwa kutumia fursa za fedha za mikopo zinazotolewa na halmashauri kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na taasisi nyinginezo ili kukabiliana na umaskini katika jamii.

Mkurugenzi wa taasisi isiyo ya kiserikali Sophia Islamic Foundation ya mjini Moshi, Sophia Said, alisema kama wanawake watatumia vyema fursa hizo ni dhahiri wataweza kupambana na umaskini kama ilivyo dhamira ya serikali.

Alisema wanawake katika jamii wana mchango mkubwa katika kuleta maendeleo, hivyo kinachotakiwa ni kupewa motisha na kukumbushwa uwapo wa fursa hizo zenye lengo la kukabiliana na umaskini.

"Nimekuwa nikifanya kazi na wanawake, na mara kadhaa nawasisitiza ni lazma tujikwamue na lindi la umaskini kwa kutumia vyema fursa zinazotuzunguka,'" alisema Sophia.

Alisema kutokana na hofu na woga walionao wanawake wengi, wamekuwa wakishindwa kutumia fursa ya kuchukua mikopo inayotolewa na halmashauri kwa lengo la kujinufaisha wenyewe kimaendeleo.

Alieleza muda umefika sasa wa wanawake kujitambua kwa kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo badala ya kukaa chini kusubiria kuletewa na kuwataka kuunda vikundi vya maendeleo ili kunufaika na fedha hizo za serikali.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la TUSONGE linalojihusisha na kujenga uwezo kwa wanawake waliopo katika vikundi, Agnatha Rutazaa, alisema kinachotakiwa sasa ni wanawake wengi kupewa elimu juu ya fursa zilizopo.

Alisema wanawake wengi wamekuwa na uelewa duni juu ya fursa zilizopo, hivyo kwa kujengewa uwezo ni ukweli usioacha shaka kuwa maeneo ya wanawake yaliyokuwa yameonekana kukwama yataanza kufanya vizuri.

# Mkoa una uhaba nafaka tani 92,627

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAKATI Serikali ikishtushwa kwa kupanda kwa bei ya mahindi kufikia Sh. 107,000 kwa gunia, Mkoa wa Kilimanjaro unakabiliwa na uhaba wa mazao ya nafaka tani 92,627 ili kukidhi mahitaji ya wananchi wanaokadiriwa kufikia 1,906,978.

Hayo yalibanishwa na Ofisa Kilimo Mkoa wa Kilimanjaro, Saimon Msoka, katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya mkoa, ambapo alisema mahitaji ya chakula kwa mkoa makadirio ya mwaka ni tani 452,431 za mafaka na tani 45,243 za protini (mikunde).

Msoka alisema kutokana na msimu wa kilimo cha masika 2018/19 ambao ndio msimu mkubwa, unyeshaji wa mvua haukuwa mzuri kwani zilianza kunyesha baada ya kuchelewa sana mwanzoni mwa Mei tofauti na ilivyozoelekea huanza katikati ya Machi.

"Licha ya mvua hizi kuchelewa kunyesha, pia ziliwezesha mazao kuota na daadaye mwanzoni mwa Juni zilikatika wakati mazao yakiwa bado katika hatua ya ukuaji hali ambayo iliathiri uzalishaji na kusababisha mkoa kuwa na upungufu wa chakula katika kipindi cha 2019/20," alisema Msoka.

Aliongeza kuwa mahitaji ya chakula kwa mwaka ni tani 452,431 za wanga ambapo walizalisha tani 359,804, huku mahitaji ya protini ni tani 45,243 ambapo zilizozalishwa ni tani 61,614 kukiwa na ziada ya tani 16,371 za protini.

Alisema mikakati waliyojiwekea ili kukabiliana na upungufu wa chakula ni pamoja na viongozi katika ngazi zote kukumbushwa kuendelea kusimamia agizo la Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, la kuwataka kutotumia nafaka hususan mahindi kutengenezea pombe za kienyeji.

Mkakati mwingine ni wakulima kushauriwa kuhifadhi vizuri mazao waliyovuna kwa kutumia teknolojia mbalimbali ili kuhakikisha mazao hayo hayaharibiwi na wadudu yakiwa ghalani pamoja na wananchi wenye upungufu wa chakula kujinunulia chakula na kujiwekea akiba wakati bei bado hazijapanda.

"Tumekuwa tukiwashauri wananchi wenye mifugo kuuza baadhi ya mifugo yao ili kujipatia fedha za kununua chakula pia wafanyabiashara wa mazao tunawahimiza kununua vyakula kutoka sehemu zenye ziada na kuuza kwenye sehemu zenye mahitaji hasa mijini," alisema Msoka.

Alisema katika msimu wa kilimo 2019/20 mkoa umelenga kulima hekta 311,381 za mazao mbalimbali ambazo zitazalisha tani 1,360,930 za mazao mbalimbali ya chakula na biashara ambapo mahitaji ya pembejeo msimu huu ni mbegu za mahindi tani 2,135, mbegu za mpunga tani 450, mbegu ya mtama tani 29.

Mbegu nyingine ni alizeti tani 77 na mbolea tani 14,163.05 ambapo pembejeo hizo zitapatikana kwa mawakala wa pembejeo waliopo katika maeneo mbalimbali katika halmashauri zote.



Kamishna Mwandamizi wa Uhifadhi, Kanda ya Kaskazini,Herman Batiho akisaidia kusukuma kiti cha magurudumu cha mtu mwenye ulemavu, Deogratius Chami, wakati akipanda Mlima Kilimanjaro hivi karibuni. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**

# DC acharuka fedha za skimu umwagiliaji

**Na Mary Mosha,** KILIMANJARO

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amewataka viongozi wa ushirika kufuatilia tuhuma za ubadhirifu wa fedha za Skimu ya umwagiliaji ya mpunga ya Musa Mwijanga na kuuvunja ushirika huo uliopo kijiji cha Mijongweni Kata ya Mnadani.

Akizungunza na Nipashe alisema ushirika uliokuwapo umeshindwa kutimiza majukumu yake kutokana na kuyumbishwa na baadhi ya wanasiasa, hali iliyopelekea wakulima kushindwa kujipatia maendeleo kupitia miradi inayoainishwa na serikali.

"Wanasiasa wamekuwa wakiyumbisha ushirika huo ambao ndani yake kumeonekana na kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha... nimetoa wiki mbili viongozi wa wilaya wahakikishe wamefuatilia na kuleta taarifa ya fedha ili kuwasomea wanaushirika mapato na matumizi pamoja na kuweka mikakati ya namna ambavyo wanaweza kujiendeleza wenyewe kupitia miradi ya maendeleo katika skimu hiyo," alisema na kuendelea:

"Mwaka 2014, Wizara ya Kilimo ilitoa mashine za kuvunia na kukoboa mpunga katika skimu ya umwagiliaji ya mpunga zenye thamani ya Sh. milioni 250 wakitegemea kuwapo kwa maendeleo makubwa ya kiuchumi kwa wakulima hao, lakini wimbi la wanasiasa wamewalaghai na kuonyesha kukwamisha maendeleo yao."

Alisema inasikitisha kuona takribani miaka mitatu mashine hizo zimeshindwa kufanya kazi licha ya wakulima wa skimu hiyo kuunda ushirika uliotarajiwa kuwa na uwezo mkubwa wa kuendesha skimu hiyo.

Wakizungumzia changamoto katika chama hicho cha Ushirika, baadhi ya wakulima Nassoro Kibanda na Juma Ngoma waliutupia lawama uongozi wa kijiji kwa kushindwa kushirikiana na ushirika huo ili kuwaletea maendeleo wanakijiji hao.

Mhandisi Said Ibrahimu, kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, aliwataka wataalamu wa skimu ya Musa Mwijanga kutoa elimu ya kilimo cha kisasa kwa wakulima sambamba na kuwaonyesha umuhimu wa kuacha siasa za kuzalisha kwa wingi ili kujikwamua kiuchumi.

ama
ALHAMISI NOVEMBA 21, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



**Profesa Museru atangaza mageuzi makubwa Muhimbili ya sasa, ijayo**

Ukurasa 20



Wavuvi wahofu kisiwa chatoweka, fukwe zamomonyoka kila upande

Ukurasa 14



Ukurasa 18

## Gharama kutibu magonjwa ya tumbaku, kiwango kinatisha



MOJA KWA MOJA SEKOU TOURE...

# Mjamzito 'anayesubiria' afunguka anahusudu kupitiliza mitishamba

Ukurasa 16




Mipira ya kiume aina mbalimbali. **PICHA: MTANDAO.**

# Kondomu feki milioni zanaswa

**Kampala, Uganda**

SHIRIKA la Maria Stopes nchini Uganda, linalotoa huduma ya kugawa kondomu, limezuia mipira zaidi ya milioni moja, ikidaiwa ubora wake ni batili

Majaribio ya ubora wa kondomu hizo zilizotengezwa nchini India, imebainisha zina matundu yanayohatarisha usalama wa mtumiaji, kwa mujibu Mamlaka ya Dawa ya Uganda (NDA).

Marie Stopes, inasimamia huduma hiyo katika nchi 35 duniani na nchini Uganda mwezi uliopita, iligawa mipira kati ya milioni moja na milioni moja na nusu.

Ni hatua inayotokana na tahadhari ya NDA baada ya kubaini upungufu wa ubora mwezi uliopita. Maria Stopes imesema inalifanyia kazi hivi sasa kwa kushirikiana na mamlaka hiyo ya kiserikali.

"Tunalifanyia kazi kwa haraka kuchunguza nini kilichotokea katika mzigo huu na kuhakikisha bidhaa zetu zinakidhi viwango bora," Marie Stopes inasema.

"Tunaweza kuthibitisha kurejesha mizigo miwili iliyokuwa vifurushi vya kondomu 335,000 kati ya milioni moja. Tumerejesha zaidi ya nusu mzigo," inafafanua.

## MAZINGIRA

### WALIA MAFIA INAZAMA

# Wavuvi wahofu kisiwa chatoweka, fukwe zamomonyoka kila upande

**Na Gaudensia Mngumi, aliyekuwaMAFIA**

TAKRIBANI kilomita 10 kutoka Mafia mjini, ipo kambi ya wavuvi ya Kitoni. Wengi hupaita Dagoni. Ni sehemu wavuvi wanapopiga kambi kabla ya kwenda baharini.

Aidha, ni kituo cha kushusha samaki, kuuza, kuangalia zana ikiwamo kufua na kuanika nyavu, kuangalia au kukarabati chombo pamoja na kupanga mikakati ya kuvua.

Kwenye eneo hilo, kunahitajika matengenezo na kubadilisha mazingira ni kwa sababu bahari inaongezeka kina, ina mawimbi makali na ina kila dalili za kutafuna ufukwe na kutishia hatima ya ardhi ya makazi, kilimo na utalii.

Hayo yanaonekana, wakati wa ziara ya wanahabari wilayani Mafia iliyoandaliwa na Shirika la Action Tanzania (AATZ).

Taasisi inashirikiana na jamii za Mafia kuzuia ukatili dhidi ya watoto wa kike, kuboresha elimu, usawa wa kijinsia na matumizi endelevu ya rasilimali ikiwamo bahari na ardhi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuzinusuru familia na njaa.

Ukiwa Kitoni, si jambo linalohitaji utafiti kila kitu kinaonekana, minazi na miti mingi imeng'olewa na kuburuzwa hadi majini na mawimbi. Ufukwe umesogea zaidi kwenye nchi kavu na ushahidi ni magogo makavu ya miti, ikiwamo mikungu, minazi na mikuyu ndani ya bahari.

Wakiwa pwani ya Kilindoni, baadhi ya wavuvi wanasema takribani miongo minne iliyopita, miti hiyo ilikuwa mbali na ufukwe, lakini sasa iko ndani ya bahari na hilo limetokea baada ya mawimbi kumega zaidi ya mita 25 za ardhi na sasa zimemezwa kuwa sehemu ya bahari.

Anazungumza na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Miburani iliko kambi ya Kitoni, Selemani Haji, anaiambia Nipashe, eneo kubwa la ardhi limemomonyoka na sasa limemezwa na bahari, ikiwa matokeo ya uharibifu mkubwa wa mazingira katika miaka ya nyuma.

Anasema, athari hizo zinatokana na ukataji mikoko na uvuvi haramu. Anataja kazi ya mikoko kuwa ni kuzuia kasi ya mawimbi na kuyakwamisha yasifike nchi kavu hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira na mmomonyoko ufukweni.


Distributed via ippmedia

Mandhari ya kisiwani Mafia kutoka angani, ikiwamo uwanja wa ndege. **PICHA: MTANDAO.**

> **Mwenyekiti wa ushirika wa Twendekazi, Mwalimu Nahodha, anaiambia Nipashe kuhusu mradi wa kulinda mazingira, kwamba wana boti la kisasa na vifaa vya uvuvi wakijihusisha na kuvua pweza.**

Haji anasema, jitihada zimefanyika kupanda miti ikiwamo mivinje na mikoko, pia kuzuia watu kukata mikoko, mambo ambayo angalau yamedhibiti kasi ya maji na kuzuia mmomonyoko ufukweni.

Haji anasema, wataalamu wakiwamo maofisa wa Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Mazingira (WWF) na serikali kwa kipindi cha miaka sita walishirikiana na wananchi kupanda mivinje na kustawisha mikoko kupunguza uharibifu huo.

**WAVUVI WALALAMA**

Kambi ya Kitoni iliyoko katika kijiji cha Miburani wilayani Mafia, inaundwa na ushirika wa wavuvi na wanachama wa ushirika wa kuvua wa Twendekazi, kikundi chenye wanachama takribani 32 waliojiunga pamoja kununua hisa 10, kila moja ikiuzwa Sh. 5,000.

Kikundi cha Twendekazi kinaundwa kwa msaada wa asasi ya Action Aid, ambao pamoja na kuwasaidia utaalamu wa uvuvi endelevu, wamepatiwa boti ya kisasa, injini na nyavu.

Mwenyekiti wa ushirika wa Twendekazi, Mwalimu Nahodha, anaiambia Nipashe kuhusu mradi wa kulinda mazingira, kwamba wana boti la kisasa na vifaa vya uvuvi wakijihusisha na kuvua pweza.

Kuhusu uharibifu wa mazingira, anasema kinachojiri kwenye eneo hilo na sehemu nyingine za pwani ya Mafia, ni uthibitisho wa uharibifu wa bahari, unaochochewa na mabadiliko ya tabianchi na binadamu.

Mwalimu Nahodha, anaeleza ilipofika mwaka 1970, alianza kuingia baharini wakati huo akiwa na miaka 20. Ni zama anazosema hakuhitaji vifaa vingi, vyombo vikubwa wala muda zaidi wa kuvua baharini, kwa vile kila samaki aliyemtaka alionekana kirahisi na ilikuwa mithili ya kumuokota.

"Pweza, ngizi, jongoo bahari, kitonge, changuu walikuwa wanaelea majini hadi ufukweni. Haikuchukua muda kufika pwani na kurudi kijijini au nyumbani na kitoweo cha kutosha, " anaeleza Nahodha.

Vilevile, anasema uharibifu wa mazingira umesababisha uvuvi kuwa mgumu mno na ili kopata samaki, sharti mvuvi aende mbali sana.

Huku akikiri kwamba, japo si mtaalamu halisi wa ardhi na mazingira, lakini kisiwa cha Mafia kinapungua ukubwa kila mwaka na samaki sasa hawapatikani tena kirahisi, baadhi yao wametoweka, akitoa mfano wa samaki mkizi na kifimbo.

Anaungwa mkono na Salum

**Inaendelea Uk. 15**

MAZINGIRA

Inatoka Uk. 14

## WALIA MAFIA INAZAMA

# Wavuvi wahofu kisiwa chatoweka, fukwe zamomonyoka kila upande




Shughuli za uvuvi zikiendelea Mafia. **PICHA: MTANDAO.**

Masudi (65), aliyezaliwa Miburani Mafia na kuanzia uvuvi ufukweni Kitoni, anayeeleza kushuhudia bahari ikiwa katika hali nzuri, ila sasa inachafuliwa na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu mazingira.

Masud anasema, uvuvi haramu umeharibu mno bahari kwanza kwenye kutumia baruti kuvunja matumbawe na kukata misitu ya mikoko.

"Miaka ya 1990 hadi 2000, baruti zilipigwa sana baharini. Zimeharibu matumbawe na kuteketeza mazalia ya samaki na wengi wamekwisha labda kuwafuata bahari kuu," anafafanua Masudi.

Mvuvi huyo wa pweza aliyeanza kazi mwaka 1975, anayaona mawimbi yalikuwa hayana kasi ya uharibifu kama ilivyo sasa na kwamba watu wamechangia sana kulipua miamba ya matumbawe iliyokuwa inasaidia kupunguza kasi ya upepo.

Anafafanua kwamba, kuvunja mwamba kumechangia mawimbi kupita kwa kasi kubwa bila kizuizi, pia kukatwa anayoyaita 'mikoko' kumeyarahishia mawimbi kwenda kasi bila kupunguzwa nguvu hali inayochangia kasi ya mmomonyoko huo.

**VISIWA KUZAMA?**

Wanapozungumzia hatari kubwa zaidi, wavuvi hawa Masudi na Nahoda wanawakilisha maoni ya wana - Twendekazi, wanaoeleza Mafia ina visiwa sita vikubwa vyenye wakazi ni: Juwani, Jibondo, Chole, Bwejuu, Shungimbili na Nyororo.

Hata hivyo, anaeleza kuwa vipo baadhi ya visiwa kama Mivinjeni na Tosamitungi vinavyozama na vingine vinajaa maji na siku za nyuma eneo la Rasi ya Mafia, nayo lilizama.

Masoud, anatoa mfano kwamba licha ya visiwa hivyo kuendelea kuwapo, wanavijiji wake wanaoishi kwenye makazio wanayoyoita 'madungu' (nyumba za juu ya miti) kwa sababu kila wakati kisiwa kinamegwa na maji yanaongezeka kina.

Anasema, kisiwa cha Bwejuu kilichokuwa na hospitali, shule na ardhi ya kilimo shughuli za uzalisaji, zimekwama kutokana na kuanza kuzama.

**KUNUSURU MAZINGIRA**

Mwalimu Nahoda, anaeleza kwamba kushirikiana na Wakala wa Hifadhi ya Bahari Kisiwani Mafia, Shirika la Uhifadhi wa Mazingira la (WWF) na Serikali ya Miburani, wameanzisha Kamati ya Hifadhi ya Mazingira, inayolinda ufukwe na kupanda miti.

Ni miti inayopandwa ni pamoja na mivinje na mikoko na kwamba hairuhusiwi kukata mkoko na pale mwanakijiji anapoomba kukata analazimika kutoa maelezo ambayo hukubaliwa ama kukataliwa.

> Wanaeleza kuwa Mafia kuna kiwanda kimoja cha kusindika samaki, hali inayosababisha kukosekana ushindani wa bei kutokana na mfanyabiashara mmoja kuhodhi soko.

**MAELEZO SERIKALINI**

Kaimu Ofisa Mazingira wa Wilaya ya Mafia, Mtemi Kasuga, anasema jitihada zinazofanyika ni kushirikiana na Hifadhi ya Viumbe Bahari Mafia (WWF), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Viumbe Bahari na serikali za vijiji kupanda mikoko na mivinje.

Kazi hiyo imefanyika kwa kushirikisha kamati za hifadhi ya mazingira za vijiji na kwamba uhifadhi umefanyika katika vijiji vya Mlongo, Chemchem na Miburani kuanzia mwaka 2017 hadi sasa.

Anapoulizwa iwapo ana taarifa za madai ya baadhi ya visiwa vya Mafia kuzama ikiwamo Mivinjeni, alisema hana taarifa lakini akakiri kuwa kulikuwa na kisiwa Rasi Mafia kilichozama siku za nyuma.

**MAPENDEKEZO**

Wavuvi wengi wanaotoa maoni yao kupitia sauti ya ushirika wa Twendekazi, wanataka Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Halmashauri ya Mafia, kusaidia kupatikana au kujenga viwanda vya kuongeza thamani mazao ya baharini.

Wanaeleza kuwa Mafia kuna kiwanda kimoja cha kusindika samaki, hali inayosababisha kukosekana ushindani wa bei kutokana na mfanyabiashara mmoja kuhodhi soko.

Aidha, wanataka kuwekeza zaidi kwenye elimu ya ulinzi na utunzaji wa mazingira bahari, ili kuokoa rasilimali zake, kwa sababu kuna uvuvi uharamu unaofanyika bahari kuu hasa nyakati za upepo mkali.

Kadhalika , wanaiomba serikali kuzidisha mikakati ya ulinzi wa mazingira ya kisiwa cha Mafia, kwa sababu kinaumizwa na mawimbi ya pepo za Kaskazi na Kusi, ambazo hukipiga pande zote kila wakati.

Wanadai kuwa mara nyingi kampeni za kusimamia mazingira zinafanywa na wadau na mashiriki ya kiraia na kuitaka serikali iongeze bajeti na mikakati kufikia wananchi wengi.



Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Miburani, Selemani Haji, akizungumza na wavuvi wa kikundi cha Twendekazi, katika eneo ambalo miti imeng'olewa kutokana na kasi ya uharibifu wa mazingira, hasa mikoko. **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI.**

AFYA

MOJA KWA MOJA SEKOU TOURE...

# Mjamzito 'anayesubiria' afunguka anahusudu kupitiliza mitishamba

- Kanuni zake: vipimo rasmi, dawa kienyeji
- Atamba imempa neema ya watoto watatu
- Daktari Mkuu abakishwa mdomo wazi

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

ALHAMISI iliyopita, ilikuwa na sehemu kwanza ya makala hii kutoka jicho kuu la matabibu kuhusu madhara wajawazito kuendekeza mitishamba, badala ya dawa rasmi, Endelea na sehemu ya pili, simulizi kutoka mtumiaji, anayeanika sababu zake.

ALIYEKUWA Rais mwasisi wa China, Mao Tse Tung, alipenda kutamka "hakuna haki ya kusema, pasipo kuwapo ushahidi wa hakika."

Hata katika maandiko na mawasilisho ya kitaalamu, mara zote kunahitajika ushahidi na ufafanuzi wa kitaaluma, kutetea uwasilisho wa namna hiyo, ili ukubalike.

Upatanisho wa hoja hiyo, ni eneo la Kanda ya Ziwa, hivi sasa linalalamikiwa kuwapo tatizo sugu la kuendekeza dawa za asili, hali inayozaa madhara katika huduma za kitabibu hospitalini, kama vile mama kutokwa damu nyingi, vifo na vilema vya watoto .

Alhamisi wiki iliyopita katika jarida hili kulikuwapo makala ambayo Mratibu wa Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto, Mkoa wa Mwanza, Secilia Mrema, alieleza ilivyo 'pasua kichwa' kushawishi wajawazito wa eneo lake, kuegemea dawa za hospitalini, badala ya mitishamba.

Ni simulizi ya aina hiyo, pia katika jarida hilo ilipatikana kutoka Hospitali ya Wilaya Kahama, ambako kulijaa malalamiko dawa za asilia kuteka mkakati bora ya huduma za hospitali kwa wajawazito, hali inayoishia madhara makubwa kiafya kwa kinamama.

Kama inavyoelezwa katika nadharia , ili kupata picha sahihi ya undani wa jambo, marejeo makuu ni kuwapo ushahidi. Nipashe ilichukua hatua ya kusaka uhalisia, kutoka kwa muumini wa mbadala huo wa mitishamba. Nani huyo na ana nini? Ni Mwanamama Nusra Sued.

AFUNGUKA ANACHOKIAMINI

Nusra mwenye umri wa miaka 27, mkazi wa Buswelu jijini Mwanza, aliyelazwa kisubiri kujifungua katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza, Sekou Toure, hakuficha mtazamo anaoutetea mbele ya Mganga Mfawidhi, Dk. Bahati Msaki, kwamba imani yake imejikita huko.

"Hospitali, kituo cha afya, hata nikienda kutibiwa nikiwa naumwa, nikirudi nyumbani dawa za hospitali naziweka pembeni kulingana na ninavyojifahamu mimi, halafu natumia za kienyeji ambazo naamini kwa asilimia 99.



Mjamzito Nusra Sued (kushoto), akiwa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza,Sekou Toure, Dk.Bahati Masaki, siku alipohojiwa na gazeti hili. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

**"Mizizi ya mmea wa Mgagani akitumia mama mjamzito wakati wa kujifungua ni 'vurugu mechi' wodini, kwa sababu inaongeza uchungu kwa kasi ya ajabu na kusababisha mama majamzito kuchanika mfuko wa uzazi."**

"Ni nzuri, hazina madhara kuliko za hospitali, ingawa za kienyeji zinatibu polepole," anatoa ushuhuda huo Nusra pasipo woga wa kuthibitisha matumizi ya dawa hizo, akisimama katika imani yake kwamba hazina vipimo, mazumguzo anayofanya hospitalini.

Mjamzito huyo anatoa ushuhuda katika siku ya tatu wodini akisubiri kujifungua, ambaye tangu tarehe 9 mwezi huu alipotaarifiwa kupitia vipimo vya hospitali, kwamba muda wake wa kujifungua umewadia.

"Bado hadi sasa sijapata uchungu, ila mimi kwa uzoefu wangu ninavyofahamu bado siku za kujifungua hazijawadia," anadai Nusra

Baadhi ya dawa za kienyeji zinazotajwa kutumiwa na wajawazito ni pamoja na mizizi ya bangi na mgagani, majani yake na magome ya miti shamba, inayotajwa na matabibu rasmi inayohatarisha maisha.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto Mkoa wa Mwanza, Secilia Mrema, dawa za kienyeji zinapotumiwa na wajawazito, zinachangia madhara makubwa, ikiwamo kupoteza maisha.

"Dawa za kienyeji zimekuwa zikisababisha madhara makubwa ikiwamo kinamama wajawazito kuchanika mfuko wa kizazi kutokwa damu nyingi, wakati wa kujifungua na mtoto kufia tumboni kutokana na kwamba hazina kipimo," anasema Secilia.

Nusra mwenye asili ya mkoani Kagera, anathibitisha kutumia mitishamba miaka yote, akitaja maeneo ya tiba kama ya malaria, mkojo mchafu (UTI) na homa ya matumbo.

Anajigamba kuzitumia kwa makini, akizingatia masharti na historia ya ugonjwa kama ilivyo hospitalini, anakopewa dawa na kuelekezwa na daktari.

Huku akihimiza mtazamo na imani iliyomuacha msikilizaji wa pili, Mganga Mfawidhi abaki 'mdomo wazi' kwa upana wa mazito kutoka simulizi ya Nusra, kwamba dawa hizo, zipo anazoziita 'chungu' na 'baridi' kama zilivyo hospitalini na duka la dawa.

"Watoto wangu wote watatu nilikuwa nikijifungua kwa kutumia dawa za kienyeji na hata ujauzito huu tangu mimba changa, nimekuwa nikitumia dawa hizo hizo, ambazo husafisha hata magonjwa ya zinaa," anasema mjamzito huyo.

Nipashe ilipotaka kuzijua, Nusra amazataja majina yake ya 'dukani' kwamba ni: Kashwagala, Nzitoima, Mzambarau, Mizizi ya Miti Shamba, Majani ya Michaichai na Mshana inayotumika wakati wa jua kali yanapotokea magonjwa.

Kuhusu mchakato wa matumizi yake, anasema hutumika kuanzia mimba changa, akitaja dawa aina ya Mshana, nayosema ina uwezo wa kusafisha hadi muwasho katika sehemu za siri wakati wa ujauzito na ina uwezo wa kuongeza uchungu.

Mbele ya ushuhuda wa Mganga Mfawidhi hospitalini Sekou Toure, Nusra ana ufafanuzi: "Mimi siamini kama kweli dawa zile zina madhara hayo. Hiyo ni sawa na kila mwamba ngoma huvutia kwake."

Anahoji: "Mbona hata tukienda hospitali kutibiwa pamoja na dawa zao zina kipimo, lakini daktari anakwambia; hii dawa usinywe bila kula ni sumu mwilini? Kumbe hata zile za hospitalini zina sumu inayodhoofisha afya zetu, ingawa haionekani hapo hapo."

Nusra anaendelea kuziponda dawa za hospitali, akidai sio zote zinazoponyesha akitumia msamiati 'zinadunda' na anapotumia miti shamba anapona, mtazamo anaounganisha na imani kwa Muumba.

Anaenda mbali katika historia zama zilizopita, kwamba watu hawakwenda hospitalini wala kuchomwa sindano na walipona, akidai ni uzoefu unaoendelea sasa vijijini mgonjwa anafika hospitali kutambua kinachomsumbua na matibabu yake anarudia dawa za kienyeji.

'Mama mtarajiwa'huyo wodini Sekou Toure, anaendelea kumuanikia Mganga Mfawidhi

**MGANGA MFAWIDHI**

Baada ya sumulizi ya kina, Nipashe iligeuza mwelekeo kupata simulizi ya upande wa kitaalamu, kutoka kwa aliyekuwa shuhuda, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza - Sekou Toure, Dk. Bahati Msaki ana maoni yafuatayo:

"Mizizi ya mmea wa Mgagani akitumia mama mjamzito wakati wa kujifungua ni 'vurugu mechi' wodini, kwa sababu inaongeza uchungu kwa kasi ya ajabu na kusababisha mama majamzito kuchanika mfuko wa uzazi."

Dk. Bahati, anatahadharisha a madhara ya dawa hizo zilizokosa viwango, anaongeza dawa hizo zinasababisha figo na ini kushindwa kufanya kazi kutokana na kiwango cha sumu yake hakijulikani, hatari ikifikia balaa la kuchangia mauti.

Kutokana na hilo, mganga huyo mfawidhi anawasisitiza kinamama wenzake, kwenda kupata huduma bora katika vituo vya afya na hospitalini kuepuka utumiaji dawa hizo hatari kwa afya na maisha yao.

Dk. Bahati anasema, wamefanikiwa kupunguza vifo vya wajawazito hadi kufikia asilimia 50 kwa mwaka, kutokana na wengi wao kupata elimu ya madhara hayo na kuacha kutumia.

Anasema, hivi sasa kuna kitengo cha utafiti wa dawa za asili katika Idara ya Afya hospitalini hapo kinachofanya utafiti kuhusu madhara hayo, ili kupata majibu sahihi. Anaiasa jamii kubadilika kwa kuzingatia dawa za hospitalini

Anataja mkakati wao ni kuendelea kutoa elimu kwa wananchi na jamii nzima kwa ngazi zote, wakishirikiana na viongozi wa kiserikali ngazi za kata, tarafa,wilaya hadi mkoa, kuhusu vita ya pamoja dhidi ya watu na hasa wajawazito kujikita na dawa zisizokuwa na vipimo. Kwa mujibu wa Mratibu wa Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto, Mkoa wa Mwanza- Secilia, hatua mbalimbali zinafanyika, ikiwamo kuzuia wajawazito wanaopeana mitishamba kwa siri wodini, kwa kuwapekua na kutajana.

Pia, anasema elimu hiyo imefikishwa mbali, hadi katika maeneo ya misibani na wodini, wagonjwa watambue madhara ya dawa hizo.

***Soma zaidi makala Alhamisi ijayo***



. Mwandishi wa makala hii alipomhoji Nusra Sued. **NA MPIGAPICHA WETU.**



Diana Kamande. **PICHA: BBC**

## Aliyenusurika kuuawa na mume asimulia

DIANA Wanjiku Kamande wa Kenya, ni mama ya watoto wawili. Anapokumbuka yaliyomkuta mnamo mwaka 2013, hupatwa na mchanganyiko wa hisia; majonzi na furaha.

Hiyo ni kutokana na alivyonusurika mauaji kutoka kwa mtu aliyempenda. Anasumulia: "Nilikuwa msichana mdogo mwenye umri wa miaka 24 tulipoanza maisha ya kuishi pamoja sikufahamu mengi kuhusu ndoa."

Diana na mumewe walianza maisha kwa kuishi kwenye nyumba ya chumba kimoja , wakati huo alikuwa na ujauzito wa miezi mitano, mtoto huyo sasa ana miaka 10.

Anasema kipindi chote cha kuishi na mumewe, hakuwahi kumpigwa au kutukanwa na mume huyo hakuwa mlevi au wa kutangatangaa.

"Mambo yalibadilika tarehe 14 Aprili Jumapili hiyo, kama saa tano hivi za usiku , Richard aliwasili nyumbani akiwa mlevi, ilikuwa mara yangu ya kwanza kumuona akiwa amelewa... alikuwa ana tabia ambazo zilinichanganya sana, alisema...mpenzi nimerudi akijirudia rudia, pole nimechelewa, " anakumbusha.

"Sikutilia maanani sana, nikasema labda amelewa tu kama wanaume wengine," anafafanua.

"Siku ya Jumanne ya Aprili 16, anakumbuka mume huyo aliingia chumbani alipokuwa ananyoosha nguo, huku akiandamana na watoto wake wawili.

''Katika chumba hicho kulikuwa na picha yake, akaitoa kwenye ukuta na kusema akifa angependelea hiyo picha itumiwe wakati wa mazishi yake,'' anasimulia mama huyo, kuwa tukio lililomshangaza sana na mumewe aliporudi usiku siku iliyofuata alimuuliza sababu za kutamka maneno hayo mbele ya watoto na alishia kucheka.

Siku ya mkasa Richard alirejea nyumbani saa mbili usiku na kuelekea katika chumba chake, huku watoto wakimfuata nyuma na mumewe hakuzungumza kitu.

Diana alienda chumbani kuwaita watoto wake ili wale chakula cha jioni, naye Richard aliondoka tu ghafla na funguo zote za milango ya nyumba yao.

Diana anasimulia alipompigia simu, hakumjibu na alimundikia ujumbe wa 'sms'kumuuliza aliko, napo hakupata jibu. Walienda kulala, baada ya mlo na watoto.

Ghafla aliamshwa na maumivu makali niliyoyahisi kichwani mwake: Duasa anasimulia:"Damu ilikuwa inatiririka kama maji huku mume wangu akinikatakata kwa panga mkononi... alikuwa na panga mkono mmoja na kisu mkono mwingine, huku akiwa amelewa."

Diana anasema alianguka kutoka kitandani na mumewe aliondoka chumbani huku akidhani alishafariki an alimsikia akimpigia simu mama yake, kwamba tayari alishamuua na kisha yeye anajimaliza, akiomba ujumbe huo ampatie baba yake kwa simu.

"Mume wangu aliemueleza baba yangu:"Utayarishe majeneza manne... kuna mazishi hivi karibuni,"anaongeza na baada ya kukamilisha mazungumzo kwa simu, Diana anasema alimsikia binti yake akipiga mayowe akilia. baba usitue "

Hapo ndipo Diana alipata nguvu na kuinuka kukimbia katika chumba cha watoto, mume wake alikuwa amemshika binti yake ambaye aling'ang'ana mikononi mwake, huku na binti mwingine alilala, mume akitaja kumchoma kisu.

'Nilipaza sauti na kumuita 'Richard!," anasema, sauti ilimshitua mume akaangusha kisu alichokuwa na wakafanikiwa kutoroka.

Mume aliokota kisu na kumsukuma Diana kwenye ukuta alipomdunga na kumchoma mkononi, alipojaribu kujikinga, lakini Diana alifanikiwa kukimbia.

Anakumbuka matamshi ya mumewe "Afadhali tufariki humu ndani, lakini kama hutaki, basi nenda ukafe huko nje; mimi nitakufa humu ndani."

Majirani zake walimpeleka hospitalini, baadaye Diana alipokea simu kutoka kwa majirani zake waliomueleza kuwa mumewe alijitoa uhai kwa kutumia kisu kile kile alichomdunga Diana. ***BBC***

Distributed via ippmedia

AFYA

Na Mashaka Mgeta

# Gharama kutibu magonjwa ya tumbaku, kiwango kinatisha

## •Taasisi za Moyo, Saratani zadai udhibiti

VITUO viwili vikubwa vinavyohusika na kutibu magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) naTaasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), zimeweka bayana athari zinazosababishwa na tumbaku na bidhaa zake hasa sigara na kushauri jitihada za makusudi zichukuliwe kuinusuru hali hiyo.

Mkurugenzi wa JKCI, Profesa Mohamed Janabi, anasema kiasi cha kati ya Sh. milioni sita na nane zinatumika kwa matibabu ya mgonjwa anayehusishwa na uvutaji sigara, hivyo kuwa sehemu ya vigezo vinavyohalalisha udhibiti wa tumbaku na bidhaa zinazotokana na zao hilo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki katika warsha ya wanahabari kuhusu ushawishi wa sekta ya tumbaku kwa sera za afya nchini, Profesa Janabi, anasema tumbaku na bidhaa zake zinaathari nyingi na kubwa kuliko faida, ikitazamwa kwa haraka hasa katika mrengo wa kiuchumi.

Anatoa mfano, matibabu ya mgonjwa wa mishipa anayehusishwa na matumizi ya sigara na bidhaa nyingine za tumbaku, inagharimu fedha hizo, kwa mujibu wa matibabu ya JKCI.

Profesa Janabi anasema, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi Septemba mwaka huu, jumla ya wagonjwa 300,836 walifika JKCI na kati yao1,4960 walilazwa, ili kupata huduma za kusimamisha na kufungua moyo.

Kwa mujibu wa Profesa Janabi, wagonjwa 4,207 walikuwa wanakabiliwa na tatizo la mishipa ya damu kuharibika kwa asilimia 20, sawa na wagonjwa 842, walibainika kuvuta sigara.

Profesa Janabi anasema, udhibiti wa tumbaku na bidhaa zinazotokana na zao hilo, unakwamishwa zaidi na kampuni zenye uwezo mkubwa kiuchumi zinazotumia mbinu mbalimbali kujitangaza.

Anasema watoto wamekuwa sehemu ya waathirika wa matumizi ya bidhaa za tumbaku hasa sigara inayokadiriwa kuwa kemikali 700 na saba miongoni mwao zinahusishwa moja kwa moja na saratani.

"Kama hatukufanya 'intervention' (kuingilia kati) katika kudhibiti tumbaku na bidhaa zake, tunapokwenda hali itakuwa mbaya zaidi," anasema.

Anasema huduma nyingine inayotolewa kwa mgonjwa anayehusishwa na uvutaji sigara ni kupandikizwa mishipa kunakogharimu kiasi cha Sh. milioni 29.

Profesa Janabi, anasema fedha hizo kama zikiokolewa na kutumiwa kwa kutibu magonjwa ya kuambukizwa, zinaweza kutosha kwa wahitaji wa mkoa mmoja nchini.

Anarejea takwimu za mashirika kadhaa ya kimataifa yanayojihusisha na afya, sigara na bidhaa zinazotokana na tumbaku zinasababisha vifo vingi zaidi ya inavyotokana na pombe, virusi vya Ukimwi, kujiua dawa za kulevya.



Distributed via ipmedia

Mkurugenzi wa Chama cha Kuzuia Matumizi ya Tumbaku Tanzania (TTCF), Lutgard Kokulinda Kagaruki (kushoto), akionyesha mchoro wa mtu aliyeathirika na matumizi ya tumbaku. **PICHA: MAKTABA.**

> **Nchini Uganda, ilifika hatua serikali wakati fulani iliamua kurudisha matumizi ya dawa aina ya DDT, iliyopigwa marufuku duniani na Umoja wa Mataifa, miaka iliyopita, ikielezwa kwamba inaacha sumu isiyodhibitika katika mazingira, hasa imapoingia katika mkondo wa maji na chakula cha nyumbani.**

Kwa mujibu wa Profesa Janabi, kumtibu mtu ambaye mishipa yake imeharibika (sigara ikiwa ni miongoni mwa visababishi) gharama za keni kati ya Sh. milioni sita na nane.

Awali mgonjwa mmoja alikuwa akigharimu Sh. milioni 30 kwa kutibiwa India.

### Watoto waathiriwa

Tabibu bingwa wa magonjwa ya watoto, Dk Francis Kuria, anasema asilimia 90 ya watumiaji sigara, wanaanza kwa hatua ya kuvutishwa wanapokuwa wadogo.

Dk Kuria anayewakilisha Chama cha Wataalamu wa Magonjwa ya Watoto (PTA), anasema watoto wanavutishwa katika hatua tofauti ikiwa ni pamoja na kupitia kwenye moshi unaotoka kwa mtu anayevuta au mjamzito.

"Mabaki ya moshi unatokana na sigara inayovutwa ndani ya nyumba au magari, yanawaathiri watu wengi wakiwamo watoto... hawafanyi kwa hiari yao, bali wanajikuta kwamba wanavutishwa (sigara) bila kutaka," anasema.

Pia, Dk. Kuria anasema kwa asili, mjamzito ama anapovuta au kuvutishwa sigara, madhara yake yanamfikia mtoto tumboni na hivyo kusababisha madhara, yakiwamo kuzaliwa kabla ya wakati, maarufu 'njiti' au kuwa na uzito mdogo.

"Mtoto anapozaliwa kabla ya wakati wake, moja kwa moja anakabiliwa na hatari nyingi, kubwa zaidi ni uwezekano wa kufa mapema," anasema.

Kwa mujibu wa Dk Kuria, takwimu za uzazi nchini zinaonyesha katika kila watoto 10,000 kati ya milioni mbili wanaozaliwa kwa mwaka katika kipindi cha 2015 hadi mwaka huu, 19 wanakufa wakiwa na umri chini ya siku 28.

Anasema, watoto hao wanapokuwa wakubwa wanakabiliwa na matatizo ya kifya kama shinikizo la damu, uzito wa kupindukia ama kisukari, hivyo katika hatari ya kuugua magonjwa ya moyo.

Pia, anataja athari nyinginezo ni watoto hao kuugua mapafu na pumu.

### Sigara na saratani

Dk John Katanga, kutoka Kitengo cha Kinga katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), anasema kuna ongezeko la wagonjwa anaowahudumia, wakiwamo wanaohusishwa na uvutaji wa sigara ya matumizi ya bidhaa nyingine za tumbaku.

Kwa mujibu wa Dk Katanga, idadi ya wagonjwa wapya wanapokelewa ORCI imeongezeka kutoka 2,500 wa mwaka 2015 kufikia 4,320 kuanzia Januari hadi Oktoba mwaka huu.

Dk Katanga anasema zipo sababu nyingi zinazosababisha saratani, ingawa inayoongoza (duniani) ni ile ya mapafu, ambayo miongoni mwa visababishi vyake ni uvutaji sigara.

Anasema, pamoja na saratani ya mapafu kuhusishwa kwa kiasi na sigara, bidhaa hiyo (sigara) inatajwa pia kuwa chanzo cha ina nyinginezo za saratani kama vile koo, utumbo mpana na shingo ya kizazi.

Dk Katanga anasema, karibu asilimia 32 ya saratani zote, zinaaminika kusababishwa na matumizi ya sigara.

Kama ilivyo kwa wagonjwa wa mapafu, Dk Katanga anasema matibabu ya saratani yanagharimu fedha nyingi, kiasi cha Sh. milioni tano.

Mwandishi wa Habari, David Rwenyagira, aliyeshiriki katika tathimini ya madhara ya tumbaku mkoani Tabora hivi karibuni, anasema pia tumbaku inalimwa katika mazingira na mfumo unaosababisha ukataji miti, hali inayoiingiza nchi katika hatari ya jangwa.

Anatoa mfano, wilayani Ulyankhulu, mkoa wa Tabora, misitu mikubwa nchini iko katika hatari kupotea, chanzo ni kilimo cha tumbaku.

Rwenyagira anasema wanufaika wa kiuchumi kwa tumbaku na bidhaa zinazotokana na zao hilo, wamebuni mbinu zinazowafanya vijana wengi kuvuta sigara.

Anataja matumizi mapya ya sigara za kielektroniki, nazo ni kuwa na athari kubwa kiafya na hata bei.

### Sheria

Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Kudhibiti Tumbaku (TTCF), Lutgard Kagaruki, anasema ipo haja kwa Tanzania kuwa na sheria mpya za tumbaku inayoendana na Mkataba wa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti Tumbaku (WHO-FCTC).

Kagaruki anasema, karibu nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zilizoridhia mkataba huo na kuboresha sheria za tumbaku, hata kufanikiwa kudhibiti kampuni za sigara, hivyo kuwa wadau wazuri kati ya nchi wanachama wa FCTC.

*0754691540*

AFYA

Na Sabato Kasika

TAMKO LA SERIKALI:

# Hii ndiyo hatari, usugu wa vimelea kwa binadamu

KAIMU Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Elias Kwesi, ana maoni kwamba usugu wa vimelea vya magonjwa, ni hatari inayotia shaka dhidi ya nguvu kazi kitaifa, kwa kusababisha vifo na kuongezeka magonjwa sugu dhidi ya dawa zilizopo.

Dk. Kwesi anasema, inasababisha ongezeko la umasikini, kutokana na kuugua muda mrefu, kunakoeandana na gharama kubwa, hali inayoenda hadi kwa mifugo.

Inaelezwa, aina ya dawa na usugu uliopo ndio unawagusa hata wanyama, huku uzalishaji vyakula nao ukibaki hafifu maradufu.

Kutokana na hivyo, wadau wa kiserikali kwa sekta za Afya, Mifugo, Uvuvi, Kilimo na Mazingira, wameanzisha kampeni ya pamoja kuongeza uelewa wa jamii, kuhusu matumizi sahihi na athari za matumizi holela ya dawa kwa binadamu na mifugo.

Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2017 inaonyesha zaidi ya watu 700,000 duniani, wanafariki kila.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, nayo inarejea ripoti hiyo kwa tahadhari hatua isipochukuliwa, kuna hatari kuanzia mwaka 2050, kutakuwapo vifo vya watu milioni 10 kila mwaka, kutokana na usugu wa dawa,.

Serikali inasema mwelekeo wa ripoti ni kwamba, ifikapo mwaka 2050 huenda uchumi wa dunia utashuka kwa asilimia 3.8.

Pia, inataja nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania zitaathirika zaidi na pesa nyingi zitatumika kila mwaka kupambana na usugu wa vimelea dhidi ya dawa hizo.

Kutokana na hali hiyo, serikali inataka hatua madhubuti za kukabiliana na hali hiyo zichukuliwe haraka iwezekanavyo, ili kusaidia kuwaepusha Watanzania kupoteza maisha kwa usugu wa dawa.

Inaelezwa, hatua mojawapo inayochukuliwa na serikali ni kuungana na nchi nyingine duniani, kuhamasisha matumizi sahihi ya antibaiotiki na tayari imezindua Wiki ya Uhamasishaji matumizi hayo, yaliyoanza tarehe 18 mwezi huu.

Maadhimisho ya wiki hiyo, yataedelea hadi tarehe 24 ijayo, ikilenga kusisitiza na kuongeza uelewa wa matumizi sahihi ya dawa, ili kuzuia ongezeko la usugu wa vimelea dhidi ya dawa zilizopo na zijazo.

SERIKALI YATAMKA

Wiki iliyopita, serikali ilitoa tamko wakati wa uzinduzi rasmi wa uhamasisha matumizi sahihi ya dawa za antibaiotiki na kuitaka jamii kuelewa athari na tatizo linaloongezeka duniani.

Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Kwesi, katika uzinduzi rasmi, anaitaka jamii kuelezea athari na tatizo linaloongezeka duniani kote, serikali ikidai hatua madhubuti kukabiliana nayo haraka, kuwaepusha Watanzania na usugu wa dawa .



Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Elias Kwesi (katikati mbele waliokaa), akiwa na wadau wengine wa afya mara baada ya kutoa tamko la serikali.

**“Lengo ni kusisitiza na kuongeza uelewa juu ya matumizi sahihi ya dawa hizi, ili kupunguza matumizi yasiyostahili na hatimaye kuzuia ongezeko la usugu wa vimelea dhidi ya dawa hizi,” anasema Dk. Kwesi.**

“Lengo ni kusisitiza na kuongeza uelewa juu ya matumizi sahihi ya dawa hizi, ili kupunguza matumizi yasiyostahili na hatimaye kuzuia ongezeko la usugu wa vimelea dhidi ya dawa hizi,” anasema Dk. Kwesi.

Akimwakilisha Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, Dk. Kwesi anaitaka jamii kuzingatia matumizi sahihi, pia kinga dhidi ya maambukizi ya mardahi kwa njia zinazozuilika ikiwamo ngono salama, kuosha mikono na chanjo.

Anaagiza vituo vyote vya huduma ya afya, kutekeleza miongozo ya kinga na uzuiaji maambukizi ambayo ni muhimu dhidi ya usugu katika sehemu zao za kazi.

**UTAFITI ULIVYO**

Anasema, tafiti zinaonyesha kugundulika kwa vijuasumu vya kwanza (penicillin) kuliwezesha wagonjwa wa homa ya mapafu na vidonda vya tumbo, kupona na wa kauendelea kuishi kwa asilimia 10 hadi 90 bila kutumia dawa hiyo.

Hata hivyo, anasema kutokana na matumizi mabaya ya dawa hizo kwa binadamu na wanyama, vimelea vya magonjwa ya kuambukiza aina ya bakteria vimejenga usugu.

Anakumbusha njia nzuri na rahisi za kuzuia na kutokomeza usugu wa vimelea dhidi ya dawa hizo, ni wagonjwa na wataalamu wa afya ya binadamu, wanyama na mazingira, kutimiza wajibu wao kwa kuhakikisha usahihi wa dawa kutumika inapohitajika.



Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Elias Kwesi, akitoa tamko la serikali.

**AFYA MOJA**

Dhana 'Afya Moja' inayomanaisha kuwapo uhusiano wa karibu, katika ubora wa afya na kuugua, kati ya binadamu, mnyama na mazingira, ina uhusiano wa moja kwa moja, hivyo mbinu za kukabiliana na athari kimazingira.

Inaelezwa, namna ya kuikabili inahusisha sekta husika za afya ya binadamu, wanyama, mimea na mazingira inayowazunguka na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kati ya magonjwa 10 ya kuambukiza za anayopata mwanadamu, sita husambaa kutoka kwa wanyama

Hivyo, katika kukabiliana na tatizo la usugu wa vimelea dhidi ya dawa, dhana ya afya moja inatumika kuikabili kwa umoja wa sekta zinazomhusu kibinadamu, mifugo, kilimo na mazingira.

Pia, serikali inataja mashirika yaliyo chini ya umoja wa mataifa, yakiwamo Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) na Shirika la Afya ya Wanyama (OIE) na sasa inatajwa Shirika la Mazingira Duniani nalo limeungana katika vita hivyo.

AFYA

# Profesa Museru atangaza mageuzi makubwa Muhimbili ya sasa, ijayo

## • Tiba figo nyumbani yaokoa bilioni kadhaa

**Na Yasmine Protace**

HISTORIA inaonyesha kabla ya kuwapo tiba ya figo nchini, wagonjwa wengi walilazimika kwenda nje ya nchi kupata matibabu.

Lakini, katika hatua za kuokoa gharama kubwa ya fedha kutumika, pia kuwafikia wagonjwa wengi, serikali imefanikiwa kuanzisha huduma hizo nchini na kupunguza matumizi ya fedha kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi..

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Profesa Lawrence Museru, anasema hadi sasa kuna wagonjwa 51 waliopandikizwa figo tangu kuanzishwa huduma hiyo, ikiigharimu serikali Sh. bilioni 1.53, wastani wa Sh. milioni 30 kwa mgonjwa mmoja.

Profesa Museru anaitaja kuwa ni mafanikio, akifanya ulinganishi kwamba iwapo wagonjwa hao wangepelekwa nje ya nchi ingeigharimu serikali Sh.bilioni 6.12, kwa wastani wa Sh. milioni 120 kwa kila mgonjwa mmoja wa figo.

Anasema, ni hatua inayoisaidia serikali kuokoa fedha Sh. bilioni 4.590, pia kwa kila mtu wastani wa Sh. milioni 90.

"Ndani ya miaka miwili upandikizaji figo wafikia asilimia 34," anasema Profesa Museru na kuongeza kuwa serikali ilisafirisha wagonjwa 150 nje ya nchi katika kipindi cha miaka 15 hadi mwishoni mwa 2015, ambayo ni wastani wa wagonjwa 10 kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Profesa Museru, kwa sasa wamefikia wagonjwa 34 pekee waliopelekwa nje ya nchi kwa kipindi cha miaka minne

Kuhusu idadi ya wagonjwa 558 waliopatiwa huduma za kibingwa za mionzi (radiolojia), kati yao 274 walikuwa na uvimbe wa kinywa na jumla ya gharama zao ni Sh. bilioni 2.192 sawa na Sh.milioni nane kwa kila mgonjwa.

"Kama wangeenda nje ya nchi ingeigharimu serikali kiasi cha Sh. bilioni 26.3 sawa na Sh. milioni 96 kwa mgonjwa mmoja kwa safari nne zinazohitajika kukamilisha mzunguko wa matibabu," anasema Profesa Museru na kufafanua: "Serikali imeokoa Sh. bilioni 24.112 kutoa huduma hizi nchini."

Mkurugenzi huyo anasema, Hospitali ya Muhimbili, imefanikiwa kuanzisha na kuboresha huduma za uchunguzi kwa wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa chakula na ini na kuna wagonjwa 380 waliopatiwa huduma kwa gharama ya Sh. 116,820,000.

Anataja gharama za mbadala, iwapo wangeenda kutibiwa nje ya nchi ni Sh. 1,514,270,000, hivyo hospitali imeokoa Sh.397,450,000.

**MABORESHO VYUMBA**

Profesa Museru anazungumzia vyumba vya upasuaji vimeongezeka hadi kufikia 20, ili kuendana na ongezeko la wagonjwa na huduma mpya zilizoanzishwa.

Anasema, hospitali ilikarabati na kuongeza vyumba vya upasuaji kutoka 13 hadi 20; viwili ni maalumu kwa upasuaji wa watoto na wagonjwa wanaohitaji kupandikizwa figo.

Anasema, hospitali imepunguza msongamano wa wagonjwa kusubiri tarehe ya mbali ili kufanyiwa upasuaji. Jumla ya Sh. bilioni 2.46 zilitumika kufanya kazi hiyo

Profesa Museru, anataja maeneo husika ni ya vyumba vya wagonjwa wenye kuhitaji uangalizi maalumu (ICU), vimeongezwa kutoka vitanda 25 hadi 78, vikiwa na nyongeza ya vifaa tiba.

Mkurugenzi Mtendaji huyo wa MNH, anataja vyumba na nyongeza ya vifaa vya waohitaji ungalizi maalum (ICU) katika makundi yafuatayo na idadi ya vitanda walivyopewa: Chumba cha watoto wachanga,10; Watoto kuanzia mwezi mmoja, 12; wagonjwa wa kawaida, 15; wagonjwa wa upasuaji; wagonjwa wanaopandikizwa figo, vitano; na kinamama wajawazito, 10.

Anasema mfumo wa hewa ya oksijeni wodini umefanyiwa ukarabati mkubwa katika wodi sita za jengo la Mwaisela, zikiwekewa mfumo wa oksijeni na vitanda 28 vya kwa ajili ya wagonjwa maalumu (HDU).

Profesa Museru, anafafanua kwamba, hospitali imekarabati na kuongeza mashine za kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo, kutoka 17 hadi 42, hivyo inaongeza uwezo wa kuhudumia wagonjwa kutoka 70 wa awali, hadi 168 kwa siku.

**UJENZI MPYA**

Pia, anasema kumejengwa barabara za lami ndani ya hospitali kwa gharama ya Sh. bilioni. 1.5, huku mipango iliyopo ni kuwapo jengo jipya la ghorofa tatu kwa ajili ya wagonjwa binafsi (IPPM).

Anasema muundo wake, litakuwa na vyumba 20 vya kulala mgonjwa; vyumba 20 vya wagonjwa wawili wawili; vitano vya kulaza watu mashuhuri (VIP) na chumba kimoja cha kulaza viongozi wa kitaifa (Presidential suite).

"Jengo hilo litakuwa na ICU yenye vitanda 10, wodi ya kinamama kujifungua, vitanda 10, wodi maalumu ya watoto wachanga vitanda 10, vyumba viwili vya upasuaji, vyumba vitano vya madaktari," anasema.

Mkuu huyo wa Muhimbili, anataja huduma nyinginezo zinazitarajiwa katika jingo jipya la kisada zaidi ni vyumba vitatu vya utengamao, maabara ndogo, vyumba vya 'Ultrasound' na huduma kama za mionzi ya X-Ray na tiba ya radiolojia

Anataja mipango mingine ni kujengwa Kituo cha Umahiri Upandikizaji Viungo, ili kuhakikisha huduma zilizoanzishwa zinatolewa katika mfumo endelevu.

Kwa mujibu wa Profesa Museru, huduma tarajiwa mbali na kuwapo maabara ya kujifunzia, pia zinahusu upandikaji katika maeneo ya: Figo, vifaa vya kusaidia kusikia; mimba, ini na uloto (bone marrow transplant)



Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Lawrence Museru. **PICHA: MAKTABA**

> **"Kama wangeenda nje ya nchi ingeigharimu serikali kiasi cha Sh. bilioni 26.3 sawa na Sh. milioni 96 kwa mgonjwa mmoja kwa safari nne zinazohitajika kukamilisha mzunguko wa matibabu," anasema Profesa Museru na kufafanua: "Serikali imeokoa Sh. bilioni 24.112 kutoa huduma hizi nchini."**

> **"Jengo hilo litakuwa na ICU yenye vitanda 10, wodi ya kinamama kujifungua, vitanda 10, wodi maalumu ya watoto wachanga vitanda 10, vyumba viwili vya upasuaji, vyumba vitano vya madaktari," anasema.**



# Wawili wafa, tisa wajeruhiwa wakihamia Malawi kinyemela

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wawili wanaodaiwa kuwa wahamiaji haramu kutoka Ethiopia, wamefariki dunia na wengine tisa kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kinyemela kwenda Malawi, kuanguka kwenye mteremko wa Namba One wilayani Rungwe mkoani Mbeya.

Akizungumza na wandishi wa habari katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe ya Makandana walipolazwa majeruhi wa ajali hiyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alidai tukio hilo lilitokea Novemba 18, mwaka huu majira ya saa 1:30 asubuhi.

Alilitaja gari walilokuwa wanasafiria watu hao kuwa ni lenye namba za usajiri CA 6439 na tela lenye namba BK 4744 aina ya Genlyon, mali ya Kampuni ya Almeida ya Malawi, akidai kuwa lilikuwa linakwenda mjini Lilongwe.

Kamanda Matei alidai watu hao walikuwa wamejificha chini ya gari hilo kwa kulala juu ya mbao ambazo walikuwa wamezitandika chini ili wasionekane na waliingia nchini wakitokea Nairobi, Kenya.

Alidai kuwa baada ya gari hilo kuanguka, askari wa kikosi cha usalama barabarani kutoka wilayani Rungwe, walifika eneo la tukio ili kuokoa na ndipo walipokuta watu hao wakiwa chini na baadhi yao wakiwa wamekufa na wengine wakiwa wamejeruhiwa.

"Gari hilo lilikuwa limebeba sabuni za unga na ni aina ya Transit (magari yanayosafirisha mizigo ya kimataifa), haya ni miongoni mwa magari ambayo sheria haziturhusu Jeshi la Polisi kuyasimamisha barabarani na kuyakagua, hivyo wametumia mwanya huo kuyatumia," Kamanda Matei alisema.

Alidai majeruhi wote wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Makandana na Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa tukio ili hatua zingine zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Kamanda Matei alidai kuwa endapo gari hilo lisingepata ajali katika eneo hilo, kulikuwa na uwezekano mkubwa wahamiaji hao kuvuka mipaka ya nchi na kuingia Malawi na hatimaye katika mataifa mengine ya kusini mwa Afrika, hasa Afrika Kusini ambako wahamiaji haramu wengi wanakimbilia.

Aliwataka madereva wa magari hayo kuwa waaminifu na kuzingatia sheria za usafirishaji wa mizigo ili kuepuka kufanya makosa kama hayo.

Wahamiaji haramu kutoka Ethiopia wamekuwa wakiitumia Tanzania kama njia kuu ya kuingia katika mataifa ya Kusini mwa Afrika kwa ajili ya kusaka maisha bora na wamekuwa wakitumia njia tofauti za kuvuka mipaka ya Tanzania ili kukwepa kunaswa.


Distributed via ippmedia

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), pamoja na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa huo, wakiwajulia hali wahamiaji haramu raia wa Ethiopia waliolazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe Makandana, baada ya kupata ajali ya gari walipokuwa wanasafiri kinyemela kuingia nchini Malawi juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC ampa siku 5 mkurugenzi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ametoa siku tano kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba, kuhakikisha anatoa kibali cha kupata ardhi kwa mwekezaji anayetaka kujenga kiwanda cha kuzalisha mbegu za mazao.

Inadaiwa mwekezaji huyo ambaye ni kampuni ya kuzalisha mbegu ya Seed Co LTD, amefuatilia kwa muda mrefu kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji huo na mkurugenzi amekuwa sehemu ya vikwazo.

Akizungumza wakati anakagua ujenzi wa kiwanda kipya cha kusindika maziwa kinachojengwa na Kampuni ya Asas LTD wilayani Rungwe, Chalamila alisema alilazimika kutoa agizo hilo kwa mkurugenzi baada ya kubaini mwekezaji huyo anakusudia kuhamisha mradi huo.

Alisema miradi mingi katika Mkoa wa Mbeya inakwama kutokana na watendaji kuwa na urasimu mwingi na kuwa wapokea rushwa, akiwataka kuacha mara moja tabia hizo kwa kuwa ni hatari kwa maendeleo.

"Mwekezaji alitaka aende akawekeze kwingine ambako hakuna urasimu, sasa nimetoa siku tano kwa Mkurugenzi wa Wilaya ya Mbeya kutoa 'invoice' ili mwekezaji alipe malipo kidogo na afunge kiwanda kikubwa," alisema.

Aliwatahadharisha watumishi wa umma katika mkoa huo kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atayeweka mazingira magumu kwa wawekezaji.

Chalamila aliipongeza Kampuni ya Asas kwa kuwekeza katika Wilaya ya Rungwe kwa kuwa kiwanda hicho kitasaidia kuboresha soko la maziwa ya wananchi wa wilaya hiyo na kuiingizia serikali mapato.

Meneja wa Kiwanda cha Asas wilayani Rungwe, Lipita Mtimila, alisema kiwanda hicho kinatarajiwa kukamilika na kuanza kazi ya kusindika maziwa hivi karibuni.

Alisema kutokana na kasi waliyonayo kwenye ujenzi huo, wana uhakika mpaka kufikia Juni mwakani, kitakuwa kinafanya kazi kwa asilimia 100. Ujenzi ulianza miezi saba iliyopita. "Uwekezaji wetu hapa unakadiriwa kuwa unafikia Sh. bilioni tatu kuanzia ujenzi wa majengo mpaka mtambo wenyewe. Kwa hiyo, ni uwekezaji mkubwa ambao tunaamini utakuwa na manufaa makubwa kwetu na kwa wananchi wa wilaya hii," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Ezekiel Mwankota, alisema wanachohitaji wananchi ni kuona maziwa wanayozalisha yanaongezwa thamani ndani ya wilaya yao.

Alisema kukamilika kwa kiwanda hicho kutatoa nafasi kwa wananchi kuongeza thamani ya maziwa yao na kuwa na soko la uhakika.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alisema Halmashauri ya wilaya hiyo inazalisha maziwa zaidi ya lita milioni 62 kwa mwaka, lakini kati yake ni asilimia 11 pekee inayouzwa katika mfumo rasmi wa soko.

Alisema kiwango kingine kinauzwa kwa njia za panya, hali ambayo inaipotezea halmashauri mapato, hivyo kiwanda hicho kitasaidia kuokoa fedha zinazopotea.

# 'Ukatili huzaa ukatili'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii vinavyomea nchini, vinatokana na ukatili wa kisaikolojia wanaofanyiwa watoto na wazazi wao kwa kuwashuhudia wakitekeleza vitendo na baadaye na wao kuvifanya wakidhani ni vya kawaida.

Hayo yalisema juzi na Ispekta wa Polisi, Mary Gumbo kutoka Dawati la Jinsia alipozungumza na wandishi wa habari kuhusu maandalizi ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kuanzia Novemba 25, mwaka huu.

Alisema mara nyingi watoto wanaposhuhudia matukio ya ukatili yakifanywa na wazazi ama na watu wazima, huwa wanakariri na kuja kuyatekeleza wakishakuwa wakubwa.

"Kwa mfano, mtoto anaposhuhudia baba akimpiga mama kila siku, yeye anaona kama ni kitu cha kawaida na anakariri kiasi kwamba siku akiwa na mke, na yeye anafanya hivyo akijua ni kitu cha kawaida, tunaendelea kutoa elimu kwa jamii ili kukomesha hali hii," alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa wanaendelea na utoaji wa elimu katika maeneo mbalimbali, yakiwamo ya shule na mikutano ya hadhara inayoitishwa na viongozi wa vijiji na mitaa.

Alisema matukio yote ya ukatili, yakiwamo ya kubakwa kwa watoto, kulawitiwa na wizi wa watoto huanzia kwenye ukatili wa kisaikolojia ambao alidai ndiyo chanzo cha aina zote za ukatili.

Alisema kuna haja wazazi kuepuka kupigana mbele ya watoto wao kwa maelezo kuwa vitendo hivyo vinavyoathiri watoto kisaikolojia na kusababisha matukio ya ukatili kuendelea kushamiri katika jamii.

Alisema kwa sasa, makosa ya ukatili yanayoongoza kufanyika katika jamii ni kutelekeza familia, ubakaji hasa kwa watoto na ulawiti.





# Magufuli kutikisa Dodoma siku tano

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS John Magufuli leo anatarajiwa kuanza ziara ya kikazi ya siku tano mkoani Dodoma, kukagua miradi miradi mbalimbali ya maendeleo.

Imeelezwa kuwa katika ziara yake hiyo, Rais Magufuli pia anatarajiwa kutunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa (Honoris Causa) na Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) kutokana na jitihada zake za kuleta maendeleo nchini.

Akizungumza na waandishi jana, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema Rais ataanza ziara hiyo leo hadi Novemba 25, mwaka huu kwa kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na jiji hilo jipya.

Alitaja shughuli zitakazofanyika katika ziara hiyo kuwa ni pamoja na mahafali ya 10 ya Udom ambayo Rais Magufuli atakuwa mgeni rasmi, kuweka jiwe la msingi kwenye miradi ya Hospitali ya Uhuru, ujenzi wa nyumba 118 za askari polisi katika maeneo ya FFU Nzuguni na Medeli East.

"Pia, jiwe la msingi litawekwa kwenye mradi wa ujenzi wa stendi kuu ya mabasi iliyoko Nzuguni na soko kuu linalojengwa katika eneo la Nzuguni.

"Mheshimwa Rais pia atazungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara utakaofanyika katika stendi ya mabasi Nzuguni," alisema.

Aliongeza kuwa Rais ataweka jiwe la msingi kwenye miradi ya ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la Wananchi Tanzania Kikombo, ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji na Ujenzi wa jengo la makandarasi katika eneo la National Capital City.

Alisema maandalizi yote yamekamilika na kutoa wito kwa wananchi kujitokeza kwenye mikutano itakayofanywa na Rais atakapotembelea miradi hiyo.

"Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa upendeleo anaotupatia daima.

"Ziara hii ya Rais kwetu ni fursa ya kumwonyesha hatua tulizofikia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo aliyotupatia na kupokea maelekezo ya namna ya kusonga mbele kwa uhakika katika hatua mbalimbali za utekelezaji wake," alisema.

Makamu Mkuu wa Udom, Prof. Faustine Bee, alisema watamtunuku Rais Magufuli shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa kutokana na jitihada za kuleta maendeleo anazozifanya nchini, hasa katika sekta ya ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuwekeza katika elimu, miundombinu, mawasiliano na kuimarisha utawala bora.

Alisema serikali ya awamu ya tano imekuwa mstari wa mbele katika kupambana na rushwa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

"Shahada hii inatolewa baada ya Baraza la Chuo na Seneta kuridhika na mambo muhimu ya kimaendeleo anayofanya nchini na ndani ya miaka 10 katika chuo hiki waliowahi kukabidhiwa ni Dk. Jakaya Kikwete na Dk. Rashid Kawawa, hii shahada hutolewa kwa mtu aliyefanya vizuri katika nyanja mbalimbali," alisema.


Distributed via ippmedia

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini humo jana, kuhusiana na ziara ya kikazi ya Rais John Pombe Magufuli, kutembelea miradi ya maendeleo mkoani humo inayotarajia kuanza leo. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobas Katambi na Katibu Tawala wa mkoa huo, Kessy Maduka. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Udom wataka mitaala ya elimu ibadilishwe

**Na Renatha Msungu, D**ODOMA

CHUO Kikuu cha Dodoma (Udom) kimeishauri serikali kuangalia namna ya kubadilisha mitaala ya elimu ya juu ili mhitimu ajiajiri mwenyewe badala ya kusubiri kuajiriwa.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Utafiti, Machapisho na Ushauri kwa jamii wa chuo hicho, Dk. Ambrose Kessy, wakati wa kongamano la wanazuoni chuoni huko.

Alisema vyuo vinapaswa kubadilisha mitaala ili kuendana na soko la ajira lililopo kwa sasa.

"Kuna baadhi ya vyuo vya serikali na binafsi vinatumia mitaala tofauti ambayo haiendani na soko la ajira, jambo hili ni chanzo cha ukosefu wa ajira, unakuta mwanafunzi anahitaji kujua kitu fulani, lakini anashindwa kutokana na ule mtaala hauna," alisema.

Alisema mitaala ya sasa inapaswa kuendana na soko la kiuchumi, kisiasa na kibiashara ili mwanafunzi akihitimu chuo kikuu, apate fursa ya kujiajiri mwenyewe na si kutegemea ajira serikalini.

"Kongamano kama hili kuna umuhimu mkubwa wa kuibua fursa za kijamii, kiuchumi na maendeleo kwa jamii kwa walengwa," alisema.

Mhadhiri wa Udom, Dk. Paul Loisulie, alisema makongamano ya wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu yanapaswa kuwapo kwa kuwa yana faida kubwa kwa washikiri kupata uelewa wa mada zinazoibuliwa.

Alisema mijadala hiyo inapaswa kuendelea kwa kuwa inajenga ili kusaidia kuibua mada za kimaendeleo ambazo zitawasaidia wanafunzi kupiga hatua katika elimu.

Kaimu Mkurugenzi mashirikiano ya taasisi wa chuo hicho, Dk. Happiness Nnko, alisema kuna haja kuboreshwa vitengo vya elimu kwa awamu kwa kuhakikisha vinakuwa na vifaa vyote vinavyohitajika kwa mwanafunzi.

Alisema kitengo cha sayansi kinapaswa kuboreshwa ili kuwa na vifaa vya kutosha ili wanafunzi wafanye mafunzo kwa vitendo.

Rais wa Jukwaa la Wahitimu Udom, Prof. Leonard James, alisema jitihada za serikali zinapaswa kuelekezwa katika ufundishaji ili kuendana na mitaala ya soko la ajira ulimwenguni.

# Amwomba JPM nafasi tatu wabunge wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** MPWAPWA

MWALIMU Mkuu mstaafu wa Shule ya Msingi Buigiri ambayo ni maalum kwa wasioona iliyoko wilayani Chamwino mkoani Dodoma, Slyevavus Hosea, amemshauri Rais John Magufuli kutoa nafasi tatu kwa walemavu kati ya 10 katika uteuzi wa wabunge.

Alitoa ushauri huo jana alipozungumza na waandishi habari wilayani Mpwapwa, akieleza kufurahishwa na uwapo wa wabunge wenye ulemavu bungeni.

Hata hivyo, mstaafu huyo alisema bado kuna uwakilishi mdogo wa kundi hilo katika chombo hicho cha kutunga sheria, akitolea mfano kutokuwa na wabunge wenye ulemavu wa macho na masikio.

Alisema ikimpendeza, Rais Magufuli katika uongozi wake, alikumbuke zaidi kundi hilo kwa kuteua wabunge wenye ulemavu huo.

Mwalimu Hosea alisema licha ya kuwapo wabunge wenye ulemavu bungeni na kupata nyadhifa mbalimbali, hawatokani na vyama vya watu wenye ulemavu.

Alisema nafasi za uwakilishi zikipatikana kwa ngazi zote za uamuzi, watu wenye ulemavu wataonyesha uwezo wao na kuaminika katika jamii kwa utendaji wao wa kazi.

Alisema bado jamii haijawa na uelewa wa kuwaamini watu wenye ulemavu licha ya kuwa jamii hiyo ya watu wenye ulemavu kuwa na uwezo wa kufanya kazi vizuri zaidi ya watu ambao wanaonekana kuwa na viungo vyote.

"Nina uhakika kama jamii ya watu wenye ulemavu itatambuliwa kikatiba na kuwa wabunge wanatakiwa kupatikana kutokana na vyama vyao vya watu wenye ulemavu, watafanya kazi nzuri katika jamii," alisema.

Mstaafu huyo hakuwa nyuma kupongeza hatua ya serikali kutambua umuhimu wa watu wenye ulemavu kwa kuwateua katika nafasi mbalimbali za kiutendaji.





## Dk. Shein akunwa kasi Ujenzi wa barabara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameeleza kuridhishwa na kasi kubwa inayoendelea ya ujenzi wa barabara ya Bububu-Mahonda hadi Mkokotoni.

Dk. Shein aliyasema hayo kwa nyakati tofauti alipokutana na kufanya mazungumzo na wazee wa Wilaya ya Kaskazini "A" katika ukumbi wa Chuo cha Amali Mkokotoni Wilaya ya Kaskazini Unguja.

Rais Dk. Shein aliwaleza wazee hao wa CCM pamoja na viongozi wengine wa chama hicho kuwa kutokana na kasi hiyo kubwa ya ujenzi wa barabara hiyo yenye kilomita za mraba 31 ana matarajio makubwa ya kuzinduliwa barabara hiyo katika sherehe za Mapinduzi zijazo.

Dk. Shein alieleza kushangazwa na kasi kubwa ya mkandarasi wa barabara hiyo, na kusisitiza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuwasogezea huduma muhimu za kimaendeleo wananchi wake wote wa mjini na vijijini kwani hilo ndio lengo la Mapinduzi ya Januari 12, 1964. Alieleza haja kwa wazee kuwaeleza vijana juu ya heshima ya wazee na vipi wazee wanatakiwa kuenziwa na kutunzwa sambamba na kupewa heshima yao kutokana na mambo makubwa waliyoyafanya.

Aliongeza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamini na inazijali juhudi za wazee walizochukua hadi kupelekea kupatikana uhuru.

Dk. Shein alisema kuwa wazee ndio walioleta ukombozi na kuwakomboa wanyonge, hivyo ni vyema wakaendelea kuthaminiwa.

Aidha, alieleza kuvutiwa na taarifa ya wazee hao wa Kaskazini "A" na kuahidi kuwa ahadi zote alizoziahidi katika Wilaya hiyo atazitekeleza na kuzifanyia kazi kabla ya kumaliza muda wake wa uongozi.

Nae Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdalla Juma Mabodi, alisema kuwa CCM inathamini uwapo wa wazee na kueleza kuwa Serikali zote mbili zimeeleza jinsi zitakavyowajali.



Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud (katikati waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na washirika wa maendeleo ikiwamo UN Women, walipomtembelea ofisini kwake, Tunguu, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanawake wapigiwa debe kwenye uongozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amesema kunahitajika kuongeza idadi ya wanawake katika ngazi za maamuzi ili kuwa na usawa wa kijinsia katika vyombo hivyo.

Akizungumza na ujumbe wa mashirika ya maendeleo kikiwamo kitengo cha wanawake cha shirika la umoja wa mataifa (UN WOMEN), ofisini kwake, alisema bado uwiano wa usawa wa kijinsia katika vyombo hivyo haujawa wa kuridhisha.

Aliwataka wanaume kuwa mabalozi wazuri wa kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi kwani idadi ya wanawake viongozi katika nafasi za juu ni ndogo ikilinganishwa na wanaume.

"Mkoa wa Kusini Unguja kuna majimbo matano ya uchaguzi, lakini majimbo yote hayo nafasi za uwakilishi na ubunge zimeshikiliwa na wanaume pekee," alisema.

Aidha, Mkuu wa Mkoa huyo aliwataka wanawake kuacha kutegemea viti maalum pekee na badala yake kuingia majimboni kugombea nafasi za uongozi.

Hata hivyo, alivitaka vyama vya siasa kiwe na asilimia 50 ya wagombea wanawake katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ili kuwa na uwiano sawa wa uongozi.

"Wanawake ni waadilifu,waaminifu na wachapa kazi hebu tuwape nafasi za uongozi badala ya kuwapa viti maalum pekee," alisema.

Naye Ofisa mwandamizi wa UN WOMEN nchini, Eurasmina Massawe, alivitaka vyama vya siasa kuzingatia masharti ya mabadiliko ya sheria ya vyama vya siasa inavyovitaka kuzingatia usawa wa kijinsia katika nafasi za uongozi.

Alisema katika marekebisho hayo viongozi wa vyama vya siasa wanatakiwa kuzingatia usawa wa kijinsia katika kuendesha vyama ili kuleta mabadiliko makubwa na kuweapo uwiyano wa uongozi.

Alisema marekebisho hayo ni muhimu kwa sababu imebainika baadhi ya vyama vya siasa vimetawaliwa na mfumo dume na nafasi zote za juu za uongozi zimeshikiliwa na wanaume.

"Wakati umefika sasa kwa vyama vya siasa kutekeleza kwa vitendo marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa na kuvitaka kuweka usawa wa kijinsia kwa kutoa nafasi kwa wanawake kushika uongozi," alisema.

Mjumbe wa timu ya wanaume ya kuleta mabadiliko kwa wanawake kushika nafasi za uongozi, Mwalimu Zimba Ali, alisema vipo baadhi ya vyama vya siasa havina mfumo mzuri unaofahamika ambao unaonesha nafasi ya mwanamke kufikia malengo ya kisiasa.

"Tunaviomba vyama vya siasa viimarishe jumuiya za wanawake ambazo zitatoa nafasi nzuri kwa wanawake kufikia malengo ya kisiasa ya uongozi," alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) Zanzibae, Asha Abdi, alisema wanawake wengi wameonyesha nia ya kujitokeza kuwania nafasi za uongozi kuelekea uchaguzi mkuu baada ya kupata elimu na mafunzo ya uongozi.

"Wanawake wengi wameonyesha nia ya kuwania nafasi za uongozi kuelekea uchaguzi mkuu... tunaviomba vyama vya siasa kuweka mazingira mazuri yatakayotoa nafasi kwa wanawake kufikia dhamira ya kisiasa," alisema Abdi.

Ujumbe wa UN WOMEN upo Zanzibar kuangalia utekelezaji wa baadhi ya miradi inayofadhili na taasisi hiyo kwa asasi za kiraia na jumuiya zake.

Miongoni mwa asasi za kiraia zinazofaidika na ufadhili wa UN WOMEN ni Tamwa inayotekeleza mradi wa wanawake kufikia malengo ya uongozi pamoja na Jumuiya ya Wanawake ya Baraza la Wawakilishi (UWAWAZA).

# SMZ yaeleza fursa kilimo cha viungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema wakati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiendelea na mipango yake ya kuimarisha viwanda vidogo na vya kati, wananchi wanapaswa kuchangamkia fursa zilizojitokeza katika kilimo cha viungo ambacho bei yake imepanda kimataifa.

Alisema wakati umefika kwa rasilimali za Taifa zinazozalishwa nchini zitumike kwa usimamizi wa wataalamu wazalendo kutengeneza bidhaa kupitia viungo wanavyozalisha ili ziifaidishe jamii kiustawi na kuongeza mapato ya Taifa kwa ujumla.

Balozi Iddi alieleza hayo kisiwani Pemba wakati akikagua miradi ya maendeleo akianzia na shamba la Kiwanda cha Mafuta ya Makonyo Mtakata pamoja na kufahamu changamoto zinazokwaza ukamilishaji wa miradi hiyo muhimu kwa ustawi wa wananchi walio wengi.

Balozi Seif alisema hakuna sababu kwa Wananchi na hasa wakulima kulalamikia ajira wakati Serikali imeshaweka mazingira mazuri ya mfumo wa upatikanaji wa fursa za kujiendeleza kimaisha bila ya kusubiri ajira za Serikali ambazo zimepungua sana.

Alimpongeza Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Balozi Amina Salum Ali, kwa ushawishi wake mkubwa wa kusimamia ufufuaji wa viwanda vilivyosimamisha uzalishaji na kuanzisha vipya.

Alisema jitihada za hizo zimeitia moyo Serikali katika azma yake ya kuelekea kwenye uchumi wa viwanda ifikapo 2025 ambao utasaidia kuongeza fursa za ajira na kupunguza umaskini kwa wananchi. Balozi Amina alisema Wizara hiyo kupitia Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar {ZSTC}, inafanya mabadiliko makubwa kwenye viwanda vyake ili vizalishe kwa kiwango na Tija.

Balozi Amina alisema hatua hiyo imechukuliwa baada ya kuzingatia ongezeko la bei kubwa kwa bidhaa zinazotokana na viungo akitolea mfano kilimo cha mikaratusi, mchaichai, mrehani na mdalasini.

Awali, Balozi Iddi alikagua barabara inayoendelea kujengwa ya Gombani kupitia Pagali hadi Pondeani itakayojengwa kwa kiwango cha lami, kuangalia maendeleo ya ujenzi wa nyumba ya makazi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar hapo Pagali.

# Bil. 1/- za korosho zawatia matatani

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoani Mtwara, inawashikilia viongozi 50 wa vyama vya Ushirika AMCOS) kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za wakulima wa korosho za msimu wa mwaka 2016/ 2017 zaidi ya Sh. bilioni moja.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mtwara, Enock Ngairo kwa wanahabari mjini Mtwara.

Alisema Taasisi hiyo inawashikilia viongozi hao wa vyama mbalimbali vya msingi kutoka wilaya zote za Mkoa wa Mtwara, baada ya kuchunguzwa na kubainika na makosa ya kuwaibia wakulima.

Ngairo alisema viongozi hao wamebainika kufanya ubadhirifu wa fedha za korosho za wakulima kwa msimu wa mwaka 2016 / 2017, na kwamba waliziiba fedha hizo kwa kutumia njia mbalimbali.

Alisema njia waliyotumia kuwaibia wakulima fedha zao ni kuwadanganya kuwa fedha zao hazijafika, huku zikiwa zimefika lakini viongozi hao walizitumia kwa manufaa yao.

Ngairo alisema Takukuru imefanya uchunguzi wa kina na kujiridhisha na kuamua kuwakamata watuhumiwa ili taratibu za kisheria zifanyike sambamba na viongozi hao kurejesha fedha hizo. Alisema Raisi John Magufuli alishatoa agizo la kutaka viongozi wote wa vyama vya msingi ambao wamewadhulumu wakulima fedha za korosho kukamatwa na kurejesha fedha hizo, hivyo Takukuru inatekeleza agizo hilo.

Ngairo alisema viongozi hao licha ya kufikishwa katika vyombo vya sheria ikiwamo mahakamani, pia lazima warejeshe fedha na wakulima wapate haki yao. Alisema miongoni mwa viongozi hao 50 wa vyama vya msingi, zaidi ya viongozi 20 walioakamatwa ni kutoka Wilaya ya Newala. Aidha, Ngairo alitoa wito kwa viongozi wa Amcos wote Mkoa wa Mtwara kuwa waadilifu wa fedha za wakulima, na kuacha tabia ya vitendo vya rushwa kupitia malipo ya korosho za wakulima.

Alisema Takukuru haitamfumbia macho mtu yeyote ambaye anajihusisha na vitendo vya kupokea na kutoa rushwa hasa katika msimu huu wa korosho ili kumdhulumu mkulima.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula (kushoto), akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Siriel Mchembe, wakitembelea Hifadhi ya Msitu wa Ukaguru wilayani humo, mkoani Morogoro, juzi. Mabula alikwenda kukagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi na nyumba za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) jana. **PICHA: WANMM**

## Wanakijiji wapata fursa ya umeme

**Na Futuna Selemani,** CHALINZE

NAIBU Waziri wa Nishati Subira Mgalu, amewasha umeme katika kijiji cha Mwindu, Kata ya Ubena, Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani na kusema vijiji vilivyosalia ambavyo bado havijapata umeme vimewekwa kwenye mpango wa REA Awamu ya tatu mzunguko wa pili.

Mzunguko huo unatarajiwa kuanza mapema mwakani na kazi itakayobaki ni kuunganisha kwenye vitongoji.

Tukio la kuwasha umeme limefanyika wakati akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani Pwani kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme pamoja na kuzungumza na wananchi.

Akizungumza na wanakijiji hao Mgalu alisema Mkoa wa Pwani ni miongoni mwa mikoa ambayo itafaidika na mradi wa ujazilizi awamu ya pili ambao unatarajiwa kuanza Desemba mwaka huu.

Aidha, alisema Kata ya Ubena iliyopo kwenye kijiji hicho ilifaidika na mradi wa ujazilizi awamu ya kwanza uliokamilika mwaka jana ambapo maeneo mengi muhimu ya huduma za jamii ziliunganishwa na mradi huo.

Alimpongeza mkandarasi kwa kazi nzuri anayoifanya na alimwambia aendelea na kazi ya kuunganishia umeme wateja waliolipa.

Meneja wa Tanesco Wilaya ya Chalinze, Patric Mtukananje, alisema Kijiji cha Mwindu ni miongoni mwa vijiji 19 ambavyo vipo kwenye mpango wa kupelekewa umeme kupitia mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza katika Wilaya ya chalinze.

Alifafanua jumla ya wateja waliokwisha kuunganishwa chini ya mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza ni 536, na bado wateja zaidi wanaendelea kujitokeza kuomba kuunganishwa, huku mkandarasi akiendelea na kazi hiyo na kadirio lililokuwa ni kuunganisha wateja 477.

# Mbarawa ajitosa kero maji Meatu

**Na Happy Severine,** MEATU

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ameagiza kusafishwa kwa bwawa la Mwanyahima lililopo wilayani Meatu mkoani Simiyu ambalo ni chanzo kikuu cha maji, baada ya bwawa hilo kujaa tope na kusababisha wananchi wa mji wa Mwahnuzi kukosa maji kwa zaidi ya siku 20.

Prof. bwarawa alitoa agizo hilo wakati wa ziara yake ya siku moja kukagua vyanzo vya maji vilivyomo na kujionea hali halisi ya tatizo la maji linalowatesa wananchi wilayani humo. Alisema serikali imesikia malalamiko mengi ya wananchi juu ya tatizo la maji na kwamba wameshatoa maboza matatu ya lita 1,800 yatakayosaidia kupunguza makali ya upatikanaji wa maji kwa kubeba na kusambaza maji kutoka kisima kidogo kilichopo karibu na mto Semu uliopo katika kijiji cha Mwagwila .

Alieleza wakati wananchi wakiwa katika kipindi kigumu cha mpito cha upatikanaji wa maji, mamlaka husika inatakiwa kulitatua tatizo hilo kwa haraka kwa kuanza kusafisha bwawa hilo pamoja na uchimbaji wa visima vingine 10 vilivyopo eneo la mto Semu na kujenga mtandao wa bomba kutoka eneo hilo mpaka mjini Mwanhuzi.

Waziri Mbarawa aliongeza kuwa kabla hawajaanza kuchimba visima hivyo 10, aliagiza uongozi wa bonde la Ziwa Victoria kufanya tathmini ya haraka ya eneo la mto Semu ambapo ndiko kunasemekana kuna maji mengi zaidi ili kivisma hivyo vichimbwe haraka.

Nae Mbunge wa Meatu, Salum Hamis, alimshukuru Prof. Mbarawa kwa kufika wilayani humo na kujionea hali halisi iliyopo, huku akiamini jitihada za haraka zitafanyika kutatua tatizo hilo.

Mbunge huyo aliongeza kuwa tatizo la maji lililopo kwa sasa ni kubwa mbali na jitihada zinazofanywa, hivyo alimuomba waziri kuhakikisha wanalitatua tatizo hilo haraka ili wananchi wasiendelee kutesema. "Sio siri, hali ya upatikanaji maji kwa wananchi wa mji wa Mwanhuzi sio mzuri, wananchi wangu wameendelea kuteseka kwa ukosefu wa maji kwa zaidi ya siku 20 na kusababisha ongezeko la magonjwa ya milipuko kipindi hiki," alisema.

Nae Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Fabian Manoza, alisema kama Wizara itafanikiwa kuchimba visima hivyo 10, vitasaidia sana wananchi kuondokana na adha kubwa ya maji wanayopata.

HABARI KIMATAIFA

## Wafanyakazi ofisi ya Waziri Mkuu wagoma

**KINSHASA, Congo**

MAMIA ya wafanyakazi waliokuwa wanajihusisha na usafi wakati wa serikali ya Rais wa zamani wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Joseph Kabila wameendelea kupiga kambi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Sylvestre Ilunga, kushikiza malipo yao.

Wanasema kwa muda wa miezi 12 sasa, hawajalipwa mshahara wao, licha ya kuwa na mkataba wa kufanya kazi, chini ya Waziri Mkuu wa zamani, Matata Mponyo.

Msemaji wa wafanyakazi hao, Jean Musenge, alisema wafanyakazi hao ambao kazi yao ni kufagia barabara za Jiji la Kinshasa, wanataka kulipwa pesa zao zote la sivyo wavunje mkataba uliopo.

"Tangu kuja kwa Waziri Mkuu Ilunga, hatujalipwa chochote, tunaomba tushughulikiwe au mkataba huu uvunjwe," alisema Musenge.

Hata hivyo, Polisi wamewazingira wafanyakazi hao ili wasiingie katika ofisi za Waziri Mkuu. Hakuna ripoti kutoka kwa Waziri Mkuu kuhusu madai ya wafanyakazi hao.

**RFI**

**"Tangu kuja kwa Waziri Mkuu Ilunga, hatujalipwa chochote, tunaomba tushughulikiwe au mkataba huu uvunjwe," alisema Musenge.**

# AG ang'aka kuzuiwa kuingia Marekani

**NAIROBI, Kenya**

MWANASHERIA Mkuu wa zamani wa Kenya, Amos Wako, amepinga vikali hatua ya Marekani kumwekea marufuku ya usafiri yeye na familia yake nchini humo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Wako alisema hatua iliyochukuliwa na Marekani dhidi yake ni kufufua kesi ya zamani ambayo haelewi lengo lake ni nini.

"Kwa miaka nane sikuwa serikalini tangu nilipostaafu japo visa vya ufisadi vimekithiri mno, jina langu halijatajwa au kuchunguzwa kuhusiana na visa vya ufisadi," alisema Wako.

Alisema sababu ya yeye kuwekewa marufuku ya usafiri mara ya kwanza ilikuwa kuhusishwa kwake na visa vya ufisadi na kwamba vyote vinatokana na kazi yake ya zamani kama Mwanasheria Mkuu.

Wako alisema haelewi kwa nini anawekewa vikwazo vipya wakati kuna marufuku inayohusiana na suala hilo miaka 10 iliyopita.

"Badala ya kukabiliana na ufisadi wanafufua visa vya zamani ambavyo havina msingi wowote," alisema Wako.

Ni mara ya pili kwa Marekani kumpiga marufuku Wako kuingia Marekani ikimtuhumu kujihusisha na ufisadi.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, marufuku hiyo ni kwa sababu ya Wako kuhusishwa na vitendo vya rushwa na ufisadi.

Hatahivyo, taarifa hiyo haikueleza ni vitendo gani vya rushwa au ufisadi ambao Wako alihusika navyo.

Hatua ya Marekani ya kumpiga marufuku Wako imechukuwa sura mpya, baada ya tume ya serikali ya kupambana na ufisadi maarufu kama EACC kusema kwamba ilishiriki kikamilifu katika hatua hiyo.

Mkuu wa tume ya EACC, Dk. Eliud Wabukala amenukuliwa na vyombo vya habari nchini Kenya akisema kuwa tume yake imekuwa msitari wa mbele kutoa habari na maelezo kuhusu ufisadi kwa Marekani na balozi za kigeni.

Wabukala alisema huenda Wakenya wengine mashuhuri wakakumbwa na hali kama iliyomfika Wako.

Wachambuzi wanasema huenda vikwazo vya usafiri vinavyomkumba Wako vilitokana na kashfa ya kifedha ya Anglo Leasing, ambayo ilisababisha serikali ya Kenya kupoteza mabilioni ya pesa.

Kashfa hiyo ililipuka wakati Wako alipokuwa akihudumu kama Mkuu wa Sheria, na alinyooshewa kidole cha lawama kwa madai ya kuwa kizuizi katika uchunguzi wa sakata hiyo.

Mwaka 2009, Naibu wa zamani wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Johnnie Carson, alitangaza Wako amepigwa marufuku kuzuru Marekani kwa madai kwamba amekuwa kikwazo kwenye vita dhidi ya ufisadi nchini Kenya.

Hatahivyo, Wako, ambaye kwa sasa ni Seneta nchini Kenya, anaweza kukanyaga kwenye ardhi ya Marekani ila tu kwenye makao makuu ya Umoja wa Mataifa (UN), ingawa haruhusiwi kwenda nje ya mipaka ya makao hayo.

Washington ilisema kuwa hatua hiyo inakusudiwa kuisadia Kenya katika vita dhidi ya ufisadi.

Wako alikuwa Mwanasheria Mkuu wa Kenya kwa muda wa miaka 20, kuanzia mwaka 1991 hadi 2011. ***BBC***




Waandamanaji nchini Iran wakichoma moto na kufunga barabara wakipinga kupanda kwa bei ya mafuta. **PICHA: FARS**

# Waandamanaji wazingirwa chuo kikuu Hong Kong

**HONGKONG, China**

WANAHARAKATI wa demokrasia wapatao 100 wamenaswa katika jengo la chuo kikuu lililozingirwa na polisi, uwezekano wao kuweza kutoroka ukizidi kupungua.

Wakati waandamanaji hao wakizingirwa, Umoja wa Mataifa (UN) umehimiza kuwapo kwa maridhiano baina ya polisi na waandamanaji.

Mamlaka ya Hong Kong imeeleza kuwa hadi saa tano usiku wa kuamkia jana, wanaharakati wa demokrasia wapatao 800 walikuwa wameondoka katika jengo hilo la chuo kikuu cha ufundi cha mjini Hong Kong, 300 kati yao wakiwa vijana wenye umri wa chini ya miaka 18.

Waliobaki ndani ya jengo hilo lililozingirwa na polisi wanajaribu kutoroka.

Msichana mmoja aliyejaribu kupita katika mfereji wa maji machafu, alisema alirudi nyuma baada ya kumuona nyoka katika mfereji huo.

Kiongozi wa Hong Kong, Carrie Lam aliwahimiza vijana wadogo waliomo katika jengo hilo kutoka nje na kukutana na wazazi wao wanaowasubiri.

Lakini pia amelaani wale aliosema wanayageuza mazingira ya chuo kikuu kuwa kiwanda cha silaha.

"Inatisha kwa chuo kikuu kimegeuka karakana ya kuunda silaha. Kulingana na taarifa nilizonazo, yamepatikana maelfu ya mabomu ya petroli ambayo hayajatumika, na kemikali zimeibiwa kutoka maabara." Alisema Lam na kuongeza kuwa:

"Baadhi ya majengo pia yanatumiwa na waandamanaji kufanya mazoezi ya jinsi ya kuwashambulia polisi"

Shirika la habari la Reuters limewaona wanafunzi wapatao 100 waliorejea nyuma baada ya kushindwa kukimbia kupitia mifereji ya maji.

Walikuwa na simulizi za kutisha, wakisema mitaro ilikuwa na harufu mbaya, mende na hata nyoka wakiwa kila mahali.

Mzozo huu wa maandamano mjini Hong Kong umeleta msuguano kati ya China, ambayo Kisiwa cha Hong Kong kiko chini ya himaya yake na Marekani inayokosoa jinsi mzozo huo ulivyoshughulikiwa.

Baraza la seneti mjini Washington limepitisha sheria ya kuunga mkono harakati za demokrasia na haki za binadamu mjini Hong Kong, ambayo inamtaka Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani kusaini agizo la angalau mara moja kila mwaka, linalotaja uhuru wa ndani kisiwa cha Hong Kong, kama sharti la mji huo kuweza kufanya biashara na Marekani.

China imeipinga vikali sheria hiyo, ikisema itafanya kila juhudi kulinda uhuru na mamlaka yake ya utaifa katika mji huo.

Umoja wa Mataifa (UN) umeitolea wito Hong Kong, wa kufanya kila liwezekanalo kupunguza mvutano baina ya polisi na waandamanaji. ***DW***

# Wachungaji EAGT wakata rufani kupinga uamuzi

**Na Hellen Mwango**

WACHUNGAJI watatu wa Kanisa la EAGT Tanzania, wamewasilisha kusudio la kukata rufani Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu uliotolewa Novemba 15, mwaka huu na Jaji Leila Mgonya.

Walalamikaji ni mchungaji Yared Lesilwa, Gilbert Weja na Petrol Kapama, kwa niaba ya wenzao 543 kutoka mikoa fofauti nchini.

Kwa mujibu wa wakili wa walalamikaji hao, Edwin Swalle, wanakata rufani kwa sababu hawajaridhika na uamuzi uliotolewa na Mahakama Kuu ikiwamo kuwataka wateja wake kuandika barua kwanza ili kuona kama wanaweza kusuluhishwa nje ya mahakama kupitia viongozi wa kanisa au la.

Wakili alidai kuwa wateja wake wanaamini kwamba mahakama ilijipotosha vibaya kwa kutoa uamuzi huo kwa sababu maombi yaliyowasilishwa mbele yake ni kutoa kibali kwa wachungaji hao watatu waweze kuwawakilisha wenzao 543 na siyo kujadili tuhuma za msingi.

"Wateja wangu wameshajaribu kutafuta muafaka nje ya mahakama bila mafanikio na hivyo chombo pekee cha kutatua mgogoro huo kati yao dhidi ya tuhuma za ubadhirifu wa mali za kanisa na ukwepaji wa kodi ni mahakamani tu, hakuna sababu ya kujadili ama kuzungumzia tena jambo hili nje ya mhimili huo," alisema Swalle.

Alidai Agosti 9, mwaka huu, Mahakama Kuu iliyoketi chini ya Jaji Mgonya, ilisema kwamba walalamikiwa wanastahili kushtakiwa binafsi na siyo bodi ya wadhamini ya kanisa hilo.

Akifafanua zaidi alisema lengo la kwenda Mahakama ya Rufani ni kuiomba iruhusu wapewe kibali cha kuendelea kuwawakilisha wachungaji wenzao 543 kutoka mikoa tofauti nchini kwa sababu itakuwa vigumu wote kusimama mahakamani ikiwamo kupoteza muda.

Katika kesi ya msingi, wachungaji hao waliiomba mahakama kuruhusiwa kuwashtaki viongozi wa Kanisa la EAGT Tanzania, walalamikiwa katika kesi hiyo ni mchungaji Christomoo Ngowi, ambaye ni mdhamini wa kanisa hilo, mchungaji Asumwisye Mwang'mbola (kwa sasa marehemu), ambaye naye alikuwa mdhamini wa kanisa hilo wakati wa uhai wake.

Wengine ni mchungaji Brown Mwakipesile, ambaye ni Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, mchungaji Leonard Mwizarubi, Katibu Mkuu na mchungaji Praygod Mgonja ambaye ni mwekahazina wa kanisa hilo kwa tuhuma za ubadhilifu wa mali za kanisa, ukwepaji wa kodi kwa kuingiza magari kinyume cha taratibu.

Ilidaiwa kuwa walipata msamaha wa kodi ya serikali wakati magari hayo hayapo kwenye orodha ya mali za kanisa na kwamba ni uvunjifu wa katiba ikiwamo kuwafukuza wachungaji bila ya kufuatia katiba ya kanisa na sheria za nchi.

Hata hivyo, kwa upande wa walalamikiwa walipinga maombi hayo wakidai kuwa wao binafsi hawapaswi kushtakiwa kwa mashtaka hayo ila bodi ya wadhamini ya kanisa hilo ndiyo ishtakiwe.

mwisho


Distributed via ippmedia

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), Emmanuel Ndomba, akizungumza na wanahabari, jijini Mwanza jana, baada ya kufungua kikao cha wadau wa mashauriano. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# AfDB yakunwa ujenzi wa umeme

**Na Mwandiahi Wetu, DODOMA**

BENKI ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeelezea kuridhishwa na kasi ya maendeleo ya mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Zuzu kinachofadhiliwa na benki hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (Jica).

Mkurugenzi Mtendaji wa AfDB, Amos Cheptoo, alisema hayo jana alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya kituo hicho kilichoko mkoani hapa.

Cheptoo alisema amejionea kazi nzuri inayofanywa na mkandarasi ya kuhakikisha mradi huo unakamilika Februari, mwakani na kutumika kikamilifu katika kupoza na kusambaza umeme kwa manufaa ya Tanzania na nchi jirani.

Alisema mradi huo utakuwa na tija zaidi baada ya kukamilika kwa mradi mkubwa wa umeme wa Julius Nyerere unaotarajia kuzalisha zaidi ya megawati 2000, hivyo kuifanya miundombinu ya kupoza umeme kutumika kimilifu.

Cheptoo alisema umeme ndiyo nyenzo muhimu katika ukuzaji wa uchumi na uendelezaji wa viwanda katika nchi za Afrika, hivyo kukamilika kwa miradi ya umeme kutasaidia uwapo wa umeme wa kutosha hasa katika nchi za Afrika Mashariki na Kusini.

Serikali ya Tanzania imechukua hatua nzuri za kuboresha miundombinu wezeshi ya uzalishaji hasa Dodoma ambako ndiko makao makuu ya nchi.

Matibu wa mradi huo, Mhandisi Peter Kigandye, alisema mradi huo utakuwa na uwezo wa kushusha umeme kwa kilovoti 400 na kupoza umeme wenye uwezo wa takribani megawati 400 kisha kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali mkoani Dodoma. Gharama ya mradi huo unajumuisha mradi mwingine ulioko Singida na gharama zake ni Dola za Marekani milioni 53 ambazo zimetolewa kwa ushirikiano wa serikali ya Tanzania, AfDB na Jica. Ujenzi kituo cha Zuzu unagharimu takribani Dola za Marekani milioni 22.

Kamishna Msaidizi wa Nishati ya Umeme kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga, aliishukuru AfDB kwa kusaidia uboreshaji wa miundombinu hasa ya umeme kwa kuwa miradi hiyo itakapokamilika, utazinufaisha pia Zambia, Botswana na Afrika Kusini, kupitia mtandao wa umeme wa kusini.

Aliwataka wawekezaji wenye nia ya kuwekeza Dodoma kutumia fursa ya upatikanaji wa umeme wa uhakika kuwekeza hasa katika viwanda vikubwa na vidogo kwa kuwa mazingira ya uwekezaji yapo vizuri.

# Kamishna maadili atoa somo UDOM

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

KAMISHNA wa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi nchini Kenya, Rose Macharia, amezitaka nchi za Afrika Mashariki kushirikiana kupambana na rushwa kwa kuwa haina mipaka.

Alisema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa pamoja na baadhi ya viongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na wa Sekretarieti ya Maadili kilichofanyika chuoni hapo.

Macharia aliwataka viongozi wa Afrika Mashariki wanaohusika na kupambana na ufisadi kuhakikisha wanalisimamia vizuri suala hilo kwa sababu uhalifu huo hauna mipaka na wahusika wanaweza kushirikiana na wengine wa nchi jirani.

"Mtu au kundi la watu linaweza kushirikiana na wengine wa nchi jirani au ya ng'ambo wakafanya uhalifu kwa kuiibia serikali, hivyo viongozi wetu wakuu wa nchi na taasisi za kumpanana na rushwa au ufisadi wahakikishe wanalisimamia hilo," alisema.

Pia alisema lengo la msafara wake kufika UDOM ni kujifunza chuo hicho kinavyosimamia maadili ya wanafunzi na watumishi.

"Tume yetu iliwahi kupata taarifa ya mipango mikakati ya chuo hiki katika kupambana na rushwa, hivyo leo (jana) tumefika kujifunza zaidi na kubadilishana uzoefu wa namna ya kupambana na ufisadi," alisema.

Kamishna Macharia alisema baada ya ziara hiyo, wamefurahishwa na uongozi wa Udom ulivyojipanga katika kusimamia maadili ya wanafunzi na watumishi wote wa chuo.

Alisifu pia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Sekretarieti ya Maadili zilivyojipanga kufanya kazi kupitia makundi na taasisi mbalimbali.

Kaimu Makamu Mkuu wa UDOM, Prof. Justin Ntalikwa, alisema chuo hicho kina idadi kubwa ya wanafunzi na watumishi, hivyo wamejipanga kwa kila eneo ili kupambana na utovu wa nidhamu.

Prof. Ntalikwa alisema UDOM ina idadi kubwa ya watu, hivyo wanafanya kazi kila wakati kuhakikisha wanalinda maadili ya kundi hilo lenye zaidi ya WATU 20,0000 ndani ya chuo. Mwenyekiti wa Kamati ya maadili ya UDOM, Dk. Ombeni Msuya, alisema chuo hicho kimeanzisha mfumo maalum ndani ya chuo wa kutoa taarifa za utovu wa nidhamu kwa watumishi na wanafunzi.

"Kwa kutumia mfumo huu tulioanzisha mwanafunzi anaweza kuwasiliana kwa njia ya siri na kamati yetu ya maadili kuhusu kuombwa rushwa ya fedha au ngono na mwalimu wake na kamati kwa kushirikiana na uongozi wa chuo na polisi watalifanyia kazi haraka na mhusika kukamatwa," alisema.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO


NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311


## 2 ACRE YARD FOR RENT

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku



## VYETI VIMEPOTEA



**GERALD PENDO SOSTHENES** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0611/0093 kilichotolewa na KABANGA SEKONDARI mwaka 2015. Certificate in Animal Health and Production chenye namba CAHP/08/808/2013 kilichotolewa na LITA KIKULULA INSTITUTE mwaka 2012. Diploma in Animal Health and Production yenye namba NS0611/0093/2012 kilichotolewa na LITA MOROGORO INSTITUTE mwaka 2016/2017.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa ya polisi: DSM/PHQ/RB/454619/2019.**

## PASSPORT IMEPOTEA




**LAMECK PHILEMON NDOSSY**
anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba AB 191718 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam November, 2006.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi:
**DAR/KIJ/RB/487986/2019.**

## KUPOTEA KWA CHETI



115527402

**Mayange Robert Mwaimu** anatangaza kupotea kwa cheti cha Kidato cha nne chenye index namba **S4928/0066** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Living Stone Boy's Seminary.Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/RB/489730/2019**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KALPESH JAYSINH ASHER** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 222 BYM TOYOTA CAMRY.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/RB/1350/2019.**

115527202

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GODFREY JOHN MBOGELAH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 195 BAE TOYOTA SPACIO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/RB/135/2019.**

115527302

## ROYAL EAST COAST COMMODITIES TANZNAIA LIMITED

### MEMBER'S VOLUNTARY WINDING UP OF THE COMPANY THE COMPANIES ACT, 2002

Notice is hereby given that; the members of ROYAL EAST COAST COMMODITIES TANZANIA LIMITED have resolved to wind up the Company voluntary and that Mr. MR. HAMZAALI AMIRALI PATWA of H. A PATWA & COMPANY located at Zahra Tower,MZ 03, Plot number 66/99, Zanaki/Indira Gandhi Street, Kisutu Ward, Ilala CBD, P.O Box 4509, Dar es Salaam, Tanzania has been appointed as liquidator for the Purpose of winding up the Company.

Creditors of ROYAL EAST COAST COMMODITIES TANZANIA LIMITED are required on and before 20th day of December,2019 to send their names and addresses with full particulars of their debts or claims against the said Company to the liquidator and proof of their debts or claims against the said Company to the liquidator and proof of their debts or claims. Creditors will be excluded from the benefits of any distribution made before such debts are proved.

***Dated this 20th day November, 2019***



LIQUIDATOR

115526702

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**


**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;220/2019**

**Ombi la AYUBU YUSUPH HASSAN**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SAIDI IDDI CHALAA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/11/2019



115526402

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

Distributed via ippmedia

STEPHEN JOSEPH NGOWI anatangaza kupotelewa na kadi pikipiki yenye namba za usajili MC 685 BLS model HAOJUE. Yenye chasis namba: LC6PCJK2XG0044071.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi:**
**MOR/MOR/RB/488727/2019.**

115526502

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**THOBIUS NGONYANI** LYANDER anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili MC 187 AWE – TVS KING. Chassis namba MD6M14PK8F4F78972. Engine namba OK4FF4239899.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
MAG/RB/5371/2019.

115526202

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ELIREHEMA METASHEYE MUNGURE** anatangaza kuibiwa kwa kadi za pikipiki zilizosajiliwa kwa namba zifuatazo.MC 726 BFY, MC 658 BLD, MC 879 BVZ,MC 576 CAK, MC 851 CBE, MC 824 AUG na MC 556 AKN.

Tukio limeripotiwa kituo cha polisi 05/11/2019 na kupewa namba

**ARU/ARU/RB/486765/2019.**

115526602


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ENRIQUE
## AREJEA KUINOA HISPANIA



**MADRID, Hispania**

LUIS Enrique alirudi kwenye kazi yake ya ukocha wa Hispania Jumanne, akitoka kustaafu kwa muda Juni mwaka huu kutokana na matatizo binafsi.

Miezi miwili baadaye, kocha huyo wa zamani wa Barcelona alipatwa na msiba wa mtoto wake wa kike mwenye umri wa miaka tisa, Xana ambaye alifariki baada ya kuugua saratati ya mifupa kwa miezi mitano.

Kwa kipindi ambacho hakuwapo, Roberto Moreno alichukua majukumu ya kuinoa timu hiyo, lakini Septemba mwaka huu alisema kwamba angekaa pembeni kama Enrique angerudi kikosini hapo.

Baada ya ushindi wa Hispania wa 5-0 dhidi ya Romania, ambao ulimaliza kapeni yao ya kufuzu Euro 2020, chanzo kimoja kiliitonya ESPN FC kwamba, Moreno angeondolewa kwenye nafasi yake hiyo.

"Ilikuwa ni wazi kwamba, wakati Enrique atakapotaka kurudi, ingekuwa hivyo," Rais wa Shirikisho la Soka la Hispania, Luis Rubiales alisema kwenye mkutano wake na wanahabari mjini Madrid Jumanne.

"Nilisema wakati naondoka aliweka uwezekano mkubwa wa kurudi, mlango ulikuwa wazi. Tumekuwa na furaha na Robert. Tunamshukuru kwa kasi yake, lakini kiongozi wa mradi huu alikuwa Luis Enrique."

Moreno bado hajazungumza chochote hadharani, akiwa pia alikataa kuzungumza kwenye mchezo dhidi ya Romania wakati uvumi tayari ulikuwa unazungumza kuhusu majaliwa yake.

## MARADONA AJIUZULU KUINOA GIMNASIA

**BUENOS AIRES, Argentina**

DIEGO Maradona amejiuzulu nafasi ya ukocha wa timu ya Daraja la Kwanza ya nchini Argentina ya Gimnasia La Plata baada ya kuwa kwenye nafasi hiyo kwa kipindi cha miezi miwili na klabu hiyo ikiwa kwenye hatihati ya kushuka daraja.

Gimnasia inashika nafasi ya 22 kwenye msimamo na Maradona akishinda mechi tatu na kupoteza tano kati ya nane.

Uamuzi ya Maradona kuondoka kwenye nafasi hiyo ulitangazwa na Rais wa Gimnasia, Gabriel Pellegrino kwamba hataendelea kuwa kwenye nafasi hiyo.

Pellegrino amekuwa kwenye timu hiyo tangu mwaka 2016 na gwiji huyo wa Argentina akaamua kustaafu.

"Maradona si kocha wa Gimnasia," alisema Pellegrino.



## TITE AKANA RASMI KUMBAGUA RODRYGO

**ABU DHABI, Falme za Kiarafu**

KOCHA Tite amekataa shutuma dhidi yake kwa kumchezesha Rodrygo Goes dakika mbili tu wakati Brazil ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Korea Kusini, juzi Jumanne.

Kocha huyo wa timu ya Taifa ya Brazil alisema Jumatatu kwamba atakuwa na subira kwa fowadi huyo kinda, ambaye ameanza vizuri maisha yake ya soka pale kwenye klabu ya Real Madrid.

Rodrygo amefunga mara mbili kwenye mechi nne alizocheza Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, akiwa na Madrid na alifunga mabao matatu 'hat-trick' wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Galatasaray mapema mwezi huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, alicheza kwa dakika 19 akianza kwa mara ya kwanza kuichezea Brazil wakati ikifungwa 1-0 na Argentina Ijumaa na alipewa dakika chache zaidi kwenye mchezo wa juzi mjini Abu Dhabi.



"Ni jambo moja kumuingiza Rodrygo kwenye mfumo ambao tayari umeshajengwa, kama ilivyo Real Madrid. Ni kitu kingine kumuweka yeye kwenye timu ambayo inaendelea kujengwa, hata kama ilikuwa kazi sawa katika nafasi yake," alisema Tite.

"Ilikuwa ni ngumu kuiunganisha timu kwa mchezo wa leo (juzi) na namna walivyocheza. Walikaribia kufunga bao la nne na la tano.

"Ilikuwa nafasi kwa Fabinho, Renan Lodi na Militao. Walipata nafasi wakashindwa kuzitumia wao wenyewe. Ingekuwa kwa Rodrygo? Ndio, lakini niliona bado aendelea kusubiri wakati muafaka."

HABARI MICHEZO



# MARTINEZ

## AIPA UBELGIJI UBINGWA EURO 2020

**BRUSSLES, Ubelgiji**

ROBERTO Martinez anaamini Ubelgiji wanastahili kushinda Euro 2020, lakini akabainisha kwamba, si kitu rahisi kama hawataonyesha kiwango cha juu.

Ubelgiji walifuzu kucheza michuano hiyo Jumanne, kwa kuifunga Cyprus mabao 6-1 na kumaliza kampeni hiyo kwa kushinda mechi zote 10 za Kundi I, wakifunga jumla ya mabao 40.

Kocha huyo wa Ubelgiji, Martinez tayari ameonyesha kwamba wanaweza kushinda taji hilo, lakini akasema kuna kazi kubwa ya kufanya.

"Kama tunaweza kushinda taji la Ulaya, hilo ni jambo ambalo lipo mikononi mwetu," alisema kocha Martinez.

"Tunahitaji kuwa bora zaidi na kuona kama tunaweza kucheza michuano mingine mikubwa.

"Tulitengeneza kiwango bora wakati tulipomaliza nafasi ya tatu kwenye michuano ya Kombe la Dunia na tunaendelea kuimarika kama timu na mashabiki pia ni muhimu kwetu.

"Tunajua kwamba tuna miezi saba kuwa kwenye kiwango bora. Timu hii inastahili kushinda taji, lakini kwenye soka si jambo rahisi la kuzungumza tu."

Akiangalia namna walivyofuzu, aliongeza kusema: "Nafikiri kila mmoja alifanya kazi yake vizuri mwaka huu. Wachezaji wanajua nini cha kufanya na wanafanya kwa kujituma kweli kweli."

Distributed via ippmedia

# Pochettino anastahili sanamu Spurs- Crouch

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Tottenham, Peter Crouch, ameachwa na "mshituko" kwa Spurs kumfukuza kocha, Mauricio Pochettino, akidai klabu hiyo ilitakiwa kumzawadia heshima ya kumjengea sanamu.

Pochettino pamoja na benchi lake lote la ufundi walifukuzwa Jumanne baada ya Tottenham kutoshinda mchezo wowote kati ya mitano ya Ligi Kuu iliyopita na wapo nafasi ya 14.

Lakini kocha huyo wa zamani wa Southampton aliiongoza Spurs kucheza fainali yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Juni mwaka huu, baada ya kuwafunga Manchester City na Ajax kabla ya kufungwa na Liverpool kwenye fainali.

Crouch, ambaye alitokea kwenye akademi ya Tottenham na kuichezea klabu hiyo kati ya mwaka 2009 na 2011, anaamini mafanikio ya Pochettino hayakupaswa kusahauliwa haraka hivyo.

"Nimeshitushwa mno kwa maamuzi ya Tottenham," alisema mchezaji huyo wa zamani wa England, Crouch, akiwa ameandika kwenye Gazeti la Daily Mail.

"Najua matokeo yamekuwa mabaya na naelewa kwa nini timu kubwa zinachukua uamuzi wakati matarajio yao ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya yanapoonekana kuwa kwenye wasiwasi, lakini ni upuuzi kufikiri Pochettino amepoteza uwezo wake haraka.

"Aliiongoza Tottenham kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Juni Mosi. Klabu nyingine zingefikia hatua hii, zingemjengea sanamu ya heshima kocha kwa mafanikio makubwa aliyofika kwenye soka.

"Lakini Pochettino amepata kitu tofauti na matarajio ya wengi. Nahofia kwa uamuzi huu Tottenham watajutia."

Jose Mourinho ndiye amechukua mikoba ya Pochettino hapo Tottenham Hot

# Giggs apagawa Wales ikifuzu Euro 2020



**CARDIFF, Wales**

RYAN Giggs ameisifia juzi, Jumanne kuwa moja ya siku bora zaidi kwenye maisha yake baada ya Wales kufuzu kucheza michuano ya Euro 2020 kwa ushindi wa 2-0 dhidi ya Hungary.

Aaron Ramsey alikuwa shujaa kwenye mchezo huo uliochezwa Cardiff, akifunga bao katika kila kipindi wakati Wales wakipata nafasi hiyo ya kufuzu na kuwa nafasi ya pili nyuma ya Croatia kwenye Kundi E.

Wakati akianza kampeni hiyo akiwa kocha wa kikosi cha Wales, Giggs alihitaji ushindi katika kila mchezo ili kuweza kufuzu kwa michuano hiyo.

Ushindi dhidi ya Azerbaijan wikiendi iliyopita kabla ya ushindi huo wa nyumbani, unawafanya wao wafuzu kucheza michuano hiyo mikubwa zaidi kwa Mataifa ya Ulaya.

"Ni zaidi ya kila kitu kwenye maisha yangu," alisema Giggs akiiambia Sky Sports. "Inafurahisha. Ukiangalia kule tulikokuwapo wakati wa kipindi cha majira ya joto (nyuma ya Croatia na Hungary), shukrani kubwa kwa wachezaji wote.

"Wameonyesha kuwa tukiamua tunaweza kufuzu. Hii ni moja ya siku bora kwenye maisha yangu ya soka."

Majeraha ya Ramsey yalimaanisha kwamba, nyota huyo wa Juventus alikuwa akicheza kwa mara ya kwanza kwenye michuano hiyo ya kufuzu Jumanne.

"Alionyesha ubora wake, ni wa daraja la juu," alisema Giggs.

Akiwa hajawahi kuichezea Wales kwenye michuano yoyote mikubwa wakati akiwa mchezaji pale Manchester United, Giggs sasa ataiongoza nchini yake kwenye michuano hiyo akiwa kocha.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MOURINHO: SABABU KUMRITHI POCHETTINO

Ubora katika kikosi na kufanya kazi na wachezaji hawa ndicho kilichonivutia...

**LONDON, England**

Jose Mourinho amefunguka baada ya Tottenham kumteua kocha huyo wa zamani wa Manchester United kurithi viatu vya Mauricio Pochettino aliyetimuliwa juzi usiku.

Mourinho, 'The Special One', ametua Tottenham, ambayo imemtimua Pochettino ikiwa ni miezi mitano tu baada ya klabu hiyo kuweka rekodi kwa kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza.

Tottenham imeamua kufanya mabadiliko mwishoni mwa kipindi cha mapumziko ya kimataifa, wakati huu ikisumbuka katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya raundi 12.

"Nimefurahi kujiunga na klabu na urithi mkubwa na mashabiki wenye shauku kama hii," Mourinho alisema katika taarifa kufuatia kuteuliwa kwake kuinoa hadi mwishoni mwa msimu wa wa 2022-23.

"Ubora katika kikosi na shule ya makinda inanifurahisha. Kufanya kazi na wachezaji hawa ndicho kilichonivutia."

Mourinho alitimuliwa na wapinzani wa Spurs kwenye Ligi Kuu England, Manchester United Desemba mwaka jana lakini kocha huyo wa zamani wa Chelsea amerejea tena kibaruani hapo London, ambapo Mreno huyo atajaribu kuuokoa msimu wa Tottenham.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 56, mshindi mara tatu wa ubingwa wa England katika vipindi vyake viwili tofauti akiwa uongozini hapo London na Chelsea, alishuhudia miaka yake miwili na nusu akiinoa United ikihitimishwa huku timu ikiwa na kiwango kibovu na kuripotiwa kukwaruzana na wachezaji kikosini.

Mourinho, ambaye pia alitwaa mataji matatu akiwa na Inter mwaka 2010 na kuiongoza Real Madrid kubeba ubingwa wa LaLiga msimu wa 2011-12, kisa cha kufunguliwa mlango Old Trafford kilianzia kwa kukwaruzana na Paul Pogba.

Kocha huyo wa zamani wa Porto amekuwa akihusishwa na Inter kabla ya Antonio Conte kuteuliwa kuinoa timu hiyo ya Italia, wakati Mourinho aliripotiwa pia kuwa katika mstari wa kujiunga na Bayern Munich kufuatia Niko Kovac kutimuliwa.

Kurejea Madrid pia kulizungumzwa wakati Zinedine Zidane awali akihaha kuirejesha katika kiwango miamba hiyo ya LaLiga, lakini Mourinho sasa atajiandaa kwa safari ya kuifuata West Ham Jumamosi kwenye mechi ya Ligi Kuu England.

## KWA UFUPI

**STERLING, CITY WATETA**
Manchester City imefungua mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wa kimataifa wa England, Raheem Sterling, 24. ***(Mirror)***

**POCHETTINO KUIGHARIMU SPURS**
Tottenham Hotspur italazimika kutumia pauni milioni 19.6 kama fidia kwa kocha Mauricio Pochettino na benchi la ufundi ambazo Manchester United ilimlipa Jose Mourinho na wasaidizi wake Desemba 2018. ***(Mirror)***

**BAYERN YAMFUATA PARROTT**
Bayern Munich inafuatilia maendeleo ya mshambuliaji kinda wa Tottenham na Jamhuri ya Ireland, Troy Parrott, 17. ***(Mail)***

**CHELSEA BADO UAMUZI CAS**
Chelsea ilitinga Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo (CAS) Alhamisi kujaribu kupindua kifungo chao cha kusajili, lakini pengine haitapata suluhisho kabla ya dirisha la usajili la Januari kufunguliwa. ***(Times)***

**HAALAND KUITOA UNITED**
Manchester United itapaswa kulipa hadi pauni milioni 85 kumsajili mshambuliaji wa Red Bull Salzburg, Mnorway Erling Braut Haaland, 19. ***(Standard)***

**TERRY APUUZA UVUMI AGUERO**
NAHODHA wa zamani wa Chelsea, John Terry amepuuzia madai kuwa ameitaka 'Blues' kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Sergio Aguero kabla ya kutua Manchester City. ***(Mirror)***

**SWANSEA, STOKE KWA HAYES**
Swansea City na Stoke City zinamtaka winga wa Jamhuri ya Ireland, Jonny Hayes, 32, wakati atakapomaliza mkataba wake. ***(Scottish Sun)***

**UNITED KUTESEKA KAZAKHSTAN**
WACHEZAJI wa Manchester United wameambiwa wanapswa kutotoka nje kwa zaidi ya dakika 10 wakati watakaposafiri kwenda kucheza na FC Astana kwenye mechi ya Europa League kwa sababu ya hali ya baridi kali iliyopo Kazakhstan. ***(ESPN)***

**MORENO KUFUNGA KUTIMULIWA**
Robert Moreno atatoa maoni yake juu ya nafasi yake ya kocha mkuu wa Hispania kuzibwa baada ya mkataba wake kukatishwa. ***(AS - in Spanish)***

**ENGLAND KUJIFUA NEWCASTLE**
UWANJA wa Newcastle United, St James' Park unapewa nafasi ya kuwa mwenyeji wa moja ya dimba ambalo England itautumia kwa ajili ya kujifua kwa michuano ya Euro 2020. ***(Times)***

**LEEDS KUMPIGA BEI COYLE**
Leeds ipo tayari kumuuza beki Muingereza Lewie Coyle, 21, katika dirisha la Januari ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo Fleetwood. ***(Football Insider)***



## HABARI MICHEZO

# MTIBWA KUIVAA BIASHARA UNITED KWA TAHADHARI

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI jana ikiondoka mjini Morogoro kwa safari ya kuelekea Musoma kuivaa Biashara United, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila amesema watashuka dimbani kwa tahadhari kubwa kutokana na kutambua ubora wa wapinzani wao hususan wanapokuwa nyumbani.

Jumamosi Mtibwa itashuka katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume kuvaana na Biashara United katika muendelezo wa Ligi Kuu Bara iliyokuwa imesimama kupisha mapumziko ya mechi za kimataifa.

Akizungumzia mechi hiyo kabla ya kuelekea mjini Musoma jana, Katwila alisema mara nyingi Biashara United huwa si rahisi kufungwa ikiwa nyumbani, lakini atawapa wachezaji wake mbinu mbadala ili kuweza kuibuka na ushindi.

"Kesho (jana alfajiri) tutaondoka kuelekea Musoma kwa ajili ya kujiandaa kukutana na timu ya Biashara United lengo ni kupata pointi tatu.

"Tutacheza kwa tahadhari kwa sababu Biashara kufungwa nyumbani kwao huwa si rahisi, lakini naamini tutashinda,"alisema kocha huyo.

Alisema wachezaji wake wote wapo vizuri na kudai kila mmoja ana morali ya ushindi.

"Lengo ni kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ili kuifanya Mtibwa kuwa na ubora wa hali ya juu," alisema.

Mtibwa inashika nafasi ya saba ikiwa na alama 15 baada ya kushuka dimbani mara 11 wakati Biashara United ipo katika nafasi ya 17 ikiwa na pointi nane kufuatia kucheza mechi 10.



Distributed via ippmedia

Mshindi wa Sh. milioni 393 wa mchezo wa kubashiri wa Perfect 12 wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, Salvatory Kambaulaya ( wa pili kulia), akiwa katika picha ya pamoja na Meneja Masoko wa kampuni hiyo, Allen Mushi (wa pili kushoto) baada ya kukabibidhiwa mfano wa hundi kwa kushinda kitita hicho. Kushoto ni Chiku Saleh kutoka bodi ya michezo ya kubashiri na kulia ni Shabani Mwanga, Mkuu wa Kitengo cha Kodi za Michezo ya Kubahatisha (TRA), Mkoa wa Kodi wa Ilala. **MPIGAPICHA WETU**

# Kili Queens waisulubu Z'bar Queens

**Na Somoe Ng'itu**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la Chalenji kwa Wanawake, timu ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens), imeendelea kutoa dozi katika michuano hiyo baada ya kuifunga Zanzibar Queens mabao 7-0 katika mchezo uliopigwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam jana.

Kwa matokeo hayo, wenyeji Kilimanjaro Queens wamefikisha pointi tisa na kumaliza mechi za hatua ya makundi wakiwa kileleni katika Kundi A na kufuatiwa na Burundi yenye pointi sita.

Kilimanjaro Queens inayonolewa na Kocha Mkuu, Bakari Shime, sasa inasubiri kujua mpinzani wake katika hatua ya nusu fainali mpaka mechi za Kundi B zitakapomalizika leo jioni.

Mabao ya Kilimanjaro Queens katika mchezo wa jana yalifungwa na Donisia Minja na Asha Rashid wakipachika wavuni mabao mawili kila mmoja, Diana Lucas, Philomena Daniel na Anastazia Katunzi.

Zanzibar Queens na Sudan Kusini ambayo mapema mchana ilifungwa mabao 3-0 na Burundi, zimeshatolewa katika michuano hiyo ambayo mwaka huu inachezwa kwa msimu wa tatu.

Michuano hiyo inatarajiwa kuendelea tena leo kwa Ethiopia kucheza dhidi ya Djibouti ambazo zote zimeshatolewa na zitacheza kukamilisha ratiba huku mchezo kati ya Uganda ikiivaa Kenya ndio utatoa kinara wa Kundi B na mshindi wa pili.

Kabla ya mechi, wachezaji wa Zanzibar Queens waliimba pia wimbo wa Taifa wa Tanzania pamoja na nyota wa Kilimanjaro Queens baada ya kumaliza kuimba nyimbo ya Visiwani.

Baada ya kumalizika kwa mchezo, wachezaji wa timu zote mbili walishikana mikono na kuunganisha duara moja wakimaanisha kudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

# Shabiki Simba asimulia ushindi mil. 393/-

**Na Mwandishi wetu**

SHABIKI wa Simba kindakindaki, Salvatory Kambaulaya, mkazi wa mkoa wa Iringa, amejishindia kitita cha Sh. milioni 393.2 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 za mchezo wa Perfect 12 unaoendeshwa na Kampuni ya M-bet Tanzania.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa hundi yake wiki hii, Kambaulaya ambaye pia ni shabiki wa Manchester City ya England, alisema hakuwa na wasiwasi baada ya kupigiwa simu na Meneja Masoko wa Kampuni ya M-Bet, Allen Mushi kuwa ni mshindi wa fedha hizo.

"Niliamini kuwa ni mshindi kwani mimi si mtu wa kwanza kushinda droo ya Perfect 12 ya M-Bet kutoka Mkoa wa Iringa, kuna mwanafunzi alishawahi kushinda na kupatiwa fedha zake.

"Ninaamini M-Bet kwa kuwa na washindi wa uhakika katika michezo yao, ndiyo maana nilicheza 'mikeka' saba, mmoja nikipatia mechi tisa na mwingine mechi 12," alisema Kambaulaya.

Alisema kiasi cha fedha alichoshinda ni kikubwa sana na anatakiwa kutuliza akili ili kujua nini anafanya kwa upande wa maendeleo.

"Nimeshinda zawadi ya kwanza, lakini nimeumia sana na matokeo kati ya timu yangu, Manchester City ilipofungwa na Liverpool, niliweka Manchester kuwa ni washindi, hata hivyo alifungwa mchezo huo.

Meneja Masoko wa M-Bet Tanzania, Mushi alisema Kambaulaya ambaye ni Ofisa wa Jeshi la Polisi mkoani Iringa, ataweza kubadili maisha yake kupitia mchezo wa Perfect 12.

Mushi alisema M-Bet itaendelea kuwa nyumba ya mabingwa ambao wamefaidika na mchezo huo tokea kuanza kwa ubashiri.

"Tumetoa washindi wengi mpaka sasa ambao wamejishindia mamilioni ya fedha na kuweza kubadili maisha yao ya kila siku," alisema Mushi.

# MOROCCO AIJARIBU ZANZIBAR HEROES

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes) imecheza mchezo wa kirafiki wa kwanza tangu kutangazwa kikosi hicho kinachoundwa na wachezaji 47 na kuambulia sare tasa.

Katika mechi hiyo dhidi ya Kombaini ya Vikosi vya Ulinzi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) iliyopigwa katika Dimba la Amaan majira ya saa kumi jioni juzi, ilikuwa maalumu kwa ajili ya kumsaidia Kocha wa Zanzibar Heroes, Hemed Morocco kujua hatua waliofikia nyota hao kabla ya kuanza kufanya mchujo.

Akizungumza na waandishi wa habari mshambuliaji wa Zanzibar Heroes, Hamad Hilika, anayeichezea timu ya Zimamoto, alisema wamezidi kuimarika tofauti na awali wakati walipoitwa.

Alisema changamoto iliyopo kikosini hapo ni kwamba wachezaji wengi hii ni mara yao ya kwanza kuitwa kuitumikia timu hiyo, hivyo wanahitaji muda zaidi kuweza kuzoeana.

Kwa mujibu wa Kocha Mkuu, Morocco, kikosi hicho cha Zanzibar Heroes ambacho ni cha awali, kitafanyiwa mchujo Novemba 26 na kisha kujumuika na wale walioitwa ambao wanacheza soka Ligi Kuu Bara.

# Michezo

Alhamisi Novemba 21, 2019

Nipashe




## Mourinho: Sababu kumrithi Pochettino

HABARI UK 30

TUMEFUZU...




Distributed via ippmedia

Aaron Ramsey akishangilia na wachezaji wenzake Gareth Bale na Joe Allen (kulia), baada ya kufunga bao lake la pili na kuipa Wales ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Hungary, hivyo kufuzu michuano ya Euro 2020. **HABARI UK. 29**

# AUSSEMS AWEKWA KANDO RASMI SIMBA

## ●●●Achungulia dili la kuinoa Polokwane ya Afrika Kusini, Kaduguda, Try Again waula kwa kuteuliwa kuwa...

**Na Somoe Ng'itu**

HAYAWIHAYAWI sasa yamekuwa! Hii ni baada ya uongozi wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, kumweka pembeni Kocha wake Mkuu, Mbelgiji Patrick Aussems katika mechi ya ligi dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Simba imefikia uamuzi huo kutokana na kukerwa na tabia ya kocha huyo kuondoka nchini na kudaiwa kwenda kwao Ubelgiji kwa matatizo binafsi bila ruhusa ya mwajiri wake. Hata hivyo, imedaiwa kuwa wala hakwenda Ubelgiji bali alikuwa nchini Afrika Kusini.

Taarifa zilizopatikana jijini jana kutoka chanzo chetu ndani ya klabu ya Simba, zimeeleza kuwa mabosi wa juu wa klabu hiyo wamesema kwamba kitendo kilichofanywa na Aussems si sahihi na wanaona si busara kumpa nafasi ya kukiongoza kikosi chao kwenye mchezo huo wa ligi.

"Aussems alikwenda Afrika Kusini kufanya mazungumzo ya kujiunga na klabu ya Polokwane inayoshiriki Ligi Kuu nchini humo baada ya kuieleza Simba atakuwa nje ya Tanzania kwa muda wa siku tatu kutokana na kuwa na matatizo binafsi," kilieleza chanzo chetu.

Kutokana na Aussems kusimamishwa, kikosi cha vinara hao wa ligi kitaongozwa na Kocha Msaidizi, Dennis Kitambi pamoja na kiungo mshambuliaji wa zamani wa timu hiyo, Mussa Hassan "Mgosi".

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Senzo Mazingisa, juzi alinukuliwa akieleza kuwa Aussems alimtumia ujumbe ukimwarifu kuwa amepatwa na dharura lakini hakuainisha kuwa ameelekea wapi.

**KADUGUDA AULA**

Katika hatua nyingine, uongozi wa klabu hiyo, umemtangaza rasmi, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, Mwina Kaduguda "Simba wa Yuda" kuwa Kaimu Mwenyekiti wa klabu hiyo ya jijini Dar es Salaam.

Kaduguda ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Tanzania (FAT sasa Shirikisho la nchini -TFF) na Mwenyekiti wa Chama cha Makocha Tanzania (TAFCA), ndiye mjumbe mwenye muda mrefu ukilinganisha na wajumbe wengine wa bodi hiyo.

Uteuzi wa Kaduguda umeanza rasmi juzi na hiyo imetokana na uamuzi wa aliyekuwa Mwenyekiti, Swedi Mkwabi, kutangaza kujiuzulu kutokana na kubanwa na majukumu yake binafsi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Masingiza, ilisema pia imemteua Kaimu Rais wa zamani, Salim Abdallah "Try Again" kuwa Makamu Mwenyekiti wa bodi wa klabu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini.

Masingiza alisema pia katika taarifa yake kuwa bodi hiyo itatangaza hivi karibuni, tarehe rasmi ya uchaguzi mdogo wa kujaza nafasi hiyo ya Mkwabi.

"Uteuzi huu umefanyika kwa mujibu wa Ibara ya 50 ya Katiba ya Simba ya mwaka 2018, tunaamini kila mmoja atatekeleza majukumu yake kikamilifu," alisema Masingiza.

Taarifa za ndani kutoka Simba zinasema kuwa kabla uamuzi wa kumtangaza Kaduguda kupewa cheo hicho, vilifanyika vikao mbalimbali ili kuweka mambo sawa na kuimarisha umoja ndani ya wajumbe wote wa bodi hiyo.

## Samatta: Sababu kichapo Libya hii

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupoteza mechi dhidi ya Libya, nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta, ametoa sababu ya kupokea kipigo hicho huku Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije akisema nafasi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021 bado ipo na mapambano yanaendelea.

Samatta amekiri kikosi chao kilizidiwa uwezo na wapinzani hasa katika kipindi cha pili cha mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Olimpiki mjini Montasir nchini Tunisia.

Katika mchezo huo wa pili wa Kundi J, Taifa Stars iliyomaliza kipindi cha kwanza ikiwa inaongoza kwa bao 1-0, ilifungwa mabao 2-1 na hivyo kukaa katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa kundi hilo linaloongozwa na Tunisia yenye pointi sita baada ya juzi ikiwa ugenini nayo kuichapa Equatorial Guinea bao 1-0.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Samatta, alisema Libya walikuwa wazuri zaidi katika kipindi cha pili ukilinganisha na wao na wenzao walitumia vizuri nafasi mbili walizozipata kufunga mabao hayo yaliyowapa ushindi katika mechi hiyo.

Samatta alisema hawakuwa na bahati ya kupata ushindi katika mechi hiyo, lakini bado nafasi ya kujirekebisha na kufanya vizuri kwenye mechi iliyobakia wanayo.

"Hatukucheza vizuri katika kipindi cha pili, wenzetu waliingia na nguvu zaidi ukilinganisha na sisi, na walitumia vizuri nafasi mbili walizopata, sisi tulitengeneza nafasi nyingi katika kipindi cha kwanza lakini hatukuwa makini zaidi," alisema nahodha huyo anayecheza soka la kulipwa nchini Ubelgiji katika klabu ya KRC Genk.

Naye Kocha Mkuu wa Stars, Ndayiragije alisema hajafurahishwa na matokeo ya mchezo huo lakini ameongeza kuwa bado wataendelea kuongeza kasi ili kusaka ushindi kwenye mechi zinazofuata.

Ndayiragije alisema kuwa mechi ilikuwa ngumu na yenye ushindani, lakini wachezaji wake wameendelea kupambana kuhakikisha wanapata ushindi, lakini juzi haikuwa siku nzuri kwa Taifa Stars.

"Bado tuna nafasi, tutaendelea kutumia nguvu na kasi katika mechi zinazokuja, naamini tutafanya vizuri na kukaa kwenye nafasi nzuri kwenye kampeni hii," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >